# Nipashe

Jumanne Januari 22, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579820

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US







## Adaiwa kumuua mdogo wake kisa mgawo kishika uchumba

UKURASA 3

UKURASA 13



# Dakika 221 za CAG bungeni

UK. 2



Picha tofauti zikimwonyesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, akiwasili, akihojiwa na Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka, katika Ofisi za Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA ZOTE: IBRAHIM JOSEPH**

## Zanzibar yapata msamaha bil. 23/- Tanesco

UKURASA 3



## Upigaji wa kutisha chanjo mifugo

• **Chanjo** ya 20,000/- mfugaji anailipia mil. 1/- *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **AUSSEMS AREJEA NA MOTO MPYA SIMBA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Dakika 221 za CAG bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, jana alihojiwa kwa saa 3:41 (dakika 221) na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kuhojiwa kwa Prof. Assad kumetokana na wito wa Bunge baada ya Spika Job Ndugai kutoa amri kuwa bosi huyo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) afike mbele ya kamati kujieleza kwa madai kuwa amelidhalilisha Bunge kwa kauli yake kwamba anafikiri chombo hicho cha kutunga sheria ni dhaifu.

CAG Assad aliwasili kwenye viwanja vya Bunge saa 4:47 asubuhi akiwa katika gari jeupe lenye namba za usajili STL 6249 na kupitia katika geti linalotumiwa na wafanyakazi na Waziri Mkuu, na alikaguliwa kwa mashine kama watu wengine wa kawaida.

Katika ukaguzi huo, CAG Assad alivua koti, miwani, saa, viatu na kulazimika kupita kwenye mashine akiwa amevaa malapa (ndala) na baada ya ukaguzi, alivaa viatu vyake na kitambulisho cha wageni, tofauti na ilivyozoeleka kupatiwa kitambulisho cha wageni maalum (VIP).

Baada ya kuingia akiwa amebeba begi dogo jeupe, huku ulinzi ukiwa umeimarishwa kwenye viwanja vya Bunge, CAG Assad, alipokewa na askari kanzu wa Bunge na kufuatana naye hadi lango la kuingilia jengo la utawala ambako aliketi katika viti vya mapokezi kusubiri kupewa maelekezo.

Baada ya kuketi, Katibu wa Spika, Saidi Yakubu, alifika kumsalimia na kumpatia kitabu cha kusaini na baada ya kusaini, aliketi kwa muda akisubiri kuitwa kuingia ukumbini.

Wakati akisubiri kuitwa kuingia kwenye mahojiano, CAG Assad alitumia muda huo kusoma nyaraka mbalimbali alizokuwa amezibeba kwenye begi lake.

Akiwa ameketi akipitia nyaraka hizo, alipita Mbunge wa Kawe (Chadema), Halima Mdee, ambaye alisalimiana naye na kuingia jengo la utawala.

Mdee pia anatakiwa kufika mbele ya kamati hiyo kuhojiwa leo kutokana na kuunga mkono kauli ya CAG Assad kwamba Bunge ni dhaifu.

Prof. Assad aliitwa kuingia kwenye Ukumbi wa Spika saa 5.04 asubuhi na saa 5:06 asubuhi aliingia rasmi ndani ya ukumbi kwa ajili ya mahojiano.

Alipofika katika ukumbi wa mahojiano, Prof. Assad aliwasalimia wajumbe 17 wa kamati hiyo walioongozwa na Mwenyekiti Emmanuel Mwakasaka, kisha aliketi kuwasha kompyuta mpakato aliyokwenda nayo ukumbini humo.

Mwenyekiti wa kamati alimkaribisha Prof. Assad mbele ya kamati na kuwaomba waandishi wa habari watoke ukumbini kwa kuwa wameshashuhudia.

"Shahidi ameshafika mbele ya kamati, Prof. Assad karibu sana, tunawaomba waandishi mtupishe, maadam ameshafika mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, tunashukuru sana," alisema Mwakasaka ambaye pia ni Mbunge

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli, akifurahia jambo na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, baada ya kutoka kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mpina anusa harufu ya ufisadi chanjo

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameibua ufisadi wa kutisha katika biashara ya chanjo za mifugo na kumwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kuandaa haraka mwongozo utakaosimamia mfumo mzima wa uzalishaji, uagizaji, usambazaji na uchanjaji wa mifugo.

Aidha, mwongozo huo unatakiwa kuweka bei elekezi itakayowezesha wafugaji kupata chanjo kwa gharama nafuu.

Mpina amesema kwa miaka mingi wafugaji wamefanyiwa dhuluma kubwa kwa kuuziwa chanjo zaidi ya mara tano ya bei halisi licha ya baadhi ya chanjo hizo kuzalishwa na Taasisi ya Chanjo za Mifugo Kibaha (TVI), ambayo ni taasisi ya serikali iliyopewa jukumu la kurahisisha upatikanaji wa chanjo na kwa gharama nafuu.

Waziri Mpina amesema taifa limefikia hapo kutokana na kukosekana usimamizi madhubuti wa utoaji chanjo nchini hali iliyochangia kuwakatisha tamaa wananchi kuhudumia mifugo yao na kusababisha mingi kufa kwa kukosa chanjo, ambapo amesisitiza kuwa serikali haitakubali dhuluma hiyo iendelee.

Akizungumza baada ya kutembelea TVI na Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Mpina, alielezea kusikitishwa kwake na usimamizi dhaifu wa mfumo wa ununuzi, usambazaji na uchanjaji wa mifugo nchini na kutaka hatua za haraka zichukuliwe ili kuondoa dosari hizo.

Mpina alisema TVI inazalisha na kuuza chupa ya chanjo ya kimeta kwa Sh. 20,000 yenye uwezo wa kuchanja ng'ombe 100, ambapo kila ng'ombe mmoja hutakiwa kugharamia Sh. 200, lakini katika hali isiyokuwa ya kawaida halmashauri, maofisa mifugo na wafanyabiashara wengine wanachanja kwa Sh. 5,000 kwa ng'ombe mmoja sawa na gharama ya Sh. 1, 000,000 kwa chupa, jambo ambalo ni dhuluma na wizi mkubwa kwa wafugaji.

"Chanjo ya mdondo TVI mnauza kwa Shilingi 22, lakini wao wanaokwenda kuchanja wanawatoza wananchi Shilingi 100 kwa kuku mmoja, wananchi wengi wamevunjwa moyo kuhudumia mifugo yao kutokana na utaratibu uliopo haueleweki na hauna msimamizi," alisema.

Mpina alisema Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo ndiye mwenye mamlaka kwa mujibu wa sheria wa kusimamia huduma za mifugo kote nchini, hivyo akakumbusha kuwa ugatuaji wa madaraka (D By D) haukugatua sera na sheria bali

INAENDELEA UK.8

## Matukio ya mauaji ya ulevi yapungua

**Na Gwamaka Alipipi**

JESHI la Polisi limesema matukio ya mauaji yatokanayo na ulevi nchini yamepungua kutoka makosa 129 yaliyoripotiwa mwaka 2017 hadi makosa 118 mwaka jana, ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 8.8.

Pia, matukio ya kupotea ama kuibiwa kwa watoto yamepungua kutoka matukio 134 yaliyoripotiwa mwaka 2017 hadi makosa 116 yaliyotokea mwaka jana, ikiwa ni upungufu wa asilimia 13.4.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Ahmed Msangi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali.

"Takwimu zinaonyesha kuwa matukio ya mauaji yanayotokana na ulevi yamepungua. Kwa kipindi cha Januari hadi Desemba matukio hayo yamepungua, ambapo kwa mwaka 2018 yalikuwa matukio 118, ukilinganisha na mwaka 2017 yaliripotiwa matukio 129, ikiwa ni upungufu wa mkosa 11 sawa na asilimia 8.8," alisema Msangi.

Msangi alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa watumiaji wa kilevi kunywa kwa kiasi na kujiepusha na matukio ya ugomvi pindi wanapokuwa wamelewa.

Kuhusu matukio ya kupotea kwa watoto, Msangi alisema mwaka 2017 kuliibuka vitendo vya kuibiwa kwa watoto ama kupotea hali iliyosababisha hofu kwa jamii hususani kwa wazazi na walezi.

"Kuhusu matukio ya kupotea au kuibiwa kwa watoto nayo yamepungua, kwa mwaka 2017 matukio yaliyoripotiwa yalikuwa

INAENDELEA UK.8

# Adaiwa kuua mdogo wake kisa mgao kishika uchumba

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

LWITIKO Mwama Mwamaloba (25), mkazi wa Kijiji cha Mwaigoga Kata ya Muungano wilayani Kyela mkoani Mbeya, anadaiwa kumuua mdogo wake, Mussa Mwamaloba, kwa kumcharanga na mapanga kisha kumpiga na mchi wa kutwangia mpunga baada ya kudai mgao wa pesa za kujitambulisha baada ya dada yao kuchumbiwa.

Akizungumza jana katika eneo la tukio, jirani wa familia hiyo, Danken Mwakapemba, alidai kuwa sababu za kumfanyia kitendo hicho ni mdogo wake kumdai mtuhumiwa mgao wa pesa ambazo shemeji yao alizitoa kwa ajili ya kishika uchumba cha dada yao.

Alisema siku mbili kabla, watu kadhaa walifika kwenye familia hiyo kujitambulisha wakihitaji kuoa dada wa familia hiyo, ambao walitoa Shilingi 150,000, ambapo kaka yao (Lwitiko) alizipokea kisha kutoka.

Alisema aliporejea nyumbani usiku mdogo wake alidai apatiwe mgao wa fedha hizo, lakini kaka hakujibu chochote, asubuhi (Mussa) aliendelea kumdai, lakini mtuhumiwa aliondoka tena nyumbani na kurejea tena majira ya saa 6 mchana na kuanza kupiga mdogo wake.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mwaigoga, Awad Mikidadi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba alikuwa shambani na kukuta mwili wa marehemu umepelekwa kuhifadhiwa katika hospitali ya wilaya na alipouliza, aliambiwa ameuawa kwa kucharangwa mapanga na kaka yake, hivyo kutoa taarifa ofisi ya kata.

Ofisa Mtendaji wa kata ya Muungano, Ally Joel, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kudai kuwa mtuhumiwa alifanya mauaji hayo kwa kumcharanga na mapanga mdogo wake kisha kumpiga na mchi wa kutwangia mpunga na kwamba tukio hilo limezua taharuki kubwa kwa wakazi wa eneo hilo.

Alisema taarifa za awali zinadai kuwa mauaji hayo yalitokana na mtuhumiwa kudaiwa na mdogo wake fedha za mgao zilizotolewa kwa ajili ya kishika uchumba cha dada yao.

Alisema baada ya uchunguzi wa kitabibu na kipolisi kukamilika, Jeshi la Polisi liliruhusu mwili wa marehemu kuchukuliwa kwa ajili ya maziko yanayotarajiwa kufanyika kwenye makaburi ya familia hiyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, alisema jeshi lake limemkamata mtuhumiwa huyo na taratibu za kipolisi zinaendelea na atafikishwa mahakamani baada ya kukamilika kwa uchunguzi.



Mchuuzi wa magimbi, akiyatoa matope kabla ya kuwauzia wateja wake, katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waliong'atwa na nyoka wapona kwa tiba asili

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU 109 wakiwamo wanaume, wanawake na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, waliokuwa wameshambuliwa kwa kung'atwa na nyoka, mkoani Lindi, wamenusurika kifo baada ya kupatiwa tiba mbadala na mtaalamu wa nyoka.

Mtaalamu huyo, Japokuwa Masawila, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wake na changamoto anazokumbana nazo katika mkutano wa waganga wa tiba asili wa mkoa huo, uliofanyika mjini Lindi.

Akiwasilisha maelezo yake, Masawila alisema majeruhi hao wa nyoka wakiwamo wanaume (59) na wanawake (50), walishambuliwa na kupatiwa matibabu kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2017, huku watoto wenye umri chini ya miaka 18 wakiongoza kwa idadi.

"Watoto hung'atwa sana na nyoka kutokana na kupenda kucheza vichakani kufuata vitoro, wakati wakubwa wanapokuwa mashambani na kidogo majumbani," alisema.

Alifafanua kwa kueleza mwaka 2015 alitibu majeruhi 29, mwaka 2016 (37) na 2017 (43) na kufanya idadi ya aliowatibu kuwa 109.

Alisema miongoni mwa majeruhi wa nyoka aliowahi kutibia ni pamoja na wale waliokuwa wameshindikana kutibiwa na dawa za kizungu (hospitalini), kwa kuwa wanaposhindwa humwita na kuwatibia kupitia dawa zinazotokana na miti shamba (tiba asili). Pia alisema tangu aanze kazi ya kutibu watu wanaoshambuliwa na nyoka, hakuna mgonjwa aliyepoteza maisha akiwa chini yake.

Masawila alisema mara nyingi amekuwa akikumbana na changamoto mbalimbali, ikiwamo kukosa ushirikiano na baadhi ya watendaji wa serikali ngazi za vijiji, mitaa na kata pale anapohitaji kuwapatia wananchi elimu na jinsi ya kujikinga na kujitibu wanapong'atwa na nyoka.

"Nimeshawahi kukamatwa ninapojaribu kutoa elimu kwa jamii na ninapoomba kibali cha kufanya hivyo mpaka niwape kitu kidogo," alisema.

Alisema hivi karibuni aliitwa kwenda kiwanda cha kubangua korosho cha Bucco, ambacho kwa sasa kipo chini ya uangalizi wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), kwenda kumwondoa nyoka aina ya chatu aliyekuwa amejificha kwenye magunia yaliyowekwa zao hilo na kuhifadhiwa kiwandani hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliyekuwa akimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, alimpongeza mtaalamu huyo kwa kazi anayoifanya ya kuokoa maisha ya wananchi wenzake, huku akiwasisitiza watendaji kumpa ushirikiano wa karibu kwa manufaa ya Watanzania wenzake.

Ndemanga alisema hakuna sababu kwa watu wa aina hiyo kuachwa bure na kuusisitiza uongozi wa idara ya afya kuendelea kumshika mkono katika jitihada zake za kuokoa maisha ya Watanzania wenzake.

# Z'bar yasamehewa deni bil. 23/- Tanesco

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia utozwaji wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye umeme unaouzwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), sambamba na kufuta malimbikizo ya deni la kodi ya VAT lililofikia Shilingi bilioni 22.9 kwa Tanesco kwenye umeme uliouzwa Zeco.

Uamuzi huo ulifanywa na Baraza la Mawaziri jana, Ikulu Jijini Dar es Salaam, katika kikao kilichoongozwa na Rais John Magufuli na kuhudhuriwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi na mawaziri.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Rais Magufuli, alisema baada ya kufanya uamuzi huo Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, atawasilisha marekebisho madogo ya sheria ya VAT, sura ya 148 kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2019, ili umeme unaouzwa Tanzania Zanzibar utozwe VAT kwa kiwango cha asilimia sifuri.

"Kwa hiyo madeni yatakayokuwa yanadaiwa kwa Zanzibar ni yale madeni ya kulipia umeme, umeme wametumia kiasi fulani wanalipa kama wanavyolipa wa maeneo mengine kwa mfano wanavyolipa Dar es Salaam, suala la kutoza VAT sasa halipo, na katika hilo kwa sababu kulikuwa na deni ambalo lilikuwa limefika Shilingi bilioni 22.9, sisi Baraza la Mawaziri tutapeleka mapendekezo Bungeni kwamba lisamehewe kwa sababu lipo ndani ya bajeti ya mwaka huu wa 2018/19, kwa hivyo litapunguza mapato yatakayotakiwa kukusanywa na serikali," alisema Rais Magufuli.

Kwa upande wake, Dk. Shein alisema pamoja na kuridhia utozaji wa VAT kwa kiwango cha asilimia sifuri, Baraza la Mawaziri pia limekubaliana kuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ataitisha vikao vya kuzungumzia masuala ya Muungano kila mara kunapokuwa na hoja ya masuala ya Muungano ili kujadili na kutoa uamuzi.

"Tungependa sana mambo haya yafanyike vizuri kwa sababu pande mbili za Muungano zinatuhusu sote, hili ni muhimu kwa sababu mambo yakikusanyika mengi wananchi wanahisi hatusaidii jitihada zao, kwa hivyo tumeridhia kuwa masuala ya Muungano ambayo yapo chini ya Makamu wa Rais, wakae pamoja wayajadili ili yapate uamuzi wa pande zote mbili," alisema Dk. Shein.

**Wakati huo huo**, Rais Magufuli alimwapisha Anjellah Kairuki kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji).

Kairuki aliapishwa kabla ya kuanza kwa kikao cha Baraza la Mawaziri, kufuatia mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Rais Magufuli Januari 8, mwaka huu, ambapo Kairuki aliyekuwa Waziri wa Madini, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji).

# Wataka tozo uvunaji misitu zipunguzwe

**Na Lusungu Helela,** IRINGA

KAMATI ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, imeishauri serikali kuona namna ya kupunguza utitiri wa tozo za ushuru kwa wavunaji wa misitu, hali inayomkwamisha mfanyabiashara kushindwa kumudu gharama za kujiendesha kibiashara.

Ushauri huo ulitolewa baada ya kikao cha wadau wa misitu kulalamikia juu ya uwapo wa utitiri wa tozo za ushuru zaidi ya sita mbali na ile inayotozwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Wadau hao wakiwamo wavunaji wadogo, wa kati pamoja na wavunaji wakubwa walisema hayo kwenye kikao kati ya kamati kilichofanyika Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa.

Mwenyekiti wa wavunaji wadogo, Bazir Tweve, alisema licha ya kuwa hana tatizo na tozo zinazotozwa na TFS, ila kumekuwa na ongezeko kubwa la kodi ya malighafi zinazoibuliwa na halmashauri pamoja na uongozi wa mkoa, hali inayosababisha kuporomoka kwa soko na kusababisha wafanyabiashara wengi kuhamisha mitaji yao kufanya biashara nyingine.

"Wavunaji wamekuwa waoga kutokana na mabadiliko hasi ya tozo za kujirudia za viwango vya juu, ndoto ya viwanda inapotea kabisa kwa tafsiri nyingine tunaita kodi kandamizi," alisema.

Akizungumzia changamoto zinazowakabili, alisema utitiri wa kodi unaleta athari ndani ya Mkoa wa Iringa na Tanzania kwa ujumla, pia unaathiri mpaka yule mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi.

Pia, wadau hao wameomba sheria inayozuia kusafirisha mazao ya misitu usiku iangaliwe upya na ili kuendana na kaulimbiu ya Tanzania ya viwanda.

Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo, alisema kodi zimekuwa kero kwa wadau hao, hivyo zikusanywe sehemu moja ili kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara hao.

Aidha, Msigwa alisema Mkoa wa Iringa ndio unaoongoza katika kuzalisha mazao ya misitu, lakini inashangaza kuona maisha ya wananchi yakiwa duni.

"Tunataka kila mwananchi anayezunguka maeneo ya maliasili awe mfaidika wa kwanza wa mazao haya," alisema.

Akijibu hoja za wananchi kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Dos Santos Silayo, ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa TFS, alisema maoni yote yaliyotolewa yatafanyiwa kazi likiwamo suala la tozo ambazo zimekuwa kero kubwa kwao.

Naye, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alizionya halmashauri nchini kuacha kuanzisha tozo za mazao ya misiti ambazo zinajichanganya na tozo zilizopo kisheria zinazotozwa na TFS

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Ardhi, Nape Nnauye, akizungumza baada ya kupokea maoni kutoka kwa wadau hao, alisema Kamati ya Bunge baada ya kupata taarifa, itaibana serikali ili iweze kufanyia kazi kwa kuwa malalamiko mengi yanajirudia rudia.



Wakazi wakionekana kukaidi kibao kinachozuia kuegesha magari madogo, katika eneo la kituo cha mabasi cha Machinga Complex, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## TEC yaomba msaada ukarabati seminari iliyoteketea

**Na Beatrice Moses**

BARAZA la Maaskofu Tanzania (TEC), limewaangukia waumini wenye mapenzi mema likiwaomba wajitokeze kutoa michango mbalimbali, ili kukarabati sehemu ya jengo la Seminari Kuu ya Mt. Kaloli Lwanga Segerea jijini hapa, iliyoteketea kwa moto.

Makamu wa Rais TEC, Mhashamu Flavian Kassala, aliwatangazia waumini na watu wote wenye mapenzi mema kuwa seminari hiyo iliyoko Jimbo Kuu la Dar es Salaam, ilipatwa na ajali ya moto ambao umesababisha hasara ambayo bado haijajulikana.

Askofu Kassala akizungumza na waumini juzi, alibainisha kuwa jengo hilo lililoteketea ni la makazi ya mapadri ambao ni walezi wa vijana katika seminari hiyo. Alisema katika ajali hiyo mapadri walinusurika wakati vyumba vyote 14 vya makazi yao vimeteketea pamoja na mali zao zote yakiwamo mavazi, malazi pamoja na nyenzo za kufundishia kama vile vitabu na kompyuta.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Charles Kitima, alisema kuwa wamelazimika kuchukua hatua ya kuomba michango kwa waumini ili kuwawezesha jengo hilo kukarabatiwa mapema. Alisema TEC wamefanya juhudi za awali za kuwatafutia hifadhi za muda kwenye hosteli za wanafunzi pamoja na kuwasaidia mapadri wapate mahitaji yao muhimu ya kibinadamu.

"Michango tunayohitaji ni vitu mbalimbali ambavyo waumini wataguswa ikiwamo vifaa vya ujenzi, fedha, lakini pia tunatamani mapadri wetu wapate tena vifaa vyao muhimu ikiwamo kompyuta na vitabu," alisema Dk. Kitima.

Baraza hilo limewaomba waumini kutuma michango yao kwenye akaunti ya Mkombozi Bank TEC Maafa Segerea Seminari namba 001 115 109 900 01.

Awali Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala, Elisa Mugisha, alisema kuwa wanaendelea kuchunguza chanzo cha moto huo.

# Balozi Seif aitaka OUT kuongeza udahili

**Na Futuna Seleman,** KIBAHA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, amekitaka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kuongeza kiwango cha udahili kwa wananchi katika elimu ya juu kwa haraka na kasi itakayowezesha kufikia lengo la nchi kuwa ya uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2025.

Balozi Seif alitoa ushauri huo katika mahafali ya 35 ya chuo hicho, makao makuu Bungo Kibaha mkoani Pwani mwishoni mwa wiki.

"Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, kiwango kidogo cha udahili katika elimu ya juu ni sifa ya msingi wa uchumi wa chini na wa kimaskini," alisema na kuongeza:

"Uchumi wa kati na wa viwanda hauwezi kufikiwa au kuwa endelevu pasipokuwa na kiwango cha udahili katika elimu ya juu angalau asilimia 23."

Alisema kiwango cha Tanzania kama ilivyo kwa Burundi na Madagascar ni asilimia 4, ambapo kwa upande wa Tanzania sababu ya kuwa na kiwango hicho kidogo cha udahili kimebainishwa kwenye sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014.

Akisema kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaona umuhimu kwa maendeleo ya chuo hicho na ndio maana inaona ipo haja kwa taasisi hiyo kuingia Zanzibar na ipo tayari kuwapatia kiwanja kujenga kituo cha pili kwa ukubwa.

"Tunaamini kuwapo kwenu Zanzibar kichwa na miguu kutasaidia sana kudumisha muungano wetu," alisema Balozi Seif.

Alisema vyuo vikuu vingi mashuhuri duniani vinachangiwa kwa kiasi kikubwa na wahitimu ambao wengine kimaisha huwanyookea na kuwa matajiri wakubwa.

"Ombi langu kwa wahitimu walioptita na wa siku ya leo na wengine watakaokuja popote mtakapokuwa kuchangia maendeleo ya chuo kwa njia mbalimbali. Wengi wetu hapa kwenye meza kuu tumesoma kwenye vyuo vya hapa nchini, lakini sifikirii kama vyuo vyenyewe vina habari na sisi," alisema.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Elias Bisanda, alisema chuo hicho kimepata mafanikio makubwa ikiwamo matumizi ya Tehama katika kuhakikisha usalama wa mitihani na ubora wa elimu umekuwa ukiongezeka ikiwamo kupeleka mitihani visiwani kama Unguja na Pemba, Ukerewe na Mafia bila kutumia ndege wala boti badala yake wanatumia Tehama.

Aliainisha changamoto mbalimbali zinazokikabili chuo hicho ikiwa ni pamoja na madai yaliyosalia ya kiinua mgongo kwa wastaafu, ambapo kinaidai serikali zaidi ya Shilingi bilioni 8 kwa stahili mbalimbali za wafanyakazi hasa wastaafu kufuatia serikali kusimamisha ajira kwa wanataaluma wenye umri wa miaka 65.

"Sisi kama waajiri wa serikali tujipange kuhakikisha tunawalipa wastaafu ukizingatiwa kwa sasa hawana ajira," alisema Prof. Bisanda.

## Mtumishi Wizara ya Mifugo na Uvuvi apotea

**Na Mwandishi Wetu**

MTUMISHI wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambaye ni Meneja wa shamba la kuzalisha mitamba la Sao Hill, wilayani Mafinga, mkoani Iringa, Nickson Keiya (pichani), amepotea na hajulikani alipo.



Taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Mifugo na Uvuvi jana, ilisema kuwa Keiya alipotea tangu Januari 15, mwaka huu, akiwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 214 BZZ aina ya King Lion, yenye rangi nyekundu, maeneo ya Ilundi/misitu ya Sao Hill.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Keiya mara ya mwisho alikuwa amevaa suruali ya kaki na shati lenye rangi ya udongo yenye michirizi myeupe na raba za rangi ya kaki yenye soli nyeupe. Aidha, ilisema taarifa za kupotea kwake zimeripotiwa Kituo cha Polisi Mafinga, Iringa.

Taarifa hiyo iliomba mtu yeyote atakayemwona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0713 757157** na **0762 952766.**

## Masauni apokea vifaa vya mil. 68/- kudhibiti uhamiaji haramu

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, amepokea vifaa vya kudhibiti uhamiaji haramu katika mipaka mbalimbali nchini vyenye thamani ya Dola za Marekani 30,000 (sawa na Sh. mil. 68.7)

Akizungumza na waandishi wa habari jana, wakati wa kupokea vifaa hivyo, Masauni alisema vifaa hivyo vitasaidia kwa kiwango kikubwa kudhibiti mipakani ambako hutumika kama mwanya wa kuingilia wahamiaji haramu na kwamba lengo ni kuhakikisha wanakomesha kabisa wahamiaji haramu ikiwamo vitendo vyote vya uhalifu katika mipaka ya nchi.

"Vifaa hivi ni kama sehemu ya kuongeza nguvu katika mipaka yetu ya nchi katika udhibiti wa wahamiaji haramu na vitendo vyote vya uhalifu katika mipaka yetu yote nchini," alisema Masauni na kuongeza:

"Tunataka kuhakikisha tunakomesha vitendo vyote katika mipaka yote, wahamiaji haramu, bidhaa haramu zinazopita katika mipaka yetu na mambo mengine yote."

Kwa upande wake Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamiaji (IOM), Dk. Qasim Sufi, alisema wametoa vifaa hivyo kama mchango wao katika kupambana na vitendo vya uhamiaji haramu Tanzania.

# Msako wanasa wahamiaji haramu kibao D'Salaam

**Na Salome Kitomari**

IDARA ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, imeanza kusaka wahamiaji haramu kwenye makazi na sehemu za kazi, ikiwamo kuwachukuliwa hatua za kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Ofisa Uhamiaji Mkoa, Kamishna Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiani, Novaita Mroso, alisema operesheni maalum imefanyika na inaendelea.

Alisema wameamua kuwasaka wahamiaji haramu kwenye mitaa, ili kuweza kuwadhibiti zaidi.

"Tukishindwa kukupata eneo la kazi tutakufuata nyumbani, kwa utaratibu tuliojiwekea Dar es Salaam, siyo sehemu salama kuwa maficho kwa wahamiaji haramu. Yeyote anayeajiri raia wa kigeni ahakikishe ana vibali vyote vya kuishi nchini," alisema.

Alisema ilianza Januari 17 mwaka huu, na hadi jana ilikuwa na siku tano na jumla ya wahamiaji 81, ambao wanatuhumiwa kwa makosa mbalimbali walitiwa mbaroni.

"Kati yao tumebaini 35 wanatoka nchini Burundi, waliobaki wanatoka Somalia na Congo, wengine 46 wanaendelea kuchunguzwa na baada ya kukamilika tutabaini uhalali wao wa kuwapo nchini," alisema.

Mroso waliobainika kuwa ni wahamiaji haramu watachukuliwa hatua za kuwafikisha mahakamani na kuwafukuza nchini.

"Operesheni maalum ni sehemu ya jukumu letu la udhibiti wa wahamiaji haramu. Pia tumekuwa tukifanya uhakiki wa taarifa za wageni waliopo Mkoa wa Dar es Salaam ambao wamejiajiri au kuajiriwa," alisema.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, jumla ya raia wa kigeni 16,102, na kwamba wanawatambua na kuwaorodhesha raia wa Malawi na wahamiaji walowezi katika wilaya zote mkoani humo na walioandikishwa ni 1,770.

"Tumejiandaa kama mkoa na tumeshachukua hatua kushirikiana na watendaji wa ndazi za mitaa, tumeugawanya mkoa katika wilaya, tarafa, kata na mitaa na tumeshaibaini mitaa 553 na kukutana na viongozi wao na kubaini shughuli zinazoendela kwneye mitaa husika," alisema.

Kuhusu kusafirishwa wahamiaji kupitia Tanzania, Mroso alisema faini ni zaidi ya Sh. milioni 20 au kifungo kisichopungua miaka 20 na kwamba mahakama imepewa mamlaka ya kutaifisha mali au nyumba zilizotumika kuwasafirisha au kuwahifadhi wahamiaji haramu.



Mganga wa tiba asilia 'akiuchapa' usingizi wakati akisubiri wateja wa dawa zake, katika eneo la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mkosamali afunguka, awashangaa wanasiasa wasiokuwa na msimamo

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa zamani wa Muhambwe mkoani Kigoma, Felix Mkosamali, amesema anajua ni kwa nini yuko upinzani, hivyo hawezi kutoka huko kama ambavyo hivi karibuni baadhi ya wanasiasa walikimbilia chama tawala.

Alisema anaamini katika upinzani imara, anaamini katika nchi kuwa na katiba mpya na anaamini katika haki za binadamu.

Mwanasiasa huyo ambaye pia ni Mkuu wa Idara ya Sheria wa Chama cha NCCR-Mageuzi na pia wakili wa kujitegemea, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kuelezea msimamo wake.

"Kwanza kabisa ninajiamini na pia ninawapenda wanasiasa wasioyumbayumba, wasiotanguliza njaa na kufikiri kwa kutumia tumbo," alisema Mkosamali.

Alisema kwa sasa siasa za Tanzania zimeingiliwa na watu wanaojipendekeza ili wapate maslahi yao binafsi badala ya kutumikia umma na kwamba watu wa aina hiyo hawafai.

"Kwenye harakati zilizoitwa kuunga mkono, kuna watu waliwahi kunizushia kuwa eti nimehama katika chama changu, huu ulikuwa ni uongo wa mchana kweupe, lakini msimamo wangu ni kwamba ninaamini katika upinzani imara, ninaamini katika nchi kuwa na katiba mpya na ninaamini katika haki za binadamu," alisema.

Alisema kuwa tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 amekuwa kimya, akifuatilia hali halisi ya siasa na kubaini mambo mengi ya ajabu yanayoendelea kufanywa na baadhi ya wanasiasa.

"Unajua wakati mwingine mtu anaweza kuwa kimya ili kujifunza mambo, ila nimeona mengi ya ajabu na hasa haya ya kuunga mkono, ambayo kwa kweli yanaonyesha kuwa tuna wanasiasa wa kuyumbayumba," alidai.

Alisema wanasiasa wa aina hiyo wanamkera, kwa madai kwamba wanafanya maamuzi magumu kwa hoja nyepesi ambazo hata mtu wa kawaida anazibaini.

"Mimi ninaamini kwamba upinzani nchini bado una nguvu kubwa, ndio maana unabanwa na vyombo vya dola, lakini pia kuna tatizo la kushindwa kujenga umoja na pia kuwapo kwa ubinafsi wa baadhi ya watu," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mzaha usipewe nafasi usimamizi wa kilimo

**MAMBO** ya ovyo yanayofanywa na watendaji kadhaa wa serikali, yanaendelea kutajwa kuwa yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kukwamisha jitihada za serikali za kuboresha sekta ya kilimo.

Mambo hayo yakiwamo urasimu, uzembe na kutokuwajibisha limekuwa jambo la kawaida kutajwa kila uchao kama kikwazo cha kufufua na kuboresha sekta muhimu ya kilimo nchini.

Itakumbukwa kuwa serikali ya awamu ya tano imekuwa na kasi kubwa ya kuboresha sekta ya kilimo kwa lengo la kuhakikisha kwamba kuboresha kwake ndiyo itakuwa njia ya kufungulia kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mkakati wa kuuboresha sekta ya kilimo umekuwa ukienda sambamba na mkakati wa kuboresha baadhi ya mazao ya biashara ambayo yamepewa jina la mazao ya kimkakati, ambayo kwa kuanzia ni kahawa, chai, tumbaku, korosho na pamba.

Mengine ambayo hata hivyo hayajaingizwa katika awamu ya kwanza ni michikichi, mkonge na mazao yanayotoa mafuta kama alizeti, ufuta na mengine. Hizi zote ni jitikada za maandalizi ya kuwa na malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda vyetu ambavyo ujenzi wake umeshaanza.

Utekelezaji wa mkakati huo haunabudi kwenda sambamba na uwapo wa wasimamizi ambao ni watendaji au kwa lugha iliyozoeleka 'watumishi' waadilifu, waaminifu, wachapakazi na wenye weledi.

Bila kuwa na watumishi wenye sifa hizi ndiko kunakoweza kuwezesha utekelezaji mzuri na wenye tija katika kuboresha kilimo chetu na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Tunayasema haya kutokana na alichokibaini na kukemea Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, katika sekta ya kilimo kwamba kutowajibika, uzembe na urasimu kwa baadhi ya watendaji katika sekta ya kilimo kusababisha ucheleweshaji wa pembejeo za kilimo.

Kutokana na hali hiyo Waziri Hasunga akiwa ziarani mkoani Tabora mwishoni mwa wiki kukagua maendeleo ya kilimo, alikemea vikali vitendo hivyo na kusema vinakwamisha dhamira ya serikali ya kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo.

Waziri Hasunga, alikemea tabia ya watendaji kuendeleza urasimu katika upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwamba asingependa kusikia hadithi za ucheleweshaji wa mbolea zikiendelea, huku wakulima wakiendelea kuathirika na hali hiyo.

Kwamba ni lazima waache kufanya kazi kwa mazoea badala yake wawasaidie wakulima wafikie malengo ya kuwa na kilimo chenye tija na uhakika.

Kama tumedhamiria kukiboresha kilimo, kila mmoja anatakiwa kubadilika kuanzia kwa wakulima wenyewe, wataalamu, watendaji katika sekta ya kilimo na watunga sera kwa kuacha mazoea na kuchapa kazi na kuwa wabunifu.

Mzaha hauwezi kutusaidia kama taifa kufikia tunakotaka kwenda, hivyo usipewe nafasi katika maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Kama kuna watendaji wataendelea kufanya kazi kwa mazoea, urasimu, uzembe na kutokuwajibika, wasiendekezwe bali waondolewe mara moja kwa kuwa vitendo hivyo vina athari kubwa kama alivyosema Waziri Hasunga kuwa baadhi yao wanasababisha pembejeo zichelewe kuwafikia wakulima.

Bila shaka watendaji katika sekta ya kilimo watakuwa wamesikia angalizo la Waziri Hasunga kuhusiana na utendaji wao unavyokwamisha makakati wa kukiboresha kilimo, ili kichochee maendeleo ya uchumi wa taifa letu. Suala la msingi ni kurejea katika mstari, vinginevyo wasipewe nafasi kuendelea kuwa ofisini.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**RIZIKI NI MAFUNGU**

**WATU WENGI WANAAMINI KUWA RIZIKI INATOKA KWA MUNGU NA KILA MMOJA WETU ANA FUNGU LAKE. PAMOJA NA KUWA HIVYO, TUSIKAE DEBWERE. KUFANYA KAZI TENA KAZI HALALI NI SEHEMU YA FUNGU HILO. BILA KAZI HAKI YA KULA HAKUNA. NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi wana mchango kuinua ubora wa elimu ya watoto wao

Na Raphael kibiriti

**YUMKINI** suala la elimu linapojitokeza, kila mtu anakubali lina umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu.

Ndiyo maana katika dunia ya sasa elimu ni moja ya sekta zinazochukua sehemu kubwa ya bajeti za nchi zilizo nyingi.

Ukitalii vyanzo mbalimbali, utakuta nchi zilizowekeza zaidi kwenye huduma za jamii, ikiwamo elimu pamoja na sababu zingine ndizo ambazo zimefanikiwa kustawisha maisha ya wananchi wake.

Ndizo nchi ambazo watu wake wameelimika kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwa na uwanda mpana wa kuchanganua mambo, kitu ambacho ni muhimu kwa maendeleo ya mtu, jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa takwimu za Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) za mwaka 2016, kuna nchi 11 zilizo nafasi ya juu katika eneo hili la uwekezaji mkubwa kwenye huduma za jamii na hivyo elimu kwa maana ya safu hii.

Unapoiangalia orodha hiyo, unakubali kwamba kumbe kuna umuhimu mkubwa wa kuwekeza katika elimu.

Hii ni kwa sababu orodha inajumuisha baadhi ya mataifa ambayo watu wake wako vizuri kimaisha.

Pamoja na orodha hiyo kuwa na nchi kutoka mabara mengine isipokuwa Afrika, Ulaya inaongoza huku nchi za Skandinavia zikiitawala orodha hiyo.

Nchi zilizo kwenye orodha hiyo ni pamoja na Singapore, Finland, Netherlands, Uswizi, Ubelgiji na Denmark.

Nyingine ni Norway, Marekani, Australia New Zealand na Iceland.

Kama Muungwana alivyoainisha mwanzo, sababu kubwa ya mafanikio ya nchi hizo kwenye sekta ya elimu ni uwekezaji mkubwa kwenye huduma za jamii, ikiwamo elimu. Tanzania vilevile haiko nyuma katika suala zima la uwekezaji katika huduma za jamii, ikiwamo sekta ya elimu.

Kwa mfano katika Bajeti ya mwaka 2016/17, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, iliomba kuidhinishiwa zaidi ya Shilingi triolini1.3 kati ya Sh. trilioni 29 za bajeti nzima, kiwango ambacho kimsingi kilikuwa ni cha kuridhisha.

Hata hivyo, suala la uwekezaji wa kibajeti kama inavyofanyika kila mwaka ni jukumu la moja kwa moja la serikali.

Na hilo halina ubishi kwa sababu ni jukumu la kikatiba.

Lakini katika kuhakikisha kwamba watoto wa Kitanzania wanaelimika kwa kupata elimu bora ambayo itawaweka katika nafasi ya kuchanganua mambo, wadau vilevile wanaingia katika hili.

Wanaingia katika jukumu la msingi la kumwezesha mtoto wa Kitanzania kuwa na elimu inayomwezesha kuchanganua lililo jema na baya katika mustakabali mzima wa kujiletea maendeleo yake, jamii na taifa kwa ujumla.

Wadau ninaorejea ni pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kama Hakielimu, Twaweza na mengineo, lakini pia na kwa uzito unaostahili wazazi na walezi wa watoto.

Hata hivyo, suala hili la kuhakikisha watoto wanapata elimu bora, ni kama limeachwa na wazazi mikononi mwa serikali na wadau pekee.

Hii ni kwa sababu utaona pale panapotokeo upungufu wa aina yoyote katika sekta hiyo, kama vile kufeli kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika mitihani ya taifa, wazazi huinyooshea mkono serikali.

Lakini hata katika jitihada za kutafuta kiini cha wanafunzi kufeli, bado utaona wazazi hawahawa wakiliacha suala hilo kwa wadau kama Twaweza au Hakielimu ili 'waumize' vichwa, wao wakijiweka pembeni kama vile haliwahusu.

Yaani maadamu wao wanawanunulia watoto wao sare, daftari, vitabu, wanatoa nauli ya kwenda na kurudi shuleni, basi kazi yao imeishia hapo.

Muungwana anaona mtazamo huu wa wazazi na walezi si sahihi.

Wanapaswa pia kushiriki katika kuona kuna ubora wa elimu inayotolewa kwa kuhakikisha watoto wao wanafanya majaribio waliyopewa shuleni, wanawauliza maswali kulingana na ngazi ya elimu yao.

Aidha, wanapaswa kuzitembelea shule ili kujua maendeleo ya watoto wao.

Muungwana anaona kwamba hili likifanyika, Tanzania itakuwa nchi ya watu walioelimika na hivyo kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

# BARUA & MJADALA

## Serikali itusaidie wakazi Dar, kelele zimezidi sana

***Ndugu Mhariri wa Nipashe,***

*NAOMBA unichapishie yafuatayo katika gazeti lako kwa faida ya wananchi.*

*Leo hii katika jiji letu hili la Dar es Salaam kumeshamiri kelele nyingi na hali inaonekana itaendelea hivyo siku hadi siku. Nyingi ya kelele hizi ni kutoka kwenye nyumba za starehe, baa, hoteli pia nyumba za ibada.*

*Na kwa bahati mbaya maeneo haya yameenea takribani katika sehemu zote za jiji letu, yaani kwenye makazi ya watu, hospitalini, katika zahanati, shule zetu na sehemu zingine za aina hii.*

*Aidha, kero zaidi ni kwamba mengi ya majengo haya yanatumia vipaza sauti ambavyo vinasababisha ukosefu wa starehe ya kupumzika kwetu sisi wananchi na mazonge mengine ambayo kwa ujumla wake yanasikitisha.*

*Wakati sasa umefika kwa serikali yetu na hasa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kuchukua hatua za makusudi za kudhibiti kero hiyo inayotutesa kwa hivi sasa.*

*Cha msingi, ni kwamba kelele hizi katika mazingira tunayoishi zinatuathiri kiafya, hivyo ni vyema taratibu, sheria na kanuni zikachukua mkondo wake.*

***Mwananchi-Dar es Salaam***

## Barua yetu ya wazi kwa Mwenyekiti CCM Taifa

***Ndugu Mhariri pole na majukumu ya kikazi,***

*NINAYO heshima kwako kuomba nafasi katika gazeti lako tukufu ili uweze kutuchapishia barua yetu hii ya wazi kwa Mwenyekiti wetu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).*

*Barua hii ya wazi kwa Mwenyekiti wetu Dk. John Magufuli ambaye pia ni Rais wa taifa letu hili inahusu suala la sisi wastaafu kunyang'anywa vibanda vyetu.*

*Kimsingi, sisi ni wazee wastaafu wa serikali na mashirirka ya umma ambao tulijenga vibanda katika eneo la klabu cha CCM, Uwanja wa Fisi kwa gharama zetu wenyewe.*

*Cha kushangaza viongozi wa kata wakatoa taarifa wilayani kwamba hatulipi kodi, kumbe tulikuwa tunalipa halafu viongozi hao hao wanakula kodi tunazolipa.*

*Kupitia kwako Mhariri tunamwomba Mwenyekiti wetu wa chama Taifa aingilie suala hili ili tuweze kurudishiwa vibanda vyetu hivyo.*

*Kwa kweli tunaomba haki itendeke katika suala hili.*

***Wazee wastaafu***
***Kijiji cha Mkamba 'A'***
***Uwanja wa Fisi,***
***S. L. P. Kidatu.***

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# Manispaa Ubungo iimarishe usafi katika Soko la Mabibo

**Na Salome Kitomari**

**MOJA** ya soko chafu, lisilo na miundombinu rafiki, lisilo na mpangilio ni la Mabibo ambalo ni maarufu kama Mahakama ya Ndizi.

Licha ya umuhimu wa soko hilo kwa watumiaji wote na Manispaa ya Ubungo, pengine na wakazi takribani wote wa Jiji la Dar es Salaam, lakini limegeuzwa kuwa 'ng'ombe' anayekamuliwa bila malisho.

Soko hili kwa sasa linauza mazao ya jumla na rejareja baada ya Soko Kuu la Kariakoo kubadilishiwa matumizi yake, ambapo kwa sasa kuna fremu za biashara na wauzaji wa pembejeo, huku wauzaji wa mazao ya shambani wakifanya biashara zao kwenye soko dogo lililo nje la Soko Kuu la Kariakoo.

Hivyo, Mabibo sasa ni soko la jumla na ndiyo maana magari yanayoleta mazao kutoka mikoani hushusha mizigo yao hapo.

Aidha, nao wanunuzi wa rejareja huchukua mizigo ya mazao sokoni hapo kwa ajili ya kwenda kuuza kwenye maeneo mbalimbali kutokana na ukweli kuwa sheria ndogondogo haziruhusu magari makubwa kuingia mjini.

Soko hilo ni chanzo cha mapato ya Halmashauri ya Ubungo na kila siku fedha hukusanywa kutoka kwa wafanyabiashara ambazo pamoja na mambo mengine zinatakiwa kutumika kuboresha usafi wa soko hilo kwa maana ya kuondoa takataka zinazozalishwa kila siku na kuweka miundombinu rafiki.

> **Mwaka jana nilifanya ripoti maalum kwenye masoko ya Jiji la Dar es Salaam, na kubaini kuwa iwapo yangeboreshwa yangeweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato ambacho kingeipatia halmashauri mabilioni ya fedha.**

Kwa nyakati za mvua kama hizi, ukifika sokoni hapo kwa ajili ya manunuzi hali siyo ya kuridhisha na hakuna jitihada zozote za wazi za kuliboresha soko hilo, ili angalau liendane na mahitaji halisi ya wafanyabiashara na wateja.

Kwa sasa maji ya mvua yametuama, kuna tope ambalo wafanyabiashara hulikabili kwa kutandaza majani ya mazao, ili waweze kupita kwa wakati huo, huku eneo la kukusanyia takataka likiwa limejaa kiasi cha kuwa kero.

Unapotaka kufanya manunuzi lazima ukodishe mabuti ambayo yanapatikana hapo na hii imegeuka kuwa biashara ya baadhi ya vijana. La sivyo, basi ununue maji ya kunawa miguu baada ya kumaliza kufanya manunuzi.

Vizimba havina paa wala makinga maji kiasi kwamba maji ya mvua huishia ndani ya soko, na bidhaa nyingine huharibika.

Kwenye eneo la kuegesha magari makubwa yanayoleta mizigo nako kuna madimbwi makubwa makubwa kiasi cha magari kushindwa kukaa vizuri, licha ya kuingiza fedha kwa wingi kila uchao.

Kwa ujumla Soko la Mabibo si jema sana kwa wafanyabiashara na watumiaji, kiasi kwamba inazua maswali kuna kigugumizi gani cha kuboresha soko hilo, ili liweze kuwa na hali njema yenye kuwajali watumiaji wote na kuwa chanzo kizuri cha mapato.

Kama manispaa inafurahia kukusanya fedha bila kuboresha miundombinu, maana yake wanamkamua ng'ombe ambaye hawamlishi kitu ambacho si sahihi kabisa.

Kama ambavyo manispaa nyingine zimefanya jitihada za kuweka masoko yao katika hali ya kuridhisha na kuondoa takataka kila wakati, basi na Ubungo napo wafanye hivyo ili kunusuru afya za watumiaji hao.

Mwaka jana nilifanya ripoti maalum kwenye masoko ya Jiji la Dar es Salaam, na kubaini kuwa iwapo yangeboreshwa yangeweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato ambacho kingeipatia halmashauri mabilioni ya fedha.

Katika uchunguzi wangu kwenye soko hilo, nilibaini kuwa eneo hilo si mali ya Manispaa ya Ubungo bali ya kiwanda cha Urafiki Textile, na walitakiwa kuondoka katika eneo hilo wakati wowote na ndiyo sababu kubwa ya manispaa kushindwa kuliboresha soko hilo.

Soko liko kando ya Barabara ya Mabibo na hatua chache kutoka barabara ya mwendokasi.

Sasa kwa kutambua umuhimu wake na afya za watumiaji wake ni vyema hatua za haraka zikachukuliwa.

Naamini kabisa haiwezekani kukusanya fedha kwenye chanzo ambacho unaweza kukiboresha kikatoa fedha zaidi, badala yake unakusanya tu pasipo kuboresha mazingira na miundombinu yake.

Manispaa ya Ubungo haiwezi kukwepa lawama za hali ya Soko la Mabibo kwa kuwa ndiyo inayokusanya mapato.

Mjadala unatarajia kwamba kupitia vikao mbalimbali vya maamuzi fedha zinazokusanywa zitaelekezwa kwenye uboreshaji wa miundombinu husika.

Haipendezi soko hilo kuwa katika hali iliyopo kwa sasa ambayo hairidhishi na ni hatari kwa afya za watumiaji wake.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Dakika 221 za CAG bungeni

INATOKA UK.2

wa Tabora Mjini (CCM).

**DAKIKA 221**

Kamati hiyo ilitumia saa 3:41 kufanya mahojiano na Prof. Assad, huku mahojiano hayo yakifanyika kwa awamu.

Awali, Prof. Assad aliingia ukumbini 5:06 asubuhi na kutoka saa 6:45 mchana, akisubiri kamati ikijadili hoja zake na mwenendo wa mahojiano ili kama kuna haja ya kufafanua aitwe tena.

CAG Assad aliitwa tena kuingia ukumbini saa 7:15 mchana na kutoka 7:57 mchana, akaketi nje ya ukumbi kwa muda kusubiri kuitwa tena saa 8:35 mchana kuelezwa uamuzi wa shauri lake. Alitoka saa 8:47 mchana baada ya kamati hiyo kumalizana naye.

**KAULI YA KAMATI**

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kamati yake kumaliza mahojiano, Mwakasaka alisema CAG Assad alitoa ushirikiano, walimhoji na bado wanaendelea na shauri lake.

"Kamati inaendelea na kazi yake, siyo kwamba tumemaliza, ukishamsikiliza shahidi, tutaendelea na uchambuzi, lakini tukishamaliza kazi yake itamshauri Spika kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na kupeleka ripoti kwake," alisema.

Mwakasaka aliongeza: "Mtu akiitwa, lazima atakuja na vielelezo vyake, lakini vielelezo vile bado vinafanyiwa kazi, hivyo hatuwezi kuongelea kwa mujibu wa kanuni zetu.

"Hapa hakuna mgogoro, na Bunge ni mhimili unaojitegemea, hivyo hakuna mgogoro kati ya Spika na CAG. Kilichopo ni yale aliyoyatamka dhidi ya mhimili. 'Body language' (lugha ya picha) aliyokuja nayo, hajaonyesha ukaidi wowote, ametoa ushirikiano mzuri na amejibu kama ambavyo inatakiwa kujibu maswali kwa kamati."

**HALIMA MDEE**

Mwakasaka alisema Mdee atahojiwa leo na kamati hiyo kutokana na maagizo yaliyotolewa na Spika Ndugai.

"Kesho (leo) mahojiano ya Mdee yatafanyika kama ambavyo ratiba imepangwa, ni vilevile, haijabadilika, atahojiwa muda uleule saa 5:00 asubuhi kama alivyohojiwa CAG," alisema.

Januari 7, Spika Ndugai alitoa amri CAG afike mbele ya kamati hiyo kutokana na kauli hiyo aliyoitoa wakati akihojiwa na Kituo cha Televisheni cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa akiwa New York, Marekani alikokuwa akihudhuria mkutano.

Ndugai alimtaka Prof. Assad kufika mbele ya kamati hiyo kwa hiari, vinginevyo atapelekwa na polisi akiwa amefungwa pingu.

"Pamoja na kwamba analindwa na Katiba namshauri sana CAG ajitathmini upya, hatutavumilia hata dakika moja kudharauliwa na mtu yeyote na tutakasirika zaidi dharau hizi ukizifanyia nje ya nchi," alisema.

Spika Ndugai pia aliagiza Mdee kufika mbele ya kamati hiyo kuhojiwa kutokana na Waziri Kivuli huyo wa Fedha na Mipango kuweka wazi kuwa anaunga mkono kauli ya CAG.

Uamuzi wa Spika kuagiza CAG kuhojiwa na kamati hiyo ulipingwa na wadau mbalimbali wakiwamo baadhi ya wabunge walioamua kufungua kesi mahakamani kuzuia Prof. Assad kuhojiwa.

Ibara ya 143(6) ya Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1977, inazuia CAG kufuata amri ya mtu au taasisi yoyote ya serikali, isipokuwa mahakama.



Wachuuzi wa ndizi wakisubiri wateja kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana, ambapo ndizi moja iliuzwa kwa bei nafuu ya Sh. 100. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Matukio ya mauaji ya ulevi yapungua

INATOKA UK. 2

134, lakini mwaka 2018 yalipungua hadi kufikia matukio 116 ikiwa ni upungufu wa matukio 18 sawa na asilimia 13," alisema Msangi.

Alisema licha ya kupungua kwa matukio hayo, Jeshi la Polisi linatoa tahadhari kwa wazazi kutowaacha watoto kutembea peke yao, pamoja na kuwa makini na watu wasiowafahamu kuwaachia watoto.

Kuhusu matukio ya usalama barabarani, Msangi alisema matukio hayo nayo yamepungua ambapo kwa mwaka 2017 yalitokea matukio 6,022 kulinganisha na mwaka jana, ambapo yalitokea makosa 3,988 ikiwa ni pungufu ya matukio 2,034 sawa na asilimia 33.8

"Kupungua kwa matukio hayo kumeonyesha kuwa kuna juhudi za Jeshi la Polisi kupambana na matukio hayo," alisema Msangi.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa taasisi mbalimbali zikiwamo za serikali, vyama vya siasa, asasi za kiraia, asasi za kidini na Watanzania wote kuendelea kutoa taarifa za kukabiliana na matukio ya uhalifu nchini.

# Mpina anusa harufu ya ufisadi chanjo mifugo

INATOKA UK. 2

ni uendeshaji tu wa shughuli hizo tu.

Aliagiza kuandaliwa mwongozo utakaoondoa mkanganyiko huo, huku akiwanyooshea kidole madaktari wa mifugo wa mikoa na wilaya kuwa pamoja na ugatuaji huo wa madaraka, lakini bado wanawajibika kwa Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo.

Mpina alisema baadhi ya halmashauri zimekuwa zikiwapiga faini wafugaji kati ya Shilingi 5,000 na 50,000 kwa kichwa cha ng'ombe kwa kisingizio cha kushindwa kuogesha mifugo yao, ambapo hata fedha zenyewe wanazowatoza hazirudi kuhudumia mifugo badala yake zinaishia kugawana posho za vikao na kuwageuza wafugaji kuwa chanzo chao cha mapato.

Pia alimwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kukaa pamoja na kuondoa mwingiliano wa majukumu wa taasisi hizo mbili ambao kwa kiasi kikubwa unaathiri usimamizi na udhibiti wa utoaji huduma za mifugo.

Kuhusu kile kinachodaiwa kuwa mgongano wa kimajukumu kati ya Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo na Wakala wa Maabara za Veterinari TVLA, Waziri Mpina, aliagiza kufanyike uchambuzi wa kina ili kubaini kama kuna upungufu wa kikanuni na kisheria katika utekelezaji wa majukumu yao na kwamba ifikapo mwezi ujao taarifa hiyo iwe imewasilishwa ofisini kwake kwa hatua zaidi.

Katika hatua nyingine Waziri Mpina ameelezea nia ya serikali kuboresha mfumo wa utoaji mafunzo ya astashahada na stashahada ya afya na uzalishaji wa mifugo pia kuweka mfumo utakaorasimisha na kuendesha mafunzo atamizi (internship) kwa madaktari wa mifugo wanaohitimu mafunzo.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Dk. Hezron Nonga, alimhakikisha Mpina kuwa maagizo yote aliyoyatoa atayasimamia kikamilifu ili kuleta mageuzi makubwa katika sekta, ambapo alisisitiza kuwa zaidi ya asilimia 60 ya magonjwa ya kuambikizwa binadamu yanatoka kwa mifugo.

Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk. Furaha Mramba, alimshukuru Mpina kwa juhudi kubwa za kuisaidia Taasisi ya Chanjo Kibaha na kwamba usimamizi na maagizo yake aliyoyatoa Agosti mwaka jana kumewezesha taasisi hiyo kuanza kuzalisha chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP), ambapo hivi sasa iko katika hatua za mwisho za majaribio.

HABARI KITAIFA

# Taasisi 4 zaagizwa kuipa TTB mil. 489/-

**Na Renatha Msungu**

SERIKALI imetoa siku saba kwa taasisi nne zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuwasilisha Sh. 488,815,005.88 kwa Bodi ya Utalii nchini (TTB), kwa ajili ya ujenzi wa studio, mabango ya utalii na maagizo ambayo walipewa na wizara hiyo.

Taasisi hizo ni Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori na TAWA.

Maelekezo hayo yalitolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya TTB jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara ya kupata ripoti ya utendaji kazi mwishoni mwa wiki.

Alisema TTB itapaswa kuwasiliana na taasisi hizo kwa ajili ya kupatiwa fedha hizo.

Waziri huyo alifafanua zaidi ya kuwa kiasi hicho cha fedha kutapaswa kutumiwa na bodi hiyo kwa ajili ya kazi ilizoelekezwa ili utekelezaji uanze haraka iwezekanavyo.

Alifafanua zaidi ya kuwa lengo ni kuona utalii wa ndani unatangazwa na watu mbalimbali ambao ni maarufu badala ya kusubiri raia kutoka nje wakati nchini watu maarufu wapo.

Alisema baada ya fedha hizo kufika TTB anahitaji kuona kazi zinaanza ili kuendeleza utalii kama alivyowaagiza na kwamba wizara imepokea maombi ya watu mbalimbali kwa kutaka kwenda kurekodi filamu na nyimbo katika baadhi ya hifadhi.

Alisema jambo hilo ni zuri kwa sababu watakapoanza kuonyesha filamu zao, hifadhi na utalii utatangazika duniani kote.

"Nawaomba kuangalia sana watu maarufu wanaweza kututangazia sana utalii wetu," alisema Kigwangalla.

Alisema hakuna sababu ya kukaa kimya kinachotakiwa ni kuingia nao mikataba ambayo itawanufaisha wao pamoja na wizara.




# Bil. 3.5/- kujenga makazi ya polisi

**Na Mwandishi Wetu**

NYUMBA 100 za makazi ya askari zimeanza kujengwa mkoani Dodoma ukiwa ni mpango wa serikali kukabiliana na changamoto za makazi ya askari polisi watakaohamia hivi karibuni.

Hatua hiyo inafuatia uamuzi wa serikali kuanza kutekeleza agizo la kuhamishia makao makuu ya nchi mkoani Dodoma.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama kutembelea eneo la Medeli Mashariki, ambapo awamu ya kwanza ya mradi huo ukihusisha nyumba 30, ujenzi wa shule ya awali, ujenzi wa kantini, ujenzi wa viwanja vya michezo umeshaanza.

**Nawapongeza kwa kutumia mapato yenu wenyewe ya ndani kuanzisha miradi mikubwa kama hii, na sisi wajumbe wa kamati tumeridhishwa na hatua hizi za kukabiliana na makazi ya wapiganaji wetu.**

"Ujenzi wa nyumba hizi unakwenda sambamba na ujenzi wa nyumba kama hizi katika maeneo mbalimbali nchini kuhakikisha askari wanaishi sehemu safi na lengo la serikali ni kuhakikisha ujenzi wa nyumba kama hizi kote nchini unafanyika kwa gharama nafuu na tukitumia wataalamu wa ujenzi waliopo serikalini na katika Jeshi la Polisi," alisema Masauni na kuongeza:

"Mradi huu utakuwa na awamu tatu, ambapo mwezi Aprili mwaka jana, awamu ya kwanza ilianza na kutarajiwa kukamilika Aprili mwaka huu, huku awamu zilizobakia zikitarajiwa kukamilika mwisho wa mwaka huu na hadi kufikia mwaka kesho katikati awamu zote zitakuwa zimekamilika."

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Mussa Zungu, aliwapongeza viongozi wa wizara na Jeshi la Polisi kwa mradi huo, huku akishauri miradi mingine wajenge maghorofa ili kuitumia ardhi waipatayo kwa matumizi mengine sambamba na ujenzi wa makazi ya askari.

"Nawapongeza kwa kutumia mapato yenu wenyewe ya ndani kuanzisha miradi mikubwa kama hii, na sisi wajumbe wa kamati tumeridhishwa na hatua hizi za kukabiliana na makazi ya wapiganaji wetu wanaotulinda usiku na mchana na nchi yetu kuendelea kuwa na amani," alisema Zungu.

Jumla ya gharama ya mradi huo wa nyumba 100 ni Sh. bilioni tatu, ambazo zinatokana na Mfuko wa Tuzo na Tozo yakiwamo malipo ya huduma mbalimbali zinazotolewa na askari polisi na faini zinazotozwa na askari kwenye makosa mbalimbali.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akiteta jambo na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Daudi Mayeji (kushoto). **PICHA: DEGE MASOLI**

# Nyufa madarasa zatishia usalama wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wanaosoma katika Shule ya Msingi Jomu Shinyanga mjini, wapo hatarini kuangukiwa na shule hiyo kutokana na baadhi ya madarasa yake kupasuka nyufa.

Imeelezwa shule hiyo ilianza kutoa elimu mwaka 1964 na kusajiliwa rasmi mwaka 1975 kwa namba 17/1/008 na sasa imefikisha umri wa miaka 55, ambapo madarasa yake yameshachakaa na kutishia usalama wa maisha ya wanafunzi.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Sarah Maloda, wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ya kukagua majengo ya shule pamoja na usafi wa mazingira hasa kwenye upande wa vyoo.

Alisema shule hiyo ina jumla ya madarasa 12, lakini matano hayatumiki kabisa kutokana na kupasuka nyufa, hivyo kubaki kutumia saba yaliyosalia, na kusababisha kuwa na upungufu wa madarasa, huku shule hiyo ikiwa na wanafunzi 400, ambapo kila darasa linatakiwa kukaliwa na wanafunzi 45.

"Changamoto kubwa ambayo tunayo hapa shuleni ni ubovu wa baadhi ya madarasa, ambayo yamepasuka nyufa kabisa na kutishia usalama wa maisha ya wanafunzi, na siku moja yanaweza kuanguka na kutokea maafa makubwa," alisema Maloda.

Naye DC Mboneko baada ya kuelezwa changamoto hiyo ya ubovu wa madarasa, alitoa maagizo kwa ofisa elimu msingi wa Manispaa ya Shinyanga, kuifanyia ukarabati wa haraka shule hiyo ili kunusuru maisha ya wanafunzi.

Ofisa elimu huyo wa shule za msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, alisema walishatuma mhandisi wa ujenzi kufanya upembuzi yakinifu, na ifikapo Machi mwaka huu wataanza kuyakarabati madarasa hayo kupitia fedha za mapato ya ndani.

# Jaji Mihayo: Bodi TTB imefanya mengi

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji Thomas Mihayo, amepingana na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, kuwa bodi hiyo imeshindwa kutimiza majukumu yake.

Waziri Kigwangalla, wiki iliyopita alitangaza kuivunja bodi hiyo, akisema kuwa imeshindwa kutimiza majukumu yake, lakini Jaji Mihayo, Jumapili aliikosoa hatua hiyo, alisema bodi yake tangu ilipoingia madarakani imetimiza majukumu yake na kutekeleza mambo mengi makubwa.

**Tangu aingie katika bodi hiyo hajawahi kupewa maelekezo yoyote na Waziri Dk. Kigwangalla licha ya hatua hizo alizozichukua.**

Jaji Mihayo alisema wakati wanaingia bodi hiyo ilikuwa na changamoto lukuki ikiwamo madeni makubwa.

"Tumeingia hapa TTB ilikuwa inadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 7, ilikuwa na akaunti mbili za fedha, moja ya dola na nyingine ya shilingi. Akaunti ya dola ilikuwa na Dola 7000, na akaunti ya shilingi ilikuwa na Sh. milioni 12. Bodi hii ilikuwa imesimama, sasa tumepambana na sasa hivi tumepunguza deni hadi kufikia Sh. bilioni 1.5," alisema na kuongeza:

"Siyo jambo baya tumefanya vizuri ukiangalia na mambo mengine ambayo tumekuwa tukiyafanya kama kutangaza utalii na kadhalika, yote haya tutakuja tuueleze umma wa Watanzania na mambo mengine ambayo tunafikiri hatukutendewa haki."

Jaji Mihayo pia alisema tangu aingie katika bodi hiyo hajawahi kupewa maelekezo yoyote na Waziri Dk. Kigwangalla licha ya hatua hizo alizozichukua.

"Nina hakika toka waziri wa sasa, Dk. Kigwangala ateuliwe kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hajawahi kuita bodi hii kuipa maagizo, hajawahi kuiandikia maagizo wala hajawahi kunipigia mimi simu Mwenyekiti wa Bodi kunielekeza mambo yoyote, sisi ni binadamu tunaweza kukosea, lakini tunafikiri hatukustahili yote yaliyotokea," alisema Jaji Mihayo.



Wafanyakazi wa Kiwanda cha Ngomeni Kamba (TANCORD), kilichopo wilayani Muheza mkoani Tanga, wakiwa kwenye mgomo wa kutofanya kazi na kujikusanya nje ya kiwanda hicho kama shinikizo la kudai mishahara yao ya miezi mitatu. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Kibano cha mafataki chaanza rasmi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga, imeanzisha dawati la jinsia ambalo litakuwa likishughulikia masuala ya rushwa ya ngono shuleni.

Imeelezwa tatizo la rushwa ya ngono kwa wanafunzi mkoani Shinyanga limeendelea kwa kasi, lakini waathirika ambao hufanyiwa matukio hayo wamekuwa waoga kwenda kutoa taarifa kwenye ofisi za Takukuru.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Shinyanga, Francis Luena, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana, kuwa ofisi hiyo imepokea jumla ya malalamiko ya rushwa 90, ambapo kesi 19 zimeshafunguliwa mahakamani.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi juu ya vitendo vya rushwa ya ngono shuleni, kuanzia msingi, sekondari hadi vyuo, lakini kutokana na waathirika wenyewe kuwa waoga kwenda kutoa taarifa Takukuru, imewalazimu kuanzisha dawati hilo ili kutokomeza rushwa hiyo.

"Tumekuwa tukipokea malalamiko mengi kutoka kwa wazazi juu ya watoto wao kuombwa rushwa ya ngono shuleni, lakini tatizo hilo huwezi kulifanyia kazi bila ya ushahidi, ndio maana imetubidi kuanzisha dawati hili, ambapo wanafunzi watakuwa wakija kutoa taarifa na kuifanyika kazi na kuwakamata wahusika," alisema Luena.

"Napenda kutoa wito kwa wanafunzi wote mkoani Shinyanga, pale wanapokuwa wakiombwa rushwa ya ngono kutoka kwa walimu wao, wasisite kuja katika ofisi za Takukuru, ikiwa kwa sasa tumeanzisha dawati la jinsia ambalo litakuwa na wanawake tu, watakao kuwa wakishughulika na kesi za namna hiyo," aliongeza.

Aidha, alisema katika mikakati yao ya mwaka 2019 ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na wanafunzi juu ya kupinga vitendo vya rushwa, kupitia kwenye mikutano ya hadhara, semina pamoja na kuunda klabu za wapinga rushwa shuleni, ili kutokomeza kabisa vitendo hivyo mkoani hapa.

Katika hatua nyingine alisema walifanya ukaguzi kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo tisa yenye jumla ya thamani ya Shilingi bilioni 5,5 na kubaini kuwapo na matumizi mabaya ya Shilingi milioni 4.3 kwenye ujenzi wa machinjio ya Maganzo wilayani Kishapu wenye thamani ya Shilingi milioni 12.

# DC azuia vivuli vitambulisho wamachinga

**Na Futuna Seleman,** MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Fillberto Sanga, amepiga marufuku watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kuwalazimisha wananchi wanaotoka vijijini kupiga vivuli fomu za usajili wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo wanaotaka kujiorodhesha ili watambulike waweze kupata vitambulisho hivyo.

Aliyasema hayo baada ya kuzindua ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali 265 wa Kata ya Mkuranga waliojiorodhesha na kuhakikiwa kuwa wana sifa za kupewa vitambulisho hivyo.

Alisema hatua hiyo inawakatisha tamaa wananchi ambao baadhi yao watalazimika kutembea umbali mrefu na baadhi ya maeneo yanapochukulia fomu hizo hakuna huduma za kutoa vivuli, hali inayozua manung'uniko miongoni mwa wananchi.

"Ofisa biashara kwani hizo photocopy Shilingi ngapi si shilingi mia tu jamani, hivi hata photocopy wananchi wahangaike mtu atoke Bupu kweli aje hadi Mkuranga kwa ajili ya photocopy tu, hili hapana haliwezekani wasaidieni wananchi tufanikishe zoezi hili msiwakatishe tamaa," alisema.

"Katika hili hakuna huruma kama una biashara yako una duka usithubutu kuvaa kitambulisho hicho sababu ukivaa wanafuatilia siku hadi siku kama je, huyu mtu tuliyempa kitambulisho ni mlengwa. Serikali imelenga kumsaidia mjasiriamali mdogo," alisema.

Alisisitiza wote watakaonufaika na vitambulisho hivyo wavivae wanapokuwa katika maeneo ya biashara zao kama ambavyo mtu anavaa pete ama saa.

"Usichukue ukakifungia ndani unaogopa kisichafuke au kuharibika ukikipokea kifanyie kazi uvae kama mtu anavyovaa saa au pete, hiki unatakiwa uvae popote unapofanya biashara uwe nacho kama huna maana yake unafanya biashara isivyo halali," alisisitiza Sanga.

Baadhi ya wajasirimali wadogo walionufaika na vitambulisho hivyo walishukuru hatua ya Rais John Magufuli kwa kuwakumbuka wananchi wanyonge kwa kuanzisha utaratibu huo utakaowasaidia kufanya bishara zao bila kunyanyaswa kama iliyokuwa awali.

Hassan Kambangwa Mwenyekiti wa Shirikisho la watu wenye ulemavu Mkuranga, alisema Rais Magufuli amewasaidia katika hilo kwa sababu sasa badala ya kila siku kulipia ushuru ambao wakati mwingine hawapewi hata risiti na bidhaa zao kukamatwa hali hiyo itakwisha.

Naye Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkuranga, Amosye Ernest, aliwataka wajasiriamali wadogo ambao mauzo yao kwa mwaka hayafiki shilingi milioni nne wafuate taratibu za kujiandikisha na kusajiliwa ili waweze kupata vitambulisho hivyo.

# Fedha za mwekezaji zawatoa macho wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, Loata Sanare, amefanikiwa kuumaliza mgogoro uliodumu kwa miaka miwili wa kugombea fedha za pango Sh. milioni 40 uliohusisha vijiji vitatu katika Kata ya Ngabobo.

Vijiji vilivyokuwa katika mgogoro huo ni Tenki, Ngabobo na Oltepesi na fedha hizo alikuwa akilipa mwekezaji wa hoteli ya kitalii ya Africa Amini Maasai Lodge.

Sanare alimaliza ugomvi huo kupitia vikao viwili vilivyofanyika ofisini kwake na kuwahusisha viongozi wa vijiji vyote vitatu mnamo Januari 4, mwaka huu.

Wakizungumza katika mkutano wa wananchi wa vijiji hivyo mbele ya mwenyekiti huyo wenyeviti na watendaji wa vijiji hivyo walikiri kukubaliana na mgawanyo wa fedha hizo kama walivyokubaliana.

Walisema makubaliano ya mgawanyo wa fedha hizo ni kwamba vijiji viwili vya Ngabobo na Tenki vitakuwa vikipokea asilimia 25 ya mapato yote ambayo ni sawa na Sh. milioni 10, huku kijiji cha Oltepesi ambacho ardhi hiyo iko kwao kitakuwa kikipokea asilimia 50 iliyobaki ambayo ni sawa na Sh. milioni 20.

Wenyeviti hao na majina ya vijiji vyao kwenye mabano ni Francis Mollel, (Tenki), Isack Paulo, (Ngabobo) na Willium Lehaleyi, (Oltepesi) ambao wote kwa pamoja na watendaji wao waliingia makubaliano na kusaini mkataba mbele ya mwenyekiti huyo wa CCM ofisini kwake.

Awali fedha hiyo ya pango la ardhi ilikuwa ikichukuliwa na kijiji kimoja cha Ngabobo kabla ya kijiji hicho kugawanywa na kutoka vijiji vingine viwili.

Ardhi hiyo ilitolewa kwa mwekezaji huyo mnamo mwaka 2012 na ujenzi wa hoteli hiyo ulianza mwaka 2013 na kukamilika kisha kuanza kazi mwaka 2015 kwa makubaliano ya kukilipa kijiji Sh. 10,000 kwa kila mgeni mmoja na watoto Sh. 5000.

# Kuhamishwa stendi kwaathiri mapato CCM

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KUHAMISHWA kwa stendi ya zamani ya mabasi na kwenda eneo la Makatanini, wilayani Babati kumeathiri mapato kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Manyara, huku Halmashauri ya Mji wa Babati ikineemeka.

Kaimu Katibu wa CCM, Mkoa wa Manyara, David Amos Madelu, aliiambia Nipashe mwishoni mwa wiki kuwa baada ya halmashauri kuihamisha stendi hiyo chama kimeathirika kimapato kutokana na kukosa fedha walizokuwa wanazikusanya kwa mwezi.

Eneo la stendi ya zamani lilikuwa likimilikwa na CCM Mkoa wa Manyara, hivyo walikuwa wakigawana mapato na halmashauri.

"Kwa mwezi tulikuwa tunakusanya Sh. milioni 12.3, hivyo tumezikosa japo kisheria kama CCM haturuhusiwi kukusanya mapato ila kwa sasa tumeomba gari ziwe zinapita pale na kushusha abiria bila kutozwa ushuru ila zipite stendi mpya zilipe ushuru," alisema.

**Kwa mwezi tulikuwa tunakusanya Sh. milioni 12.3, hivyo tumezikosa japo kisheria kama CCM haturuhusiwi kukusanya mapato ila kwa sasa tumeomba gari ziwe zinapita pale na kushusha abiria bila kutozwa ushuru ila zipite stendi mpya zilipe ushuru.**

Alifafanua kuwa CCM hawajazuia stendi kuhama ila wanawahurumia abiria kwenda kuwashushiwa stendi mpya wakati wa usiku na ukizingatia stendi hiyo iko mbali na mjini na ni sehemu ambayo haina huduma za kijamii.

Aliongeza kuwa wanatarajia kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa ili kama inawezekana stendi ya zamani magari yawe yanashusha abiria na kuondoka.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, William Haaly, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki alisema mapato katika stendi mpya yaliyokusanywa kwa wiki mbili zilizopita hadi kufikia Januari 16, mwaka huu ni Sh. milioni 45.3.

Alisema miongoni mwa huduma zilizoingiza fedha ni pamoja na ushuru wa vyombo vya usafiri ingawa hakutaja kiasi.

Lakini alisema kwa upande wa huduma ya choo cha kulipia walipata Sh. milioni 1.34 na vibanda Sh. milioni 34.9.

Alisema mtu anayeingia stendi anatakiwa kulipia Sh. 200, ambapo kwa siku moja waliyoanza walikusanya Sh. 70,800 pamoja na faini mbalimbali za watu wanaochafua mazingira kwa kujisaidia vichakani zimekusanywa Sh. 1,050,000.

Aidha, alisema wanajipanga kuboresha miundombinu ya stendi hiyo, ili itoe huduma kwa viwango stahiki kwa wananchi wa Babati na viunga vyake, lakini huku fedha hizo zikisaidia kuimarisha huduma za kijamii.

Mfanyabiashara Nyange Polepole katika stendi ya zamani alisema, baada ya stendi kuhama hali ya biashara imekuwa mbaya kwa kuwa hawapati wateja na mauzo yameshuka.

Kwa upande wake, Bohari Iddy, alisema shida wanayoipata abiria ni kubwa kwa kuwa wengine hadi wafike stendi mpya ni umbali wa kilometa tano hivyo wakiwa wanasafiri wanashindwa kuyawahi magari.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni, akimkabidhi 'redio call' Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makaka, ikiwa ni moja ya vifaa vilivyotolewa msaada na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamiaji (IOM) jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ofisi za Uhamiaji mipakani. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# TAHA kutosheleza soko la mboga, matunda

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

TAASISI ya wakulima wa mboga, matunda na maua Tanzania, (Taha), imeweka bayana mwelekeo wa utendaji wa kazi kwa mwaka 2019, huku ikidhamiria kutosheleza soko la ndani la bidhaa zake na kufikia masoko ya kikanda, Afrika na Ulaya.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Taha, Jackline Mkindi, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya utendaji kazi wa chama hicho kwa mwaka huu.

Alisema mwaka jana licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali, sekta ya kilimo ilikuwa na wawekezaji waliweza kupata masoko hasa katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Aliongeza kuwa ripoti ya East African Trade and Investiment ya mwaka jana, imeonyesha mauzo katika masoko ya kikanda yameendelea kuongezeka sana.

Alisema kwa mfano, mwaka jana mauzo hayo yaliongezeka kwa asilimia 11, wakati mwaka juzi Tanzania iliuza mazao katika soko la kikanda yenye thamani ya dola laki 6 milioni.

Mwaka 2017 Tanzania iliuza katika soko la kikanda la Afrika Mashariki bidhaa zenye thamani ya zaidi ya dola laki 7, kwa hiyo, kuongeza mauzo yake katika soko la kikanda kwa takribani asilimia 11.

"Kwa hiyo utaona kati ya asilimia hizo 11, asilimia kubwa au 6 hivi inatokana na mazao ya mboga na matunda," alisema na kusisitiza, Tanzania imeongoza kwa mauzo katika masoko ya kikanda ya Afrika Mashariki," alisema.

Pamoja na soko la kikanda, lakini alisema watashambulia sana soko la ndani ambalo kwa mujibu Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), idadi ya Watanzania ina kadiriwa kuwa zaidi ya milioni 54.

Hata hivyo, alisema bado kuna kazi kubwa ya kuhamasisha Watanzania kupenda kutumia mboga na matunda katika mlo.

Aidha, alitaja mikakati mingine watakayojikita nayo kuwa ni kutoa ushawishi na utetezi kwa wadau mbalimbali wa kilimo ikiwamo serikali ili kuweka sera na mazingira mazuri ya kukuza kilimo cha biashara ya mboga na matunda.

Kwa upande wake, Meneja Sera na Utetezi, Kelvin Remen, alisema Sheria ya VAT ya 2014, inazuia uuzaji nje wa bidhaa zozote bila ya kuziongezea thamani.

Remen alisema serikali ilikuwa na nia nzuri kutunga sheria hiyo kwa bidhaa zingine kama vile madini, lakini kwa bidhaa kama matunda kuna changamoto zake.

# Nguvu ya upinzani 2015 yaitisha CCM Kilimanjaro

**Na Paul William,** MOSHI

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Gaudensia Kabaka, ameitwa na wanachama wenzake mkoani Kilimanjaro kujadiliana namna ya kukabiliana na upinzani katika uchaguzi wa serikali za mitaa ambao utafanyika mwaka huu.

Kabaka ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, ameombwa kuongeza nguvu pamoja na kuwapa mbinu za namna ya kuwakabili wapinzani katika uchaguzi huo.

Habari zilizopatikana jana na kuthibitishwa na Katibu wa UWT Mkoa wa Kilimanjaro, Mary Sule, zinaeleza kuwa Kabaka ameridhia wito huo na leo atatua Moshi mjini kuanza rasmi vikao na mikutano ya ndani.

"Kabaka ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, anakuja kuwasihi wanachama kuunganisha nguvu pamoja tunapoelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa, yeye ndiyo mlezi wa Mkoa wa Kilimanjaro na amekuwa hataki watu wanaounda makundi. Kimsingi anakuja kuyavunja makundi yote yaliyopo kwa sasa yaliyotokana na uchaguzi mbalimbali.

**Mwaka 2015 Mkoa wa Kilimanjaro CCM kiliambuliwa wabunge wawili kati ya tisa, huku Chadema kikipata wabunge sita na NCCR-Mageuzi kikipata nafasi moja.**

"Unajua mwenyekiti huyu wa UWT, anataka wanachama wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro wahakikishe kwamba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wagombea wa chama tawala wanashinda ubunge wa Moshi Mjini, Hai, Rombo, Vunjo na Moshi Vijijini maeneo ambayo wapinzania wanatamba."

Mwaka 2015 Mkoa wa Kilimanjaro CCM kiliambuliwa wabunge wawili kati ya tisa, huku Chadema kikipata wabunge sita na NCCR-Mageuzi kikipata nafasi moja.

Zaidi Sule ameeleza: "Katika uchaguzi huu, tunajipanga vizuri na tutazungumza na wanachama wa CCM kata kwa kata, mtaa kwa mtaa, kijiji kwa kijiji, ili kujua changamoto zao na kuhakikisha tunarekebisha makosa na kukomboa maeneo yote yanayoongozwa na wapinzani."

Pamoja na harakati hizo za kuanza kung'oa mizizi ya ngome hiyo ya upinzani, Kabaka pia anadaiwa kuja kuhamasisha wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na umoja huo, Kabaka ataanza ziara yake katika Wilaya ya Same na kufuatiwa na Mwanga, Rombo, Moshi Vijijini na Mjini na kumalizia katika Wilaya za Hai na Siha.



Mamalishe akihudumia wateja kando ya Barabara ya Sokoine, katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wajasiriamali watoa siri ya kuanzisha kiwanda

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAJASIRIAMALI wachache waliothubutu kuanzisha kiwanda cha kuzalisha chaki cha Suma Super Chalk Ltd kilichopo Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro wamesema utafiti wa kisayansi na tafsiri sahihi ya sera ya viwanda kulingana na mazingira, ndiyo siri ya mafanikio yao.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Abdulkarim Lema, alisema kutokana na tafsiri ya sera, nafsi ya kutaka kuwa na kiwanda hicho iliwasukuma kuwashirikisha watendaji wote muhimu kutoka ngazi ya mkoa, wilaya hadi kata kuhakikisha kila mtu anaafiki na kufurahia ujio wa kiwanda hicho muhimu katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

"Nadharia mbalimbali za uchumi zinataka watu wenye uthubutu na ndio maana sisi tumekuja na kiwanda hiki muhimu ambacho kitapunguza gharama za uagizaji wa chaki kutoka mikoa mingine. Kuna fursa ya ajira, kodi ya serikali na mzunguzuko wa fedha pia utazinufaisha wilaya za mkoa wa Kilimanjaro kutokana na mauzo,"alisema Lema.

Alisema mpango uliopo ni kukipanua zaidi na kuongeza uzalishaji wa vifungashio, kwa vile wakati wanaanza walikuwa wakizalisha makasha 10 kwa siku kutokana na matambo waliyokuwa nayo.

"Kwa sasa tumenunua mashine kubwa ambayo kwa siku tunazalisha boksi 50 (makasha), lakini kama soko litakuwa zuri, tunao uwezo wa kuzalisha chaki nyingi zaidi na tulipofikia kwetu ni hatua kubwa tumepiga. Tunachoomba kwa serikali hasa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kutuunga mkono katika jitihada ambazo tumeanza kuzionyesha," alisema mkurugenzi huyo.

Chaki hizo zinatarajia kupunguza kwa kiasi kikubwa uagizaji kwa ajili ya shule za msingi na sekondari za mkoa wa Kilimanjaro kutoka maeneo tofauti au nje ya nchi.

# Kamishna asema idara maendeleo jamii imevamiwa

**Na Mary Mosha,** MWANGA

KAMISHNA wa Wizara ya Afya anayeshughulikia idara ya maendeleo ya jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, amesema kuna watu ambao wameanza kuvamia taaluma ya ustawi wa jamii, wakidhani ni kazi holela inayoweza kufanywa na mtu yeyote.

"Kazi za ustawi wa jamii ni muhimu na zinapaswa kufanywa na wataalamu wenye weledi, wanaotoa huduma kwa kuzingatia maadili na miiko ya kazi. Ni kazi ya kuogopa kufanya, siyo kila mtu anaweza kuifanya, hivyo wanaovamia huduma za ustawi wa jamii bila kupata mafunzo wakome na waache mara moja," alionya.

Dk. Ng'ondi ametoa angalizo hilo, wakati akizungumza na mamia ya wananchi katika mahafali ya kwanza ya Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kisangara kilichopo Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Kutokana na wavamizi hao wa taaluma kuibuka, Kamishna huyo amewasihi wahitimu hao kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na miiko ya taaluma yao, ili kujitofautisha na watumishi wengine kutokana na elimu waliyoipata.

Kuhusu udahili wa wanafunzi wa kada hiyo, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema kuwa kwa mwaka wa masomo 2018/2019, chuo hicho kimedahili wanafunzi 158, ambapo wanafunzi wa kike ni 115 na wa kiume ni 43.

Ongezeko hilo katika udahili ni zaidi ya asilimia 100, ukilinganisha na udahili uliofanyika mwaka 2016/17.

Taaluma ya ustawi wa jamii msingi wake ni haki na ustawi katika jamii ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayeachwa nyuma na kubaguliwa ama kutengwa katika huduma mbalimbali za maendeleo ya jamii husika.

Pia taaluma hiyo ni muhimu katika kuwasaidia watu walio katika makundi tete mfano wanaonyanyaswa, wanaonyanyapaliwa na maskini ili waweze kufaidika na rasilimali au huduma mbalimbali.

Kufuatia mafanikio hayo katika udahili, wizara hiyo imewapongeza wazazi na walezi kwa kuthamini utoaji wa fursa sawa kwa mtoto wa kike na kuwezesha udahili wa wanafunzi wa kike.

kufikia asilimia 73, ukilinganisha na asilimia 43 ya wavulana, ongezeko ambalo ni takribani ni mara mbili zaidi ya wavulana.

Kabla ya Dk. Ng'ondi kueleza changamoto hiyo, awali Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, Anna Mwingira, alieleza kuwa chuo hicho kwa sasa kinatoa mafunzo katika fani ya Ustawi wa Jamii ngazi ya cheti na diploma (NTA Level 4, 5 na 6) na fani ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (ECD) ambayo inasimamiwa na Wizara ya Afya.

Chuo kinaendesha masomo kwa kutumia mtaala wake wa fani ya ustawi wa jamii, ambao ulikamilika mwaka 2016/2017.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 22, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?

ALIMWA FAINI KUMTUMA PAKA KWA NJIA YA POSTA




## Mapana, marefu ya kupungua kwa uwezo wa kufikiri tangu 1980

Ukurasa 15




# 'Fikiri mara mbili' sanaa inayolenga kuchangia utatuzi mimba za utotoni

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Jamani Kiswahili kinafishwa!

'FISHA' (kitenzi) ni sababisha kufa, ondoa uhai wa kitu, ua. Fishana, fishia, fishwa.

"Yanga SC ni vibe kama lote Taifa" ni kichwa cha habari cha gazeti la michezo lililoandika:

"Nahodha wa Yanga, Kelvin Yondani na kiungo Mzimbabwe, Papy Tshishimbi, wamewashusha presha mashabiki wa timu hiyo baada ya jana kuungana na wenzao katika mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Chuo cha Polisi, Kurasini, jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mchezo wao wa leo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya JKT Tanzania." (maneno 53)!

Paragrafu ya tatu yenye maneno 48, imeandikwa:

"Yondani ambaye ni kipenzi cha mashabiki wa Yanga, anaweza kuwa ni miongoni mwa wachezaji wa timu hiyo watakaoivaa JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam ili kuimarisha safu ya ulinzi ya Wanajangwani hao waliopania kuendeleza 'vibe lao kama lote' la ushindi ndani ya ligi hiyo yenye timu 20."

Sentensi ni tungo yenye kiima (sehemu ya sentensi yenye kukaa mtenda) na kiarifa (sehemu ya sentensi inayojengwa kwa kitenzi, shamirisho* na chagizo*).

*Shamirisho ni jina linalokaa pahali pa kitendwa au kitendewa katika sentensi. *Chagizo kwa muktadha huu, ni jumla ya vielezi vilivyomo katika sentensi. Pia ni neno lenye maana ya 'usumbufu' lisilohusiana na mjadala huu.

Mwandishi aandike maneno yanayoeleweka ili msomaji asihangaike kutafuta maana yake. Msomaji asipoelewa, hawezi kuendelea kusoma! Atasomaje wakati haelewi?

'Vibe lao kama lote' maana yake nini? Mara nyingi ninapotumia maneno ninayodhani hayaeleweki kwa wengine, huyatolea ufafanuzi ili kuwarahisishia wasomaji na pia kuwapa maana ya baadhi ya maneno ya Kiswahili.

"Naye mshambuliaji wa Yanga, Mrisho Ngassa ambaye kwa siku za karibuni ametokea kuwa tegemeo katika kutengeneza pasi za mabao na kufunga pia, amewataka mashabiki wao kujaza uwanja kwa kuwa amewaandalia 'surprise.'

Kama lugha yetu ya Kiswahili yatushinda kuitumia itakiwavyo, kwa nini twapenda kutumia maneno ya Kiingereza ambacho pia hutuwezi kukitumia itakiwavyo?

Maana ya 'surprise' ni mshangao, mastaajabu, mzimbao. Kwa hiyo ingeandikwa kwa ufupi kuwa " ... amewataka mashabiki wajaze uwanja kwa kuwa atawashangaza."

Gazeti lingine la michezo liliandika: "Mbelgiji shangwe kama lote Msimbazi." Chini ya kichwa hicho iliandikwa:

"Simba wamerejea ndani ya Tatu Bora ya Ligi Kuu Bara, lakini Kocha Mkuu wake, Patrick Aussems ni kama hajaridhika, huku akisisitiza kikosi chake hata akikosekana nani, bado wanaweza kumpiga yeyote ndani na nje ya uwanja."

'O-ote' maana yake ni bila kubagua au kuchagua; na 'ote' ni bila kubaki kitu. " ... Shangwe kama lote ..." maana yake nini?

"Ninje apewa shavu jingine TFF." 'Shavu' ni minofu iliyo upande wa kulia na kushoto kwenye uso wa mtu. Wingi wa 'shavu' ni 'mashavu.' Ninje ambaye majina yake kamili ni Ammy Ninje alikuwa na shavu moja tu ndio maana TFF ilimwongezea lingine?

"Mwalimu Kashasha shangwe kama lote Sauzi," "Kashasha mfuniko Sauzi kama yote." Vichwa hivi viwili vinaeleweka kwa mwandishi aliyeviandika tu. Apaswa kutambua kuwa hajiandikii yeye bali wasomaji ambao ndiwo wanunuzi. Kama hawaelewi yanayoandikwa humo watanunua?

"Hata watasha kuna ombaomba buana!" Mwandishi hatuelezi 'watasha' ni watu wa aina gani; kama asivyotueleza pia maana ya 'buana.' Nashangazwa na ukimya wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)! Ina maana linakubaliana na upotoshwaji huu wa lugha ya Taifa?

"Azam raha kama zote" ni kichwa cha habari kikifuatiwa na sentensi ifuatayo:

"Asikuambie mtu, raha waliyonayo Azam kuanzia benchi la ufundi kupitia kwa kocha wao, Hans Van Pluijm pamoja na wachezaji ni kama zote, baada ya mwendelezo mzuri wa matokeo bora ya Ligi Kuu Tanzania Bara."

Mwandishi katumia maneno 'kama zote' mara mbili lakini hakueleza maana yake! Ina maana upotoshwaji wa lugha ya Kiswahili unakubaliwa hata na wahariri?

Wanaodurusu (soma kwa makini, pitia tena yaliyoandikwa) habari/makala huwa hawayaoni haya au wameambiwa kutosahihisha yanayoandikwa? Kama ndivyo, wameajiriwa kufanya kazi gani?

"Kitenge, ambaye alifunga 'hat trick' mchezo wao dhidi ya Yanga uliomalizika kwa kufunga mabao 4-3, alisema atahakikisha anafanya tena hivyo dhidi ya Simba leo."

Ilivyo sentensi hiyo ni kwamba Kitenge wa Stand United ndiye aliyefunga mabao 4-3 dhidi ya Yanga! Haikuwa hivyo kwani Yanga ndio iliyofunga mabao 4 na Kitenge wa Stand United kufunga mabao 3, washindi wakiwa Yanga.

"Kwa upande wake, kipa Kitenge alisema: Nitahakikisha nazitumia vizuri nafasi nitakazozitapa, hivyo endapo wakizubaa tu nitarudisha historia niliyopeleka Yanga na kuwafunga hat trick nyingine."

Inavyoelekea ni kwamba mwandishi alivutiwa mno na Kitenge hata kumpa nafasi mbili uwanjani kwamba alikuwa mshambuliaji na pia golikipa kwa wakati mmoja!

Soma jinsi waandishi wanavyokurupuka kuandika sentensi zisizoeleweka! "Staa anayeshikilia rekodi ya mabao kwa nyota wa kigeni, Amissi Tambwe ameamua kufanya kweli baada ya kuanza maandalizi ya kuwapiga watu ubeche wakati akijiandaa kufanya sherehe ya ndoa dhidi yake na Raiyan 'Ray Sharp.'

Nadhani tupo wengi tusiojua maana ya 'ubeche.' Kwa upande mwingine, maana ya neno 'dhidi' ni kushindana na, kinyume na; enye kupingana. "Sherehe ya ndoa dhidi yake na Raiyan ..." maana yake nini?

"Dante sasa ajitosa Simba mazima," "Manji aitosa Yanga mazima," "Mwanasiasa naye ajitosa mazima" neno 'mazima' lina maana gani?

**Methali: Mhadaaji kihadaiwa huona uchungu.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI



Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna wa Polisi (DCO) Ahmed Msangi. **PICHA: MTANDAO**

# UTATUZI WA MIGOGORO NDANI YA FAMILIA HUSAIDIA KUZUIA MAKUNDI YA UHALIFU

MIGOGORO ni hali ya kutoelewana baina ya mtu na mtu au kikundi au jamii.

Migogoro ni sehemu ya maisha ya kila siku na hutokea katika jamii zetu pale watu wanapotofautiana kimawazo ili kufikia maamuzi fulani.

Migogoro hutofautiana kulingana na jamii husika, wakati, sababu na wahusika. Kuna juhudi mbalimbali ambazo familia huzichukuwa katika kutatua migogoro ndani ya familia.

Migogoro ikitatuliwa ndani ya familia husaidia kutengeneza jamii yenye uelewano na ushirikiano ambayo huwezesha kujenga misingi bora ya maisha na kuzuia wanafamilia kujihusisha na vitendo vya uhalifu na kushirikiana na wahalifu kwa kuwaficha ili wasikamatwe.

Utatuzi wa migogoro ni hali ya kumwezesha mtu kutambua na kukabiliana na migogoro kiukamilifu, kiumakini na kwa tija.

Katika hali ya kawaida ya kiubinadamu migogoro ni sehemu ya maisha na ikumbukwe kuwa kuna watu ambao wanaifahamu migogoro katika jamii na wanajua pia namna ya kuitatua.

Kwa mujibu wa Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Ahmed Msangi, alipohojiwa na mwandishi wa makala haya alisema kuwa migogoro katika familia ni miongoni mwa sababu za uhalifu na wahalifu ndani ya jamii.

Aliongeza kuwa uzembe wa kulea watoto husababisha watoto wa mitaani ambao hujiingiza katika makundi ya uhalifu na wahalifu.

"Ni jukumu letu sote kuimarisha malezi bora ya familia ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza katika familia na jamii kwa ujumla," alisema DCP Msangi.

Ifahamike kuwa ni wajibu wa kila familia kuhakikisha inajijengea stadi za kutambua vyanzo vya migogoro inayoweza kuyumbisha umoja, mshikamano na usalama wa familia.

Chanzo cha migogoro katika familia hutokea kati ya pande mbili zinapokosa maelewano au kuwatofautiana kimtazamo kuhusu jambo fulani, kukosekana kwa uaminifu katika ndoa, masuala ya fedha, masuala ya ndugu/wazazi, uzazi pamoja na kutofautiana katika maamuzi.

Athari za migogoro katika familia nyingi inaweza kusababisha huduma duni, kutokuwa na huduma bora katika familia, ongezeko la wimbi la watoto wa mitaani, malezi ya mzazi mmoja, wizi na ukosefu wa maadili katika jamii.

Kuna njia mbalimbali za kutatua na kupunguza migogoro katika familia. Utatuzi wa migongano unahitaji umakini na stadi za hali ya juu ili kuweza kutoa maamuzi sahihi yasiyo na upendeleo kwa pande au wanajamii wanaotofautiana kimtazamo.

Ili kutatua au kupunguza migogoro kunamhitaji mpatanishi ambaye anatakiwa kuwa na sifa au stadi za hali ya juu katika kukabiliana na migogoro katika jamii.

Mpatanishi huyo lazima awe tayari kuziweka wazi pande zote zilizo katika mgogoro na wakubali kukaa katika meza ya majadiliano ya pamoja ili kuimarisha na kuendeleza amani na utulivu.

Kuna taasisi mbalimbali za serikali na wataalamu walioajiriwa na serikali kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri bure.

Hao ni maofisa wa ustawi wa jamii, wapo katika kila wilaya pamoja na dawati la jinsia na watoto la Jeshi la Polisi.

Hawa ni wataalamu wa fani hizo, ambao jamii bado haijawatambua na kuwatumia ipasavyo.

Wananchi wanapaswa kutambua kuwa kitendo cha familia kumuhifadhi mhalifu aliyetenda vitendo vya uhalifu vinavyosababisha migogoro katika familia ni kosa la jinai kama yalivyo makosa mengine, hivyo ni vyema wananchi wakajiepusha na kutenda kosa hilo.

Aidha, uwepo wa migogoro katika familia kunasababisha madhara katika jamii ikiwamo kutokuwapo kwa maadili mema katika familia, wazazi na walezi kutojali familia, hivyo kusababisha watoto kukosa uangalizi na kujikuta wanaingia katika makundi mabaya.

Katika kukabiliana na kutatua vyanzo mbalimbali vya migogoro katika familia, Jeshi la polisi nchini linaendelea na mkakati wake wa utoaji wa elimu juu ya malezi bora katika familia kupitia dawati la Jinsia na watoto katika kila mkoa ambalo linasaidia kutatua migogoro mbalimbali ya kifamilia pamoja na kuwajengea wanafamilia misingi ya malezi bora kwa watoto wao.

Wananchi wote wakiwamo wenye ushawishi mkubwa katika jamii wanapaswa kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kukemea vitendo vyote vinanyosababisha migogoro katika familia na kuwa sehemu ya usuluhisho wa migogoro hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya kusababisha migogoro badala ya kuendelea kutii na kufuata sheria za nchi zilizopo.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Mapana, marefu ya kupungua kwa uwezo wa kufikiri tangu 1980



Mmoja ya majaji wa Tuzo za Uwezo kwa wanafunzi kwa ajili ya mashindano ya kupima uwezo, akieleza vigezo vitakavyowafanya wanafunzi wa shule mbalimbali kushinda alama. **PICHA: MTANDAO**

WATAALAMU wa kupima uwezo wa kufikiri wa watoto wadogo ambao kimsingi wanabaki nao maisha yao yote wameshangazwa na mabadiliko katika matokeo ya kupima IQ (intelligence quotient) kuanzia takribani miaka 30 iliyopita.

Katika miongo iliyotangulia ya karne ya 20 uwezo wa kufikiri (IQ) ulikuwa unapanda, lakini katika miaka iliyofuata kumekuwa na mwelekeo wa kushuka kwa matokeo katika vipimo vya 'IQ', jambo ambalo linatia wasiwasi.

Kwa vile wataalamu wanapima na kuainisha kiwango, hawana maelezo halisi nini chanzo cha hali hiyo kwa kuwa sasa linakuwa suala la nadharia, ambayo ni mkusanyiko wa maeneo tofauti ya nadharia kadhaa.

Utafiti huo ambao ulifanyika nchini Norway ulihusu vijana wanaoingia Jeshi la Kujenga Taifa (kipindi cha lazima cha kutumikia jeshi kama ilivyo kawaida katika nchi nyingi duniani kwa wahitimu wa shule za sekondari na baadhi ya vyuo) kati ya mwaka 1970 na 2009.

Utata ulianzia pale ilipoonekana kuwa wale waliozaliwa mwaka 1991 walikuwa na alama za IQ ndogo zaidi kwa pointi tano kulinganisha na wale waliozaliwa mwaka 1975, lakini nao walikuwa na alama tatu pungufu za IQ ukilinganisha na wale waliozaliwa mwaka 1962.

Ilikuwa ni kinyume cha hali ya IQ kwa karne ya 20 kwa jumla ambako uwezo wa kufikiri ulikuwa unapanda asilimia tatu kwa mwaka.

Kabla ya hapo, kuanzia ugunduzi wa IQ na uchapishaji wa mada kuhusu mtiririko huo mwaka 1981 na mwanataaluma James Flynn, ilikuwa inaonyesha kuwa IQ ilikuwa inapanda kwa kasi, kukiwa na pengo la alama 18 kati ya kizazi kimoja kwenda kingine kwa miongo ya awali ya karne ya 20.

Sasa tatizo linakuja kwa mtiririko huo kuvurugika na uwezo wa kufikiri kuanza kupungua, ambako kwa utafiti huo wa Norway, mazingira hayo yanaanza kuelekea mwisho wa miaka ya 1970.

Tatizo ni kuwa siyo rahisi kusema utafiti huo ni kweli kwa nchi zote duniani au zinazoendelea kwa jumla, kwa kuwa ulichukuliwa katika vituo vya kuandikisha vijana jeshini Norway.

Ukitafuta ufafanuzi kiasi fulani wa suala hilo unapata picha ya upande mwingine, kuhusu mazingira ya upimaji IQ katika muongo uliopita, ambako taarifa moja inasema kuwa nchi zenye kiwango kidogo zaidi cha kufikiri ni zile zenye mzigo mkubwa zaidi wa magonjwa.

Ilitaja nchi kadhaa za Afrika kuwa ndizo zenye IQ ndogo zaidi duniani, yaani Equatorial Guinea, Cameroon, Msumbiji, na Gabon wakati zile zenye kiwango kidogo zaidi cha magonjwa zinaongoza kwa vipimo vya uwezo wa kufikiri, ambapo zilizotajwa kuondoza ni Singapore, Korea ya Kusini, China, Japan na Italia.

> Enzi za Profesa Mukandala wanaohitimu darasa la saba walikuwa wanaandika barua zao wenyewe na hata kwa Kiingereza, lakini hali hiyo imepungua hatua kwa hatua, kiasi kwamba hata wanaomaliza vyuo wana tatizo kwa suala hilo hivi sasa.

Ni katika vipimo vilivyotambulishwa hapo Julai 12, 2010. Magonjwa ni kikwazo.

Bila kutumia vipimo rasmi vya IQ na badala yake kuangalia ufaulu na viwango vya elimu kwa jumla hapa nchini halafu ukatumia utafiti huo, unapata picha kama hiyo.

Utafiti wa mwaka 2009 wa afya na mama na mtoto hasa wakati wa kujifungua ulionyesha kuwa kuna kiwango kikubwa zaidi cha vifo vya kinamama na watoto katika ukanda wa pwani, kuzidi viwango kama hivyo kwa vipimo vya aina moja kwa mikoa mingine.

Vipimo hivyo ni pamoja na umbali wa zahanati au kituo cha afya, uwepo wa kliniki wakati wa ujauzito, n.k, kuwa kwa vigezo au mazingira yanayofanana, bado vifo vilikuwa vingi zaidi ukanda wa pwani - lakini baadaye mada hiyo ilifia tu.

Ungechukua utafiti huo ukaoanisha na ufaulu darasani kwa watoto wa shule za msingi, uwezekano wa kupata matokeo kama hayo si mdogo, pamoja na maeneo mengine mikoani.

Kwa mfano shule za maeneo kadhaa, kwa sababu hupimwa zaidi kwa wilaya hivyo kuna mchanganyiko kimkoa pia zinaambatana na uwepo wa lishe ndogo na maeneo yenye sifa ya ushirikina kwa kiwango kikubwa hayana maendeleo darasani.

Anayejua hulka za 'parapsychology,' yaani mifumo ya hulka na mawasiliano katika ulimwengu wa roho, ni rahisi kuona kuwa mtoto ambaye mzazi wake mmojawapo anaanza kumwingiza katika uchawi, hafaulu katu masomo.

Fikiria mtoto ambaye usiku wa manane anaamshwa ajiunge na bibi yake kwenda maeneo ya madhabahu za kichawi, na athari katika mwili na ubongo wa mtoto pale anapoanzishwa hulka za kichawi ambazo zinauvaa mwili kwa vipindi fulani akiwa katika hali ya kuwanga.

Akiwa ametoka katika hali hiyo ni wa kawaida, anakula chakula cha kawaida, lakini katika hali ile nyingine mwili huo ni kama siyo wake, na vitu hivyo vinachanganyika ndani ya mwili wa kawaida kwa njia ambayo ni tata kiasi fulani.

Mazingira ya uchawi na kuwinda watu ili kupata sifa katika madhabahu za kishirikina ni kielelezo muhimu cha vifo vya mama na mtoto kwa mikoa, wilaya zote.

Ni wazi kuwa Tanzania (ambayo ina vigezo vingi tu vinavyoendana na nchi hizo zilizoshika mkia katika vipimo vya IQ mwaka 2010) iko katika mazingira tofauti ya upimaji wa IQ kwa sababu kuna maeneo mengine ambapo upungufu wa kina siyo tu wa kufikiri ila wa ngazi ya kisaikolojia ya maisha kwa jumla.

Kwa mfano hapa nchini upimaji wa IQ ungeweza kufanyika wakati wa kuangalia ufaulu wa wanafunzi shule za sekondari, kwa kuwa kwa sehemu kubwa siku hizi wanabaki katika mikoa waliyosomea madarasa ya awali, na siyo IQ ipimwe moja kwa moja.

Kuna vipimo vingine, kwa mfano mtindio wa ubongo kwa watoto wanaoanza shule, ambao unatisha.

Kuna wakati aliyekuwa Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Rwekaza Mukandala, alikataa hadharani matokeo ya vipimo vya mtindio wa ubongo kwa watoto wa umri wa kuanza shule kuwa ni theluthi moja ya watoto wote.

Alichosema ni kuwa mazingira yake binafsi ya kusoma shule ya msingi, sekondari na hadi UDSM, hasa kwa upande wa lishe na vipato vya wazazi hayatofautiani na kwingineko nchini, na kwa maana hiyo haiwezekani kuwa theluthi moja ya watoto wawe na mtindio wa ubongo.

Alichosahau Profesa Mukandala ni kuwa yako maeneo mengi ambako watoto wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma, kuandika.

Enzi za Profesa Mukandala wanaohitimu darasa la saba walikuwa wanaandika barua zao wenyewe na hata kwa Kiingereza, lakini hali hiyo imepungua hatua kwa hatua, kiasi kwamba hata wanaomaliza vyuo wana tatizo kwa suala hilo hivi sasa.

Inaendana na utafiti kuhusu kupungua kwa IQ kwa jumla katika mazingira ya miongo takribani mitatu iliyopita, kama si minne, kuanzia mwaka 1980.

Na baadhi ya wanataaluma wanadhani kuwa kuna tatizo la mabadiliko ya hali ya hewa duniani, kwa kuwa mabadiliko ya vyakula hayawezi kuwa makubwa.

Ila kuna wasiwasi kuwa kuingia kwa vifaa vinavyoondoa sehemu kubwa ya kufikiri, hesabu, kusoma vitabu vya zamani na kukariri hoja kunachangia tatizo hili.

Badala yake elimu 'imepigwa pasi' ina hoja zile zile, hulazimisha kufaulu na inadidimiza ari, fikra.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# ‘Fikiri mara mbili’ sanaa inayolenga kuchangia utatuzi mimba za utotoni

KATIKA enzi hizi zilizojaa pilika, udaku na michapo ya mitandaoni, kazi ya kuomba usikivu toka kwa watu inazidi kuwa ngumu zaidi.

Ari ya watu kujisomea vitabu na machapisho mengine ya kimaarifa au kuhudhuria semina zinazofundisha mambo ya kimaendeleo inasemekana kushuka kila uchwao.

Utafanyaje basi kuwafikishia ujumbe wa kitaalamu, tena mzito kueleweka au ujumbe unaoonewa haya na hadhira, lakini wa muhimu sana kwa maelfu ya watu ambao tayari wametingwa na pilika za maisha ya kisasa na mitandao ya kijamii?

Waelimishaji, taasisi na mashirika kadhaa yaliyogundua nguvu ya sanaa yameshaanza kuitumia kuvuta usikivu na kupenyeza jumbe mbalimbali kwa watu.

Wazo la kutumia sanaa kama zana ya kufundishia si dhana mpya nchini Tanzania na duniani kote.

Mzee Mwinamila, kwa mfano, ni mmoja wa wasanii wengi wa awali waliotumika katika kampeni za uelimishaji katika masuala mbalimbali ya maendeleo, afya, mazingira na hata ajali za barabarani.

Mbali na kuburudisha, nyimbo, michoro, mashairi, maigizo na sanaa zote kwa ujumla zina nguvu ya ulimbo au sumaku ya kuvuta usikivu wa watu.

Moja ya taasisi na mifuko inayoamini katika nguvu ya sanaa kama zana yenye nguvu kubwa ya kufikisha ujumbe wa muhimu katika jamii pana ni Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania, kupitia programu yake ya utamaduni.

Kwa dhamira ya kuchangia katika ukuaji wa sanaa, utamaduni na kuhamasisha mijadala, programu hii imekuwa ikitenga fedha na kufadhili miradi kadhaa ya sanaa toka vikundi mbalimbali kila mwaka.

Kama ilivyokuwa mwaka jana, mwaka huu tena Ubalozi wa Uswisi ulichagua, miongoni mwa maombi mengi, miradi mitano ya sanaa itakayoangazia na kuhamasisha jamii kuhusu janga la mimba za utotoni.

Miongoni mwa vikundi hivi vimo vinavyorekodi nyimbo zenye ujumbe wa kupiga vita mimba za utotoni.

Vilevile vimo vitakavyoshindanisha vipaji vya kuandika nyimbo zenye maudhui ya kuwajengea uwezo wasichana na washindi kupewa nafasi ya kutumbuiza katika majukwaa makubwa na radioni; vitakavyoeneza ujumbe huo huo lakini kwa kutumia sanaa ya katuni jongefu na wanasesere wa kutumbuiza (puppet) na vile vitakavyozunguka mikoa mbalimbali vikiendesha semina pamoja na sanaa mbalimbali za maonyesho.




Wanafunzi wa Sekondari ya Chang’ombe, jijini Dar es Salaam, baada ya kupokea nakala za jarida la Fikiri Mara Mbili. **PICHA ZOTE: MTANDAO**




Wanafunzi wa Sekondari ya Itezi, mkoani Mbeya, baada ya kupokea nakala zao za jarida la Kingo.

**KIWANGO CHA MAFANIKIO YA SANAA**

Ni kwa kiwango gani sanaa hufanikiwa kutimiza makusudi yaliyokusudiwa na waelimishaji ni hoja inayotegemea mambo mengi.

Mwafaka kati ya sanaa iliyochaguliwa na ujumbe uliokusudiwa; mvuto wa sanaa iliyochaguliwa kwa hadhira inayolengwa; umahiri wa msanii na uwezo wa sanaa yenyewe katika kuifikia hadhira kubwa.

Mambo hayo machache ni miongoni mwa vigezo vilivyotumika katika kazi ngumu ya kushindanisha mamia ya miradi inayoomba kufadhiliwa na mfuko huo wa Ubalozi wa Uswisi mwaka huu.

Miongoni mwa miradi mitano iliyochaguliwa na mfuko huu ni mradi wa Fikiri Mara Mbili kupitia jarida la Kingo: Mradi wa jarida la michoro ya katuni, riwaya za kusisimua na mchezo wa igizo la redioni kutoka kampuni ya Gaba Africa.

Walengwa wa moja kwa moja wa ujumbe wa Fikiri Mara Mbili ni wanafunzi wa sekondari, walimu, wazazi na viongozi wa jamii.

> Maelfu ya wanafunzi waliopokea nakala hizi walishauriwa kuwapa majarida hayo wazazi wao mara baada ya kujisomea.

Mchoraji na mwongozaji mkuu wa jarida la Kingo alipoulizwa kwa nini kampuni yake iliamua kuchagua sanaa ya michoro ya katuni (Comics) na igizo la redioni, James Gayo alisema kuwa, michoro ya katuni ina nguvu ya kipekee kwa sababu haimchoshi msomaji kwa maelezo mengi.

Sababu zingine alizotaja ni urahisi wa jarida la katuni kusomwa faraghani na mlengwa bila hofu au aibu ya kuonekana na watu wengine; uwezo wa kusomwa wakati wowote msomaji anapokuwa na nafasi.

Kuhusu mchezo wa kuigiza redioni, Gayo anasema kuwa, Gaba Afrika ilikusudia kutumia sanaa hiyo yenye mvuto kupitia redio za jamii zinazosikilizwa na watu wengi katika miji midogo na vijijini.

Katika simulizi ya Fikiri Mara Mbili, shujaa wa hadithi ni binti mdogo wa kike, Rubi, aliyetokea nchi ya kusadikika hadi kitongoji cha Nangale ambako tatizo la mimba za utotoni lilikuwa ni sugu.

Kabla Rubi hajafanikiwa kutatua tatizo la mimba za utotoni hapo Nangale, anapambana na vikwazo vingi vya kimaslahi kati ya viongozi wababaishaji, wazazi wasiojali majukumu yao na vijana waliokubuhu kwa uharibifu wa mabinti wa shule.

Tamthilia ya Fikiri Mara Mbili, mbali na kuburudisha ina ujumbe mzito kwa viongozi, walimu, wazazi, wavulana na jamii nzima kuhusu umuhimu wa kumwezesha na kumjengea uwezo mtoto.

Jumla ya nakala 10,000 za majarida ya Fikiri Mara Mbili zilichapishwa na kusambazwa kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Mwibara, Natta, Ngokolo, Old Shinyanga, Itiji, Ilezi, Karema, Ilela. Chipukizi, Jangwani, na Chang’ombe katika mikoa ya Katavi, Morogoro, Dodoma, Tabora, Shinyanga, Mara na Dar es Salaam.

Michezo ya redio yenye ujumbe huohuo pia imerushwa katika redio za Mpanda FM, Voice of Tabora FM, Pambazuko FM, Mazingira FM, Boloha FM na Kyela FM za mikoa hiyo hiyo.

Shule na vituo hivi vya redio viko mikoa inayoongoza kitakwimu kwa idadi vya mimba za utotoni.

Gayo anasema kwa kuwa mimba za utotoni ni eneo nyeti lililohitaji, mbali ya kuburudisha na kusisimua, umakini, lugha mwafaka na takwimu sahihi, hivyo iliilazimu Gaba Afrika kuihusisha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika mradi huo kama mshirika wa kiufundi.

Maelfu ya wanafunzi waliopokea nakala hizi walishauriwa kuwapa majarida hayo wazazi wao mara baada ya kujisomea.

Gayo anasema kuwa, utafiti uliopekea utunzi wa hadithi za Fikiri Mara Mbili ulionyesha kuwa, utatuzi wa tatizo la mimba za utotoni utategemea mwitikio wa wazazi, walimu, wavulana, wasichana wenyewe na jamii nzima kwa ujumla.

Ndiyo maana waliazimia Fikiri Mara Mbili imlenge na kusomwa na kila mtu.

“Umekuwa msimu wa kipekee kwetu... hakuna jambo lililotufurahisha kama kuwaona mabinti na wavulana wakifungua kurasa za jarida kwa tabasamu, huku tukijua kuwa walikuwa wanakwenda kukutana na ujumbe muhimu kabisa kuhusu mafanikio yao ya baadaye,” anasema James.

JIELIMISHE



Vyakula vinavyoshauriwa na utafiti watu kuvitumia kwa ajili ya lishe bora. **PICHA: MTANDAO**

# Utafiti wahimiza kula zaidi mboga, matunda kuliko nyama nyekundu

WATAFITI wanasema, binadamu wanatakiwa kula zaidi maharage na dengu na kupunguza ulaji wa nyama nyekundu ili kuilinda dunia na afya zao kwa ujumla.

Katika utafiti uliochapishwa kwenye jarida la sayansi la Lancet, mabadiliko makubwa yanahitajika katika uzalishaji na ulaji wa chakula ili kuepusha vifo vya mamilioni ya watu na kuilinda sayari kutokana na uharibifu.

Kitu muhimu hapa ni kuwa na mabadiliko ya lishe ya dunia na hii inamaanisha kutumia sukari kwa kiwango kidogo na kupunguza ulaji wa nyama nyekundu na badala yake kula kwa wingi mbogamboga, kunde, matunda na njugu, umebainisha utafiti huo.

Watafiti kutoka kamisheni ya EAT-Lancet, wanasema iwapo watu watafuata mpango huo wa lishe, zaidi ya vifo milioni 11 kila mwaka vinavyotokea kabla ya wakati vinaweza kuepukika.

Aidha, hewa chafu ya kaboni huenda ikapungua huku ardhi zaidi, maji na uwepo wa viumbe hai vikahifadhiwa.

**NYAMA KIASI GANI NI AFYA?**

Mpango huo wa lishe bora kwa dunia unaelekeza kila binadamu ale gramu 14 tu ya nyama nyekundu kwa siku, gramu 29 ya vyakula vitokanavyo na kuku, na gramu 13 ya mayai au yai moja na nusu kwa wiki.

Mpango unatokana na utafiti uliofanywa kwa takriban miaka mitatu, ulioanzishwa na kamisheni hiyo ya Lancet, kwa kuwahusisha wataalamu 37 kutoka mataifa 16.

“Tuko katika hali ya janga,” anasema mwandishi mwenza Tim Lang, ambaye ni profesa katika Chuo Kikuu cha Uingereza na kiongozi wa sera wa Kamisheni ya EAT-Lancet iliyofanya utafiti huo.

Lang anasema kulisha idadi inayoongezeka ya watu bilioni 10 ifikapo mwaka 2050, kwa lishe endelevu na ya kiafya haitawezekana bila kubadilisha namna tunavyokula, kuimarisha uzalishaji wa chakula na kupunguza uharibifu wa chakula chenyewe.

Lang anaongeza kuwa chakula tunachokula na namna tunavyokizalisha inategemea pakubwa afya ya watu pamoja na sayari na kwa sasa mambo yanakwenda kombo.

Magonjwa hatari kama vile unene wa kupita kiasi, kisukari na aina tofauti ya saratani, yanahusishwa na lishe mbaya ya chakula.

Watafiti wanasema, lishe kama hizo zinachangia vifo zaidi na magonjwa kuliko hata yale yanayotokana na kufanya ngono bila ya kutumia kinga, unywaji wa pombe, dawa za kulevya na hata uvutaji wa sigara vikichanganywa pamoja.

Lakini mabadiliko hayo ya lishe yataonekana zaidi katika baadhi ya maeneo kuliko mengine.

Kwa mfano watu kutoka Amerika ya Kaskazini, wanakula mara sita na nusu zaidi ya kiwango kinachopendekezwa cha nyama nyekundu, huku watu kutoka Kusini mwa Asia, wakila nusu ya kiwango kilichopendekezwa.

Na wakati huo, utafiti huo unaonyesha kuwa kufikia viwango vinavyopendekezwa vya vyakula vya wanga kama vile viazi na muhogo, kutahitaji mabadiliko makubwa katika kanda ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako kwa wastani watu hula mara saba na nusu ya kiwango kinachopendekezwa.

Walter Willet kutoka Chuo Kikuu cha Harvard, anasema zaidi ya watu milioni 800 hawana chakula cha kutosha, huku watu wengi zaidi wakila chakula kisicho na lishe bora, kinachosababisha vifo vya mapema na magonjwa hatarishi.

Walter anasema kama watu hawawezi kufanikisha mpango wa lishe bora duniani, basi ni vizuri wajaribu kuukaribia.

**DW**

SAYANSI

# Chombo anga za juu chaotesha mbegu za pamba kwenye mwezi

MBEGU ambazo zimepelekwa mwezini na chombo cha utafiti wa anga za juu cha Chang'e-4 cha China zimechipua, mamlaka jijini Beijing, zimethibitisha.

Hii ni mara ya kwanza kwa mmea wa kibaiolojia kuchipuka mwezini na ni hatua inayofungua njia ya utafiti zaidi wa kisayansi.

Chang'e - 4 pia ndio chombo cha kwanza kutafiti sehemu ya mbali zaidi ya mwezi, ambayo haitazamani na uso wa dunia.

Chombo hicho kilitua mwezini Januari 3 mwaka huu, kikiwa kimebeba vifaa vya kuchunguza jiolojia ya eneo hilo.

Mimea imekuwa ikioteshwa kwenye kituo cha kimataifa cha anga za juu, lakini haijawahi kujaribiwa mwezini.

Uwezo wa kuotesha mimea mwezini utakuwa ni sehemu muhimu ya utafiti wa muda mrefu katika sehemu hiyo na pia safari ya kuelekea Mars ambayo inakadiriwa kuchukua miaka miwili na nusu.

Hii inafungua milango ya uwezekano wa wanaanga kuweza kuzalisha chakula chao wenyewe wakiwa anga za mbali na kupunguza uhitaji wa kurudi duniani ili kufuata chakula.

Chombo hicho cha China kilibeba udongo wenye mbegu za pamba, viazi na hamira.

Mimea hiyo imo ndani ya mabakuli yaliyofungwa. Mazao hayo yanatarajiwa kujitengenezea kinga na kujikuza katika mazingira yake yatakayojitengenezea.



Mbegu zikiwa ndani ya Chang'e 4. **PICHA: MTANDAO**

**JE, MWEZI UTAATHIRIKA?**

Swali kuu linaloulizwa ni iwapo jaribio hilo la kuotesha mimea litaleta madhara.

Lakini utafiti huo ambao unafanywa kwa ushirikiano wa vyuo 28 vya China, unalenga kupata taarifa za namna gani viumbe hai vinavyotumia hewa na kuzalisha nguvu ya baianuwai (hasa mimea) vinaweza kukua mwezini.

Mimea hiyo iliyohifadhiwa vizuri imewekewa hewa, maji na virutubisho vingine vitakavyoisaidia kukua.

Changamoto kubwa kwa wanasayansi wa China ni kubadilika kwa hali ya hewa mwezini ambapo huwa baina ya Sentigradi (C) -173 na 100 ama zaidi.

Wanasayansi wengi wanaamini kuwa uwezekano wa kuathiri mwezi ni mdogo kutokana na utafiti huo.

Na pia wanasisitiza kuwa tayari kuna mifuko takribani 100 ya uchafu iliyoachwa na binadamu waliotua mwezini na chombo cha Marekani cha Apollo.

Fred Watson, mwanaanga kutoka Australia ameiambia BBC kuwa kuchipuka huko kwa mbegu ni habari njema.

"Hii inatueleza kuwa yawezekana kusiwe na shida kwa wanaanga kuzalisha chakula chao wenyewe mwezini katika mazingira salama," anasema Watson na kuongeza:

"Kuna umuhimu mkubwa sana katika suala hili, hususani kuutumia mwezi kama kituo cha kurusha vyombo kwenda sayari ya Mars, sababu mwezi upo karibu na dunia."

Profesa Xie Gengxin, ambaye ndiye msanifu mkuu wa utafiti huo amenukuliwa na gazeti moja la China akisema, wanalichukulia kwa umuhimu suala la kuishi anga za juu kwa siku za usoni.

"Kujifunza namna ambayo mimea inakuwa katika nguvu za mvutano wa asili ndogo, kutatuwezesha kuweka msingi wa uwepo wetu wa baadaye kwenye anga za juu," anasema.

Chombo hicho kilichukua siku 20 kutoka duniani mpaka mwezini na kimeshapiga picha 170 ambazo zimetumwa duniani na zinafanyiwa kazi, shirika la habari la Xinhua linaripoti.

**BBC**

JE, WAJUA?

# Alimwa faini kumtuma paka kwa njia ya posta

WAFANYAKAZI wa kituo cha malezi ya wanyama jijini Taipei walipigwa na mshangao baada ya kupokea kifurushi kilichotoka posta kikiwa na paka.

Kutokana na kadhia hiyo, mtu mmoja nchini Taiwan, amepigwa faini baada ya kumsafirisha paka wake kama kifurushi kwa njia ya mawasiliano ya posta.

Kwa mujibu wa mtandao wa habari wa wa UDN, bwana huyo mwenye umri wa miaka 33 aliyetambulika kwa jina lake la ukoo la Yang, amepigwa faini ya dola za Taiwan NT$60,000 ( sawa na dola za Marekani 1,952), kwa kuvunja Sheria ya Ulinzi wa Wanyama ya Taiwan.

Tukio hilo lilitokea wiki iliyopita ambapo Yang alimfungasha kwenye kifurushi paka wake aina ya Scottish fold kwenda kwenye kituo kimoja cha kuhifadhi wanyama nchini humo, katika Wilaya ya Banciao.

Yang amedai kuwa hakuwa na mahitaji tena ya kuendelea kumfuga paka huyo.

Kutokana na kosa hilo, alilipishwa faini ya ziada ya NT$ 30,000 kwa kuvunja sheria ya kuzuia na kupambana na magonjwa ya kuambukiza ya wanyama, kwa sababu wafanyakazi wa kituo cha wanyama alikopelekwa paka huyo waligundua kuwa hakupewa chanjo ya kichaa na hivyo kuzua hasira kali.



Daktari akimchunguza afya paka aliyetumwa kwa njia ya posta, kabla ya kukabidhiwa kwa mmiliki mpya. **PICHA: MTANDAO**

Maofisa wa ulinzi wa wanyama wa jijini Taipei, walifanikiwa kumnasa mtuma kifurushi hicho kupitia kampuni ya posta na mkanda wa kamera za ulinzi za polisi.

Mamlaka ya ulinzi wa wanyama inasema paka huyo ana afya njema na baada ya uchunguzi zaidi, anaweza kuchukuliwa na mmiliki mpya.

Baada ya kufanya uchunguzi wao, wakamtia mikononi mwao Yang ambaye alijitetea kuwa alijaribu kumgawa paka huyo bila ya mafanikio.

Ndugu huyo pia alidai hakuwa na muda wa kutosha wa kumwangalia mnyama huyo na kumtunza.

Paka huyo pia ana matatizo ya kutembea baada ya kujeruhiwa, na licha ya kupatiwa matibabu kadhaa, yakiwamo ya kimila, bado hali yake haijatengemaa.

Mkurugenzi wa mamlaka ya wanyama, Chen Yuan-chuan, amelaani vikali mkasa huo akisema: "Mnyama anaweza kukutwa na hali mbaya kwa kukosa hewa ndani ya kifurushi na kupandwa na ghadhabu, pia hakukuwa na maji safi na salama ya kunywa."

Yuan-chuan amewataka watu kufuata taratibu halali za kisheria pale wanapoona hawawezi tena kuendelea kuwatunza wanyama wao wa nyumbani.

**BBC**

# ELIMU
## NA DK. RAYMOND MGENI



Kuishi maisha yenye furaha inawezekana kwa kufuata njia za kufikia ufanisi na kanuni zake. **PICHA: MTANDAO**

# UCHAMBUZI WA KITABU;
## THE LAW OF ATTRACTION BLUEPRINT by Vardan Dash
### ■ Sheria ya uvutano, njia za ufanisi kufikia malengo na kudhihirisha utele katika maisha yako

DUNIA imezungukwa na utajiri tele kila eneo na vile ambavyo utakavyojitengenezea mazingira bora katika ubora wa mawazo, hisia na hatua unazochukua ndivyo unavyoweza kuvuta utajiri katika maisha yako.

Dunia inaongozwa na kanuni ambazo kwa wanaoweza kuzifuata huwaletea matunda na ambao hawazifuati wanakosa matokeo bora kwa maisha yao.

Moja ya kanuni kubwa mbali na kanuni kama zile kisababishi na matokeo (law of cause and effect) basi kanuni ya uvutano ni kanuni muhimu sana katika safari nzima ya mafanikio.

Sheria ya asili ya uvutano inaonyesha ni kiasi gani kile ambacho ukipatacho katika maisha yako ni matokeo ya mawazo ambayo umekuwa ukifikiria na hisia ambazo umeambatanisha katika fikra zako.

Hivi ndivyo mambo hutokea katika maisha kuwa tunavuta vitu vije katika maisha yetu kwa mawazo ambayo kila siku tunayawaza.

Kumbuka siku ambayo ulivyojenga fikra zako juu ya kufikiri kutokea au kuona kwa kitu kilikuwa. Hii nguvu ya kusababisha kitu kitokee ni nguzo kubwa kuitumia kufikia malengo yetu makubwa ya maisha yetu.

Mawazo haya ni nguvu na hii inadhihirisha kuwa katika ulimwengu karibu kila kitu kimebeba nguvu na nguvu hii huonyesha athari na kudhihirika katika maisha yetu ya kila siku.

Kama kila kitu ni nguvu basi mawazo yako kama ni hasi basi kuna nguvu hasi inaweza kujidhihirisha na kuleta matokeo.

Na vivyo hivyo katika mawazo chanya ni nguvu ambayo inaweza kuvuta mafanikio kama kila siku utakuwa ukiona utele na uchanya katika maisha yako. Vile sumaku huvuta vilivyo vya asili yake ndivyo na mawazo yako huvuta vile utakavyoruhusu uwaze na itakuwa.

Wakati mwingine hatupati kile ambacho tunatamani kupata katika maisha yetu, maana katika mawazo yetu hatujaandaa mawazo chanya ya kuvuta hayo yawe katika uhalisia wetu katika maisha. Sheria ya uvutano ukiiweza kuitumia vizuri basi unaweza kuvuta uhalisia wowote uutakao.

Nguvu ya kupata chochote na kuona sheria ya uvutano ikifanya kazi kwako na maisha yako basi kuna mambo ya kufanya kila siku za maisha yako.


Kuna mambo saba ambayo unapaswa kuyafanya ili uone nguvu ya mvutano ikikuletea maisha ambayo ungependa yawe.

Kwanza, Shukuru kwa kila kitu kizuri kinachoendelea katika maisha yako. Usichukulie kawaida katika mambo ambayo yako vizuri katika maisha yako. Shukuru uwepo wa watu wako wa karibu, afya yako na fursa zote ambazo zinatokea katika maisha yako. Kwa njia ya kushukuru unaruhusu akili yako kuona utele na katika utele ndipo ulipo utajiri.

Lingine ni kwamba sikiliza muziki mzuri kukufanya urudi katika hali nzuri ya fikra zako. Muziki unasaidia kukurudisha katika hali ya utulivu na ukapata hamasa ya kuendelea na safari.

Chagua aina ya muziki ambao unakupa hamasa ya kuchukua hatua na iwe ni sehemu ya maisha yako katika kupata hamasa ya kusonga mbele. Inawezekana katika gari lako au simu janja yako tumia kwa ajili ya kukupa utulivu na katika utulivu kuna ushindi.

> Malengo yako yajengee picha na yafikirie katika picha maana akili hufanyia kazi malengo yakiwa katika picha akilini. Haitoshi tu kuwa na malengo pasipo kuwa na muda wa kuchukua hatua.




Aidha, fanya tahajudi kwa kuwa na utulivu mkubwa na kuifanya akili itulie katika ufanyacho. Tafuta eneo tulivu na kisha ruhusu akili itulie na fikiri kwa kina juu ya maisha.

Fanya hivi asubuhi na jioni huku ukiambatanisha na dua, sala au ombi la shukrani na hekima ya kuyatawala maisha na kukua katika maadili.

Lakini jingine ni kujipa wakati wa kuhisi hisia ambazo unazo sasa zikoje kila upatapo muda wa kufanya hivyo.

Ondoa kulalamika na kuza hisia chanya na maisha yako. Jaribu kuona uzuri katika kila ubaya na katika hali ngumu ona upenyo wa kupita.

Vilevile andika chini kitu gani unataka kwa maisha yako, kiwe wazi na weka mawazo, hisia na chukua hatua kwa kile ulichokiandika. Ikiwezekana jikumbushe kila asubuhi juu ya malengo yako na ndani ya muda utaona kumbe mambo yanawezekana ukijitoa katika nidhamu ya hali ya juu.

Hatimaye, anza kukiri ulichokiandika katika hali chanya kila siku.

Nguvu kubwa katika fikra zako ziko katika akili isotambuzi (subconscious mind) hii huzalishwa na ruhusa ya akili ya utambuzi (conscious).

Hivyo ruhusu mawazo chanya yaingie katika akili yako na yakae katika akili isotambuzi ili uweze kufanikiwa. Kuwa na malengo yaandike chini, na ukiweza mshirikishe unayemwamini na kama ni malengo makubwa yaweke katika mafungu madogo madogo na anza kuyaishi kila siku.

Malengo yako yajengee picha na yafikirie katika picha maana akili hufanyia kazi malengo yakiwa katika picha akilini. Haitoshi tu kuwa na malengo pasipo kuwa na muda wa kuchukua hatua.

Pale unapochukua hatua tu unaruhusu dunia ikutengenezee mazingira ya malengo yako kuwa katika uhalisia. Malengo yako yafanyie kazi na iwe ratiba yako ya kila siku. Kuna nguvu kubwa ya kufanya kila siku kuelekea malengo yako makubwa kwa hatua ndogo ndogo.

**Dk. Raymond Mgeni, Mchambuzi wa vitabu anapatikana kupitia anwani raymondpoet@yahoo.com**



# WADAU SABATO KASIKA

## SERA ya elimu ya mwaka 2014, inaelekeza serikali na wadau wa elimu wakiwamo wananchi kushiriki kutatua changamoto za sekta hiyo na kuleta maendeleo.

Jamii inatambua hilo? Wadau wanajadili.



**DEOGRATIUS MSHEMBA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

LENGO la sera hiyo ni kuhakikisha elimu inayotolewa kwa watoto wa Kitanzania inakuwa bora na yenye kiwango kinachokubalika kimataifa ili kupata Watanzania walioelimika watakaoliwezesha taifa kupata maendeleo na kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Lakini pamoja na kwamba sera hiyo imeonyesha wajibu wa kila mdau kwa ajili ya kuleta mafanikio katika elimu, tatizo moja ni kwamba haijatoa ufafanuzi ni jinsi gani jamii inaweza kufanikisha kile ambacho kimekusudiwa na sera yenyewe.

Hali hiyo inasababisha kuwapo kwa changamoto kubwa, zinazozikabili shule za serikali kwa muda mrefu, hasa kutokana na wananchi kutotambua kuwa shule hizo ni mali zao na wanatakiwa kushiriki katika kuziletea maendeleo.

Baadhi ya migogoro kati ya wananchi na walimu na hata uongozi wa shule imekuwa ikichangiwa na kutokuwapo kwa ufafanuzi wa sera hiyo.

Wapo baadhi ya wananchi, ambao wamekuwa wakigoma kushiriki katika shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya shule wakidai hilo ni jukumu la serikali.

Ni vyema sasa mtindo huo ukaachwa, na hili litawezekana iwapo wananchi watatambua kuwa shule hizo ni zao ili hata wanapotakiwa kushiriki kwa namna moja au nyingine, basi kusiwepo mkwaruzano wowote kati yao na walimu.



**MARY MWITA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NINADHANI kuna tatizo pande tatu, kwa watunga sera, wale wanaopewa kwa ajili ya kuiweka wazi na wananchi. Inawezekana watunga sera wakawa nayo ofisini kwao bila kuisambaza sehemu husika. Hili ni tatizo.

Au inawezekana wamesambaza lakini wanaotakiwa kuuelimisha umma wakakaa kimya.

Pia inawezekana wananchi wakawa wanaijua sera hiyo, lakini hawataki kushiriki katika shughuli za maendeleo ya shule.

Hivyo kila upande uangalie ni wapi umejikwaa katika kuhakikisha sera inatekelezwa inavyotakiwa.

Lakini niongozee kuwa tabia yetu Watanzania ni kutozingatia mambo hata kama tunayajua na tumekuwa watu wa kulalamika tu hata pale pasipostahili kufanya hivyo.

Kwa mfano baadhi ya wazazi wamekuwa wakikataa kuchangia hata unga, maharage au chakula kwa ajili ya kusaidia watoto wao kupata angalau mlo wa mchana wawapo shule.

Wakiulizwa wanajibu kuwa serikali imetangaza kwamba elimu ni bure. Wanajibu hivyo kuangalia au kujua hali halisi ambayo watoto wao wamekuwa wakikumbana nayo shuleni.

Hebu fikiria mtoto anatembea umbali wa kilometa 10 kwenda shuleni halafu anashinda bila kula! Hivi kweli masomo yatamwingia? Mzazi akiambiwa kuchangia japo chakula anang'aka eti serikali imesema elimu ni bure.



**DANIEL NACKSON (MHITIMU WA CHUO CHA UALIMU)**

MENDELEO ya shule na ya wanafunzi yanachangiwa na ushiriki wa wazazi na walezi kwa kuchangia mahitaji mbalimbali ya shule kutegemea kile walichoombwa kuchangia, na pia wanatakiwa kufuatilia maendeleo ya watoto wao, siyo kuacha jukumu hilo kwa walimu tu.

Kumekuwa na malalamiko mengi yakiwamo ya wazazi kwamba wanachangishwa michango wakati ilishazuiwa na pia walimu wanalalamika kwamba baadhi ya wazazi hawafuatilii maendeleo ya watoto wao.

Ninachofahamu ni kuwa, majukumu walionayo wazazi na walezi siyo tu kupeleka watoto wao shule bali pia wanawajibika kufuatilia maendeleo yao na wana wajibu wa kuchangia michango ya maendeleo yao.

Wazazi wasitafute nafasi za watoto kwa ajili ya kusoma tu bali wajue kuwa wanatakiwa kuhusika kikamilifu katika maendeleo ya shule wakitambua kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Ushirikishwaji katika maendeleo ni jambo la msingi sana, hivyo kila mzazi atambue kuwa ana wajibu wa kushirikiana na serikali kwa ajili ya maendeleo ya shule anayosoma mtoto wake.

Cha msingi ni kuacha mtindo wa kulalamika hata pale ambapo ni wajibu wao kuchangia kwa hali na mali kwa ajili ya maendeleo ya shule.



**MICKIDADI MCHILLAH (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA mtazamo wangu ni kwamba sera hii ni nzuri na inahimiza dhana ya umoja ni nguvu, kwa kuwa bila kuunganisha nguvu katika shughuli zozote, siyo rahisi kufikia mafanikio.

Bahati mbaya sijawahi kuisoma, lakini kama ndivyo inavyoelekeza, basi inafaa na inabidi nakala zake zisambazwe kwa wananchi ili waijue, kwa sababu baadhi yetu tumekuwa ni wagumu kushiriki katika shughuli za maendeleo, huku tukiwa na visingizio vingi ambavyo si vya msingi.


Siyo rahisi serikali kutufanyia kila kitu kwa ajili ya maendeleo ya watoto wetu, bali na sisi tunatakiwa pia kuchangia nguvu zetu. Kwa mfano serikali imeondoa ada kwa shule za msingi hadi kidato cha nne.

Hapa maana yake ni kwamba mambo mengine kwa ajili ya maendeleo ya shule zetu tunatakiwa kushiriki kulingana na jinsi tunavyokubaliana.

Lakini tukisema ni jukumu la serikali kutufanyia kila kitu, hapo ninaona tutakuwa tunaionea bure.

Hivi hata choo kikibomoka tusubiri serikali ijenge wakati uwezekano wa kufanya kazi hiyo tunao? Je, hata mchango kidogo ili watoto wetu wapate angalau uji shuleni tunasubiri serikali itufanyie?

Tufanye sehemu yetu, kwa sababu tunahusika kwa asilimia kubwa katika maendeleo ya shule zetu.



**RODA DANIEL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SUALA la ushiriki wa wananchi katika maendeleo ya shule limekuwa likiingiliwa na wanasiasa na kuwashawishi wasishiriki shughuli za maendeleo ya shule.

Kwa sababu wapo baadhi yao ambao wamekuwa wakihamasisha wananchi wagome kuchangia maendeleo ya shule kwenye maeneo yao, kwa madai ni jukumu la serikali.

Hili limekuwa kama jambo la kawaida kwenye baadhi ya maeneo hapa nchini na tumekuwa tukiyasikia kupitia vyombo vya habari.

Wakati mwingine unaweza kukuta viongozi na wajumbe wa kamati za shule ni wanasiasa na hivyo si ajabu kukuta vikao vikijadili au wajumbe wakipingana kutokana na itikadi za kisiasa badala ya kujadili maendeleo ya shule.

Kwa hali kama hiyo ni vigumu kuzingatia maelekezo ya sera, ambayo inaitaka serikali, wadau mbalimbali na wananchi kushiriki katika maendeleo ya shule.

Ombi langu ni kwamba wanasiasa waache kukwamisha maendeleo ya shule kwa maslahi yao ya kisiasa, watambue kuwa mtindo huo una madhara makubwa kwa maendeleo ya shule na elimu kwa ujumla.

# Takukuru wamtuhumu kwa rushwa ya Sh.500,000

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mbeya, imemfikisha mahakamani mtumishi wa Wakala wa Barabara (Tanroads) mkoani hapa, Zabron Kenan, kwa tuhuma za kupokea rushwa ya Sh. 597,000.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Emmanuel Kiyabo, alipokuwa anatoa taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo katika kipindi cha robo mwaka ya kuanzia Oktoba hadi Desemba.

Mhandisi Kiyabo, alisema mtaalamu huyo wa Tanroads alikuwa msimamizi wa kituo cha mizani cha Uyole jijini Mbeya, lakini akawa anapokea rushwa kwa madereva wenye mizigo iliyozidi.

Alisema mtaalamu huyo alipokea rushwa hiyo kutoka kwa dereva wa Kampuni ya Kichina ya Chongqing Foreign Trade Economic Corporation, Onesphory Ngonyani, ambaye alikuwa anaendesha gari aina ya Howo yenye namba za usajili T. 755 BZC na tela lenye namba za usajili T. 587 BPY.

**Mpokeaji wa fedha hizo Kenani tulimkamata na kumfikisha mahakamani na kumfungulia kesi ya jinai namba CC. 189/2018 chini ya kifungu cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.**

Alidai kuwa dereva huyo alikuwa anaendesha gari hilo likiwa limebeba mzigo wenye upana usiokuwa wa kawaida (Abnormal Wide Load) bila kuwa na kibali na hivyo hakutakiwa kuwa barabarani kwa mujibu wa sheria.

Mhandisi Kiyabo alisema kutokana na gari hiyo kutokuwa na kibali, alipofika katika kituo cha mizani cha Uyole alimpatia rushwa Kenani ili na kuendelea na safari wakati huo Takukuru ikiwa imeweka mitego yake.

"Mpokeaji wa fedha hizo Kenani tulimkamata na kumfikisha mahakamani na kumfungulia kesi ya jinai namba CC. 189/2018 chini ya kifungu cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007," alisema Mhandisi Kiyabo.

Hata hivyo alieleza kuwa mtoa rushwa ambaye ni Ngonyani, alikimbia na kutokomea kusikojulikana baada ya kubaini kuwa anafuatiliwa na maofisa wa Takukuru.

Alisema maofisa wa taasisi hiyo wamekuwa wakimfuatilia dereva huyo ili wamkamate, lakini kila akiwaona anachoropoka na kutokomea na kwamba hivi karibuni walimkuta maeneo ya Uyole na wakaweka mtego wa kumkamata akakimbia na kitokomea na kutelekeza gari yake aliyokuwa anatembelea.

Kiyabo alisema baada ya Ngonyani kutelekeza gari hiyo aina ya Toyota Carina yenye namba za usajili T. 108 BQH maofisa wa Takukuru waliivuta na kuipeleka kwenye ofisi za taasisi hizo na hivyo wanamtaka ajisalimishe ili achukuwe gari yake.

"Tumebaini kuwa gari hii aliinunua kutoka kwa mwananchi mmoja wa Dar es Salaam na bado hajabadilisha umiliki wake, hivyo kuna fedha ya serikali inatakiwa kulipwa kama ada ya kuhamisha umiliki, endapo ataendelea kujificha tutafuata taratibu za kisheria na mapato yake yaingie serikalini kwa maslahi ya Watanzania," alisema Mhandisi Kiyabo.

Pia alisema katika kipindi hicho kesi tatu zilikuwa zimefunguliwa na taasisi hiyo zilitolewa hukumu na kwamba walishinda kesi moja na zingine mbili walishindwa na hivyo wahusika kuachiwa huru na kwamba wanakusudia kukata hukumu mahakamani.



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Nape Nnauye (kulia), akiteta jambo na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, katika kikao na wadau wa misitu kilichofanyika wilayani Mufindi mkoani Iringa jana. **PICHA: WMU**

# Waongoza watalii wakiri kuzidiwa kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAONGOZA watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo iliyopo wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe, wameomba watu wengine wenye taaluma hiyo kujitokeza katika hifadhi hiyo ili kuongeza nguvu kwa madai kuwa idadi yao haiendani na ongezeko la watalii.

Akizungumza na Nipashe juzi, kiongozi wa waongoza watalii hao, Japhari Ngogo, alisema hifadhi hiyo kwa sasa imeanza kuboresha vivutio vya utalii na hivyo kuwa na uwezekano mkubwa wa ongezeko la watalii ambao hawatoendana na idadi ya waongozaji. Alisema waongoza watalii katika hifadhi hiyo wameanzisha chama ambacho kina wanachama 10 pekee, huku baadhi ya wanachama hao wakiwa na majukumu mengine tofauti na hilo la kuongoza watalii.

Ngogo alisema kutokana na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kuboresha hifadhi hiyo kwa kuanza kurejesha wanyama waliokuwa wametoweka wakiwamo pundamilia kuna uwezekano wa watalii kuongezeka, hivyo hata wao wanatakiwa koboresha huduma yao.

"Wenzetu wanapoboresha huduma zao hata sisi tunatakiwa kuboresha huduma zetu, sasa wameleta wanyama na kuna uwezekano wa kuongezeka watalii, hivyo hata sisi tunatakiwa tuongezeke idadi ili tuendane na ongezeko la watalii hao," alisema Ngogo. Alisema mwaka jana walipokea makundi ya watalii 501, lakini kutokana na waongoza watalii kuwa wachache, yeye ndiye aliongoza watalii kati ya 350 na 400.

Hivi karibuni Tanapa kwa kushirikiana na Shirika la Wanyamapori (WCS), walirejesha pundamilia katika hifadhi hiyo ambao inadaiwa waliwahi kuwapo miaka 50 iliyopita, huku wakiahidi kuendelea kuleta wanyama wengine wadogo wadogo kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

Hata hivyo uongozi wa hifadhi hiyo ulitoa tathmini ukidai kuwa unatarajia idadi ya watalii kuongezeka kwa zaidi ya mara mbili kwa madai kuwa wengi waliokuwa wanaenda kutalii walikuwa wanaenda kuangalia maua ya asili, ndege na vivutio vingine vidogo vidogo.

# Tamisemi yakerwa wanasiasa kushusha walimu vyeo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKURUGENZI wa Halmashauri zote nchini wameagizwa kuwasimamia walimu kutekeleza vema majukumu yao badala ya kusubiri wanasiasa kuwashusha vyeo walimu wakuu na wakuu wa shule zao zinapopata matokeo mabaya kwenye mitihani ya kitaifa.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini Mbeya na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Tixon Nzunda, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya kuinua ubora wa elimu ambayo yanashirikisha wakurugenzi na maofisa elimu kutoka wilaya zote za mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

Nzunda alisema kuwa wakurugenzi wengi wamekuwa wakitumia muda mwingi kukaa maofisini bila kuwasaidia walimu kufanikisha majukumu yao na baadaye wanaungana na wanasiasa kuwafukuza ama kuwashusha vyeo walimu wakuu inapotokea shule zao zimepata matokeo mabaya.

"Kuanzia sasa mkurugenzi unatakiwa kushiriki moja kwa moja kutatua changamoto za walimu na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa majukumu yao na sio kukaa ofisini kisha baadaye unaungana na wanasiasa kuwavua vyeo walimu wanaopata matokeo mabaya," alisema Nzunda.

Alisema kuwa miongoni mwa changamoto ambazo zinatakiwa kushughulikiwa moja kwa moja na wakurugenzi ni pamoja na kutoa fedha na kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa, kushughulikia kero za walimu ikiwamo upatikanaji wa vitendea kazi, maslahi yao na kusimamia ubora wa taaluma inayotolewa.

Nzunda alisema kuwa kuanzia sasa ni marufuku kumsimamisha kazi au kumvua cheo mwalimu mkuu kwa sababu ya shule kupata matokeo mabaya kwenye mitihani ya kitaifa.

Badala yake aliwataka wakurugenzi na maofisa elimu wa maeneo husika kushirikiana na walimu kushughulikia kero kwenye sekta ya elimu na sio kunyoosheana vidole.

Aidha, Nzunda alisema kuwa serikali inakusudia kuelekeza fedha nyingi kwenye uboreshaji wa miundombinu ya elimu na afya, hivyo akawataka wakurugenzi kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema kutokana na uamuzi huo, utendaji wa wakurugenzi utaanza kupimwa kwa vigezo vya michango yao katika usimamizi wa sekta za elimu na afya kwenye maeneo yao.

Alisema katika sekta ya elimu, wakurugenzi wanalo jukumu la kusimamia ubora wa taaluma ikiwa ni pamoja na kuhakikisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wa shule za msingi.





# Askofu atabiri neema wanaofanya kazi kwa bidii

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Mlima wa Moto, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kati, Silvanus Komba, amesema mwaka huu ni wa mafanikio kwa wale ambao wanafanya kazi kwa bidii na siyo kwa wavivu.

Akihubiri katika ibada ya Jumapili katika kanisa hilo, lililoko Sabasaba jijini hapa, askofu huyo alisema mwaka huu viongozi wa dini wanatakiwa kuwahubiria Watanzania ukweli na siyo kwa maneno ya kuigizi ili watambua umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii badala ya kuilalamikia serikali.

"Wapo watu ambao wamemaliza vyuo vikuu, lakini kutokana na uzembe na uvivu wamekuwa wakitembea na vyeti wakitafuta ajira badala ya kutumia elimu yao kujiajiri wakati wakisubiri ajira," alisema Askofu Komba.

**Hakuna mtu ambaye anaweza kukuona katika dimbwi la umaskini kama mtu hata weza kufanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa na kwa ustadi wa kazi.**

Aidha, alisema utendaji wa serikali ya awamu ya tano katika kupambana na rushwa pamoja na masuala ya uonevu imefanikisha na kila Mtanzania sasa anafanya kazi kwa uaminifu.

"Nataka niwaambie waumini wangu hata kama mtalala kanisani kwa kuomba mafanikio, lakini kama hakuna juhudi ya kufanya kazi hakuna baraka ambazo zinaweza kuwa juu yako," alisema.

Aliongeza kuwa "Katika maandiko matakatifu yanaeleza kuwa mtu asiyefanya kazi na asile, lakini inaenda mbali zaidi kuwa utabarikiwa mashambani na mjini na mwingiapo na mtokapo kwa maana nyingine ni lazima ufanye kazi."

Aliwaasa viongozi wa dini kuhakikisha wanawafundisha waumini wao juu ya kufanya kazi kwa bidii badala ya kufundisha masomo ya utoaji na ya yale ya kuigiza.

Alisema kuwa hapendezwi kuona waumini wa kanisani wakiendelea kulalamika kwa madai kuwa maisha ni magumu wakati kufanya kazi hawataki.

"Hakuna mtu ambaye anaweza kukuona katika dimbwi la umaskini kama mtu hata weza kufanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa na kwa ustadi wa kazi," alisema.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga (kushoto), akimpongeza Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (sekta ya ujenzi), Arch. Elius Mwakalinga, baada ya kumkabidhi ofisi hiyo jijini Dodoma jana. **PICHA: WUUM**

# Wizara yajiandaa kuboresha mifugo

**Na Oscar Mirindo,** SINGIDA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeandaa mikakati ya kuboresha sekta ya mifugo ikiwamo kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Hayo yalielezwa jana wilayani Singida na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, katika zoezi la uhamasishaji wa uogeshaji wa ng'ombe kwenye majosho kanda ya kati.

Alisema hivi sasa serikali inaendelea kuboresha sekta hiyo kwa kuhakikisha kuwa dawa katika majosho yote nchini zinapatikana kwa wakati.

Alisema kwa sasa serikali imeondoa tozo za uogeshaji wa mifugo ili wafugaji waweze kuogesha mifugo yao kwa wingi.

"Hivi karibuni kulikuwa na changamoto zilikuwa zikirudisha nyuma wafugaji na kushindwa kuwafikisha mifugo yao kwenye majosho kutokana na uhaba wa dawa na uchakavu wa majosho," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imepunguza tozo ambapo kwa ng'ombe mmoja anatozwa Sh. 50, kwa mbuzi ni Sh. 20.

Aliwataka wafugaji kutumia fursa hiyo kuogesha mifugo yao na kuondokana na

# CCM yakagua miradi ya maendeleo

**Na Augusta Njoji,** BAHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), mkoani Dodoma, kimefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo, huku kikiagiza usimamizi wa karibu ujenzi wa kituo cha afya cha Chifutuka wilayani Bahi ili kikamilike kwa wakati.

Akizungumza katika ziara hiyo jana akiwa ameambatana na kamati ya siasa ya Mkoa, Mwenyekiti wa CCM mkoani humo, Godwin Mkanwa, alisema kituo hicho kinatakiwa kukamilika kwa wakati ili kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Aidha, alisema ukamilikaji wa kituo hicho uende sambamba na uwepo wa miundombinu ya umeme na maji.

"Nikiangalia siku zilizobaki ni chache ukilinganisha na hatua iliyopo, sasa jicho lako liwe hapa Mkuu wa Wilaya vifaa vifike kwa wakati, mafundi washinde hapa kazi ifanyike na kukamilika kwa muda uliowekwa katika makubaliano yenu," alisema mwenyekiti huyo.

Alilitaka Shirika la Umeme nchini (Tanesco) Mkoa wa Dodoma, kufikisha miundombinu ya umeme kwa wakati ili kituo kitakapokamilika na umeme uwepo.

Mkanwa aliwahamasisha wananchi kujikita katika kilimo cha korosho, ili wajiinue kiuchumi na kuufanya mkoa kuwa kijani kama dhamira ya Makamu wa Rais, Samiah Suluhu Hassan alivyoagiza.

"Wananchi pandeni miche ya mkorosho inafaida kiuchumi, lakini pia inasaidia kutunza mazingira yetu, tunahamasisha pia mpande angalau mti mmoja wa matunda kila kaya," alisema Mkanwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya hiyo Mwanahamisi Mukunda, aliwasisitiza mafundi wanaojenga kituo hicho kukamilisha ujenzi kwa muda uliopangwa vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Hapa mwenyekiti tumekubaliana na mafundi kuwa Februari 2 wanatukabidhi mradi huu ukiwa umekamilika, sasa niwasisitize tu watekeleze makubaliano yetu la sivyo nitawaweka ndani na hatutawapa tena kazi katika wilaya hii," alisisitiza Mukunda.

Aliwataka viongozi katika ngazi zote katika wilaya hiyo kuwa na usimamizi shirikishi, ili kuwezesha mradi huo kukamilika kwa muda uliowekwa.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Leo Mavika, alisema ujenzi huo ulianza Julai 2 mwaka jana na ulikuwa ukamilike Novemba 30 mwaka jana, lakini kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo kusitishwa kwa muda mfumo wa malipo na mafundi kutokukaa eneo la mradi kumesababisha kutokamilika kwa wakati.





# Mwakilishi ajitwisha zigo ujenzi wa shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Donge, Dk. Khalid Salum Muhammed, ameahidi kumalizia ujenzi wa Shule ya Babuso iliyoko Donge Chechele Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa muda wa wiki mbili kuanzia sasa ili kuwaondolea usumbufu wanaoupata watoto katika kufuata elimu masafa marefu.

Alisema wananchi kupitia mfuko wa maendeleo wa diwani wameanzisha ujenzi wa shule hiyo, ili kuwaondolea usumbufu watoto kufuata elimu na kwamba atahakikisha anaunga mkono juhudi hizo ili shule hiyo iweze kumalizika.

Dk. Khalid aliyasema hayo eneo la Donge Chechele alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji hicho kuhusiana na masuala ya maendeleo.

Alisema kitendo cha kufuata shule kwa zaidi ya umbali wa maili mbili kunaweza kusababisha kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji wakati wakienda au kurudi shule.

"Watoto wanahitaji ulinzi, hivyo kutembea masafa mazuri bila ya ulinzi, wahalifu wanaweza kutumia mwanya huo kuwadhalilisha," alisema.

Aliwataka wazazi na jamii kwa ujumla kuendeleza uzalendo kwa kujitokeza kufanya kazi za kujitolea wakati wa kumalizia ujenzi wa shule hiyo ili kumalizika muda mwafaka.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kaskazini B, Unguja, Subira Muhamed Ameir, alisema viongozi wa Jimbo la Donge tayari umeshatekeleza Ilani ya CCM katika sekta ya elimu, afya, umeme, barabara, kilimo na vikundi vya kinamama jambo ambalo limesababisha wananchi kuzidi kujenga imani na viongozi hao.

Aidha, alisema mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano mzuri unaoonyeshwa na wananchi kwa viongozi wao na kuwaomba kutokubali kurubuniwa na wanasiasa wasiopenda maendeleo ya nchi.

# Waliokwenda nje ya nchi kufanya kazi salama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

**Vijana hao wameenda katika nchi za Qatar, Dubai na Oman, ambapo mara ya mwisho walisafiri mwezi Desemba mwaka jana.**

MKURUGENZI wa Idara ya Ajira kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Ali Suleiman Amir, amesema vijana 673 walioenda kufanyakazi nje ya nchi wapo salama na wanaendelea kufanya kazi.

Alisema idadi ya vijana hao waliosafiri kwenda kufanya kazi ni kwa kipindi cha miezi sita kati ya Julai na Desemba mwaka jana.

Aliyasema hayo alipokuwa akijibu hoja za wajumbe wa Kamati ya Maendeleo, Habari, Utalii, Utamaduni na Wanawake na Watoto ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema kuwa vijana hao wameenda katika nchi za Qatar, Dubai na Oman, ambapo mara ya mwisho walisafiri mwezi Desemba mwaka jana.

Alifafanua kwamba vijana hao wamekuwa wakisafiri kwa kazi tofauti, ambapo kuwa waliokwenda kwa kazi za udereva, kazi za ndani na wauza bidhaa.

Aidha, alisema kuwa wafanyakazi hao husafirishwa kupitia wizara yao na vigezo vinavyotumika ni baada ya kukubaliana na waajiri wao.

Alisema kwamba wao jukumu lao kubwa ambalo wanalifanya ni kuhakikisha wanaenda na wanakuwa salama wakati wowote, lakini kuhusu vigezo ni makubaliano baina yao na waajiri wao.

Alisema kuwa tangu kuanza kazi hiyo ya kusafirisha vijana hao hakuna tatizo hata moja lililojitokeza na mara nyingi wale wanaopata matatizo ni wale ambao wameenda bila ya kupitia kwao.

Alitoa wito kwa vijana ambao wanaenda kufanyakazi nje ya nchi kufuata taratibu na kuacha tabia ya kuondoka kwa njia za panya kwa kuwa wanapopata matatizo huwa vigumu kupatiwa ufumbuzi wa haraka.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akikagua madarasa ya Shule ya Msingi Jomu mjini Shinyanga, ambayo yameweka nyufa na kuhatarisha maisha ya wanafunzi shuleni hapo. Katikati ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Sarah Maloda. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Baraza la Vijana lakabiliwa uhaba vitendea kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Vijana Zanzibar linakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na nyenzo za kutendea kazi katika shughuli za uzalishaji mali kwa mabaraza yao.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Khamis Faraji, aliyasema hayo alipokuwa akitoa ripoti ya utekelezaji wa baraza hilo mbele ya Kamati ya Maendeleo, Utalii, Utamaduni, Habari na Wanawake ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema pia baraza halijapatiwa fedha zilizotengwa na serikali Shilingi bilioni tatu za mradi wa ajira kwa vijana jambo ambalo limesababisha baraza hilo kuwa katika wakati mgumu.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilitenga jumla ya Sh. milioni 130 kwa Baraza la Vijana Zanzibar, ikiwa na lengo la kufanya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Alisema baraza hilo kwa mwaka huo wa fedha limetekeleza shughuli mbalimbali ikiwamo kushiriki katika maadhimisho ya kitaifa na kimataifa, kufanya mikutano ya baraza la watendaji, kufanya mkutano mkuu wa baraza la vijana taifa, ziara ya kutembelea na kuyasimamia mabaraza ya vijana Zanzibar pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua vifaa na kutoa mafunzo ili kukuza ufanisi.

Aidha, alisema pia wamepata mafanikio ikiwamo kukuza uelewa kwa vijana ya kuwa wazalendo katika nchi yao kupitia makongamano mbalimbali, kama kumbukumbu ya kumuenzi Baba wa Taifa, kongamano la Siku ya Kimataifa ya Vijana.

Alisema baraza hilo limeweza kuyaunganisha mabaraza ya vijana na wadau mbalimbali wa maendeleo pamoja na wadau mbalimbali wa kimataifa katika kusaidia kutatua changamoto ya ajira kwa vijana wa Zanzibar.

Kwa upande wao wajumbe wa mabaraza ya vijana walisema kuwa wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo, ofisi kwa ajili ya kufanyia shughuli zao ikiwamo kujadili masuala yao, pamoja na kutafutiwa ajira kwa vijana kwa kuwa sasa imekuwa ni kilio kikubwa kwa vijana.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Khamis Mbaraka, alisema kuwa wakati umefika kwa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kukaa pamoja na vijana ili kuweza kutatua changamoto zinazowakabili ili lengo liweze kufikiwa kwa wakati uliopangwa.

Aidha, aliishauri wizara hiyo kuwa na mawasiliano ya Wizara ya Wanawake na Watoto kwa kujadili masuala ya ajira kwa vijana ili waweze kuajiriwa.

Aliwataka vijana kuondoa dhana ya kuajiriwa serikalini na badala yake watumie fursa zinazotolewa na serikali kwa kuweza kijiajiri wao mwenyewe bila ya kutegemea ajira serikalini.

HABARI KIMATAIFA

# Washukiwa ugaidi Kenya wajisalimisha

**NAIROBI,** Kenya

JESHI la Kenya limewakamata watu wanaodaiwa kuhusika na shambulio la kigaidi katika eneo la Riverside mjini Nairobi.

Taarifa zaidi kutoka Kenya zinaeleza kuwa watu hao walijisalimisha katika kituo kimoja cha polisi mjini Isiolo, Kaskazini mwa mji mkuu wa Nairobi.

Wakati huo huo, vikosi vya usalama nchini Kenya vinasema kuwa vimetibua shambulio la kigaidi lililotaka kutekelezwa katika eneo la Kaskazini Mashariki mwa mji wa Nairobi karibu na mpaka na Somalia.

Mamlaka ya usalama nchini Kenya inasema kuwa wapiganaji hao walikuwa wamelenga kutekeleza shambulio katika kampuni mbili za ujenzi mjini Garissa.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa maofisa wa jeshi wakishirikiana na wale polisi walijibu shambulio hilo na kufanikiwa kuwaua takribani wapiganaji wanne.

Hakuna ofisa hata na hata wafanyakazi wa ujenzi huo walioripotiwa kuuawa.

Kenya inaendelea kukabiliana na matokeo ya shambulio katika hoteli, ambapo takribani watu 21 waliuawa. Kundi la Al-Shabab kutoka Somalia limekiri kutekeleza shambulio hilo.

Hadi sasa watu kadhaa wamekamatwa kuhusiana na shambulio hilo na maofisa wa polisi wamechapisha picha za watu wengine wanane wanaosakwa.

Wakati huohuo, wazazi wa watu watatu waliojisalimisha katika kituo cha polisi cha kaunti ya Isiolo wamesema kuwa watoto wao hawana hatia.

Lakini licha ya kujisalimisha, wazazi wa washukiwa hao bado wanahoji wakitaka kujua kwa nini majina ya watoto wao yalikuwa katika orodha hiyo ya magaidi wanaosakwa na serikali ya Kenya.

Wazazi hao kutoka eneo la Tulloroba mjini Isiolo waliwasilisha malalamishi yao kwa Naibu Kamishna wa kaunti hiyo kufuatia kutolewa kwa orodha hiyo na shirika la huduma za polisi.

Wazazi hao walieleza kuwa walishangazwa wakati walipoona majina ya watoto wao katika vyombo vya habari siku ya Jumapili usiku licha ya kwamba wamekuwa tayari kuwawasilisha kwa mkurugenzi wa kitengo cha jinai pamoja na kitengo kinachokabiliana na ugaidi kuhojiwa.

Baba mmoja wa watuhumiwa hao, Abdi Bidu, alielezea kuwa watoto wao walijaribu kuvuka kuelekea nchini Somalia 2017, lakini wakakamatwa.

Wazazi hao walieleza kuwa watoto wao kwa sasa ni wahudumu wa bodaboda katika mji wa Isiolo na kwamba wamebadilika kitabia.

Ndugu mmoja wa washukiwa hao, Hussein Wario, aliitaka serikali kuwahakikishia usalama watoto wao, huku akisema ndugu yao alikamatwa akitazama soka katika ukumbi mmoja miaka mitatu iliyopita.

**BBC**



Jeshi la Polisi mjini Harare likikabiliana na waandamanaji. **PICHA: AFP**

# Mnangagwa akatisha ziara baada ya maandamano

**HARARE,** Zimbabwe

RAIS wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, amesitisha ziara Ulaya alikotakiwa kuhudhuria jukwaa la kimataifa la kiuchumi, baada ya nchi yake kukumbwa na maandamano ya umma. Katika maandamano hayo inaelezwa kuwa watu zaidi ya 10 wameuawa.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter, Rais Mnangagwa, alisema anarejea nyumbani kutokana na hali ya kiuchumi iliyoko nchini mwake na jambo atakalolipa kipaumbele ni kuifanya Zimbabwe kuwa tulivu, thabiti na kufanya kazi tena.

Rais Mnangagwa ameonekana kuwa na mtizamo wa maridhiano ulio tofauti na ule wa msemaji wake, George Charamba, ambaye amesema msako dhidi ya waandamanaji ni kionjo cha yale yanayokuja, huku kukiwa na madai ya kukamatwa kwa nguvu kwa viongozi wa upinzani, wanaharakati na raia.

Shirika lisilo la serikali la kutetea haki za binadamu limesema watu wasiopungua 12 wameuawa na 78 wamejeruhiwa na risasi katika kipindi cha wiki moja.

Umoja wa Mataifa (UN) umeishutumu serikali ya Zimbabwe kwa namna ilivyoshughulikia maandamano hayo ya umma yaliyoanza Januari 14, mwaka huu.

Mnangagwa amekuwa akishinikizwa kurejea nchini Zimbabwe kutoka ziara ya wiki mbili aliyokuwa anafanya katika nchi za magharibi, baada ya kuibuka ripoti kuwa vikosi vya usalama vimetumia nguvu kubwa dhidi ya waandamanaji waliokuwa wanapinga kuongezeka zaidi kwa bei ya mafuta.

Wiki iliyopita, maelfu ya watu nchini Zimbabwe waliandamana kupinga kuongezeka kwa bei ya mafuta kwa zaidi ya asilimia 100, inayotajwa kuwa bei ya juu zaidi ya mafuta duniani.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini Zimbabwe, Charity Charamba, amewashutumu wahalifu kwa ghasia zilizojiri katika maandamano.

Rais Mnangagwa akiwa katika jukwaa la kimataifa la kiuchumi la Davos alitarajia kuomba uwekezaji wa kigeni na mikopo kuisaidia nchi yake kujikwamua kiuchumi na kifedha.

**DW**

# Walinda amani wauawa katika shambulio Mali

**BAMAKO,** Mali

ASKARI 10 wa Umoja wa Mataifa (UN), kutoka nchi ya Chad wameuawa, huku wengine 25 wakijeruhiwa katika shambulio lililotokea katika eneo la Aguelhok, Kaskazini Mashariki mwa Mali.

Shambulio hilo limetokea umbali wa kilometa 250 kutoka Kaskazini mwa mji wa Kidal, huku kundi la kijihadi la Aqmi, lenye mfungamano na kundi la Al-Qaeda limekiri kuhusika na shambulio hilo.

Shambulio hilo limetokea wakati ambao nchi ya Ufaransa ikitangaza kuanza kwa operesheni za kikosi cha kimataifa kutoka nchi za ukanda wa Sahel (G5 Sahel).

"Walinda amani 10 kutoka Chad wameuawa na wengine zaidi ya 25 wamejeruhiwa," alisema Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres.

Ripoti ya awali iliyotolewa na UN ilieleza kuwa walinda amani wanane waliuawa katika shambulio hilo.

Kundi la wanamgambo wa Kiislamu la Aqmi lenye mafungamano na Al-Qaeda limekiri kuhusika na shambulio hilo, likieleza kuwa limefanya hivyo katika hatua ya kupinga ziara ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu nchini Chad siku ya Jumapili.

Mapema Alfajiri, kikosi cha askari wa Umoja wa Mataifa kutoka Chad waliopiga kambi katika eneo la Aguelhok, kilomita 200 kutoka kwenye mpaka wa Algeria walizima shambulio lililozinduliwa na wauaji waliowasili kwenye magari mengi, huku wakijihami kwa silaha za kivita.

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Mali ulieleza kuwa wauaji wengi waliuawa katika shambulio hilo hata Umoja wa Mataifa ulipoteza askari wake kadhaa.

Kikosi cha Umoja wa Mataifa nchini Mali ambacho kinasimamia amani nchini humo tangu mwaka 2013, baada ya eneo la kaskazini mwa nchi hiyo kuanguka chini ya udhibiti wa kundi la kijihadi lenye mafungamano na al-Qaeda, Minusma, ambayo ina askari na polisi 12,500, tayari imepoteza walinda amani zaidi ya 160.

Inaelezwa kuwa shambulio hilo ni baya zaidi kuwahi kukikumba kikosi cha Umoja wa Mataifa nchini humo.

**RFI**

# FAO, Tanzania kushirikiana kuboresha usalama chakula

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), imezindua mradi maalum unaolenga kuboresha Mfumo wa Uchambuzi wa Masuala ya Usalama wa Chakula na Lishe nchini (MUCHALI).

Uzinduzi wa mradi huu ulifanyika jijini Dodoma, ambapo mgeni rasmi alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Maafa - Ofisi ya Waziri Mkuu, Jimmy Matamwe, na Shirika la FAO liliwakilishwa na Ofisa Mtaalamu wa masuala ya Lishe wa FAO, Stella Kimambo.

Akizungumza muda mfupi kabla ya uzinduzi, Matamwe alisema kuwa serikali inatilia mkazo mkubwa katika masuala la usalama wa chakula na lishe hapa nchini, ili kuhakikisha wananchi wote wanapata chakula cha kutosha na chenye virutubisho vyote muhimu muda wote.

"Suala la ukosefu wa lishe bado ni tatizo nchini, mamilioni ya watu hususan kundi la kaya lenye kipato cha chini wako kwenye hatari kubwa zaidi," alisema na kuongeza:

"Katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe inahitajika ufuatiliaji wa mara kwa mara na kuchukua maamuzi stahiki katika utekelezaji wa jukumu la hali endelevu ya usalama wa chakula na lishe nchini."

Mfumo wa MUCHALI unazingatia mihimili minne ya usalama wa chakula ambayo ni upatikanaji, ufikiwaji wa chakula, utumiaji na ulaji wa chakula na uhakika wa upatikanaji.

Matamwe alisema kuwa kupitia mradi huu, mfumo wa tathmini na uchambuzi wa masuala ya usalama wa chakula na lishe utaboreshwa kuanzia ngazi ya wilaya pamoja na uboreshwaji wa ukusanyaji wa taarifa kwa kutumia technolojia ya simu hivyo kusaidia upatikanaji wa takwimu na taarifa husika kwa wakati, ili kukidhi mahitaji ya serikali na wadau mbalimbali.

Kwa upande wake Kimambo alisema FAO inafurahia kushirikiana na serikali kupitia wataalamu wa uchambuzi wa masuala ya usalama wa chakula na lishe, ili kuboresha mfumo huo utakaohakikisha upatikanaji wa takwimu na taarifa za masuala ya chakula na lishe kwa wakati, zenye ubora na zakuaminika.

"Watoa maamuzi wanahitaji taarifa zilizo bora na za kuaminika na kwa wakati, ili kutatua changamoto ya ukosefu wa chakula na lishe mapema kabla ya madhara yake kuwa makubwa na kuathiri watu wengi," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jesca Mbogo (kulia), akisalimiana na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Adadi Rajabu, alipowasili wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi, kwa ajili ya ziara ya siku moja. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Takukuru yaokoa milioni 22/- kwa watuhumiwa wa ubadhirifu

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Kigoma, imeokoa Sh. milioni 22 kutokana na ubadhirifu na manunuzi hewa katika miradi ya maendeleo pamoja na ukwepaji kodi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kamanda wa Takukuru mkoani hapa, Raphael Mbwambo, alisema fedha hizo zimetolewa na watuhumiwa wanne wa ubadhirifu wa fedha za umma, matumizi mabaya ya madaraka pamoja na manunuzi hewa.

Mbwambo alisema pamoja na kulipa fedha hizo baada ya uchunguzi watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Alisema jumla ya malalamiko 142 ya vitendo vya rushwa yalipokelewa katika kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2018 na yanaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali.

Aidha, Mbwambo alisema malalamiko mengi yanatoka kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Kata, Baraza la Ardhi Wilaya ya Kigoma pamoja na watendaji wa kata, vijiji na mitaa na Jeshi la Polisi hasa usalama barabarani.

Alisema Takukuru imebaini kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha katika miradi ya ujenzi inayotekelezwa katika ngazi za chini za halmashauri mbalimbali, uchunguzi uliyofanyika kati ya kipindi cha mwezi Oktoba na Desemba, mwaka 2018, umebaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanashirikiana na wajumbe wa kamati za ujenzi kuuza vifaa hewa vya ujenzi pamoja na kuandaa nyaraka za manunuzi zenye bei ya juu kuliko bei halisi ya vifaa husika.

Kamanda huyo alisema, uchunguzi uliofanyika ulibaini kuwa wafanyabiashara wanaouza vifaa vya ujenzi wanatoa nyaraka za mauzo ya vifaa hewa kwa kamati za ujenzi na baadaye kupokea malipo kupitia katika akaunti zao za benki.

Aidha, alisema imethibitika wafanyabiashara hao kurejesha kiasi cha fedha hizo kwa wajumbe wa kamati hizo.

"Nyaraka zilizopatikana katika ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Airport, zinaonyesha kuwa jumla ya mifuko 400 ya saruji imetumika kujenga vyumba hivyo hadi hatua ya linta pekee bila kuweka sakafu wala kupiga lipu."

Aidha, alisema mwanya huo wa udanganyifu umetokana na kutokuwapo kwa usimamizi, ukaguzi na ufuatiliaji makini wa idara ya ujenzi na manunuzi katika ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mbwambo alisema, tatizo kubwa ni watumishi kutofika katika maeneo ya miradi husika badala yake kuacha kazi zote kwa kamati za ujenzi ambazo hazina weledi wa kutekeleza na kusimamia miradi hiyo.

## Wadau utalii wataka mikutano ya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KATIKA kukuza idadi ya watalii nchini, sekta binafsi imeshauri kujengwa kwa kituo kikubwa cha utalii wa biashara kitakachokuwa chachu ya kuongeza idadi ya watalii wa mikutano na matukio kama ambavyo inafanyika Berlin, Ujerumani.

Meneja Mkuu wa Maendeleo, Anthony Chamanga, kutoka Taasisi ya Wakulima wa Mbogamboga, Matunda na Maua nchini (Taha), alisema hayo jijini hapa jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa mafunzo unaoendelea jijini hapo kuhusu utalii biashara.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Bodi ya Utalii (TTB), na kuishirikisha Taasisi ya Africa Tourism Partners ya Afrika Kusini kama watoa mafunzo, yanahudhuriwa na wadau mbalimbali wa utalii wakiwamo wawakilishi wa kumbi za mikutano za taasisi za serikali, hoteli na sekta binafsi.

Chamanga alisema kwa muda sasa Tanzania haijawahi kuwa na mkutano mkubwa wa kimataifa kama ule wa Agra uliofanyika mwaka 2012 na Sullivan Summit, yote iliyofanyika jijini hapa.

Kufanyika kwa mikutano kama hiyo kunatoa fursa ya kuongezeka kwa idadi ya watalii, kukua kwa sekta zingine za biashara kama hoteli, usafiri na wakulima kupata soko la mazao yao kama vile mbogamboga na matunda.

"Tunaomba kuwa na kituo kimoja kikubwa cha mikutano na maonyesho kama ambavyo inafanyika Berlin, Ujerumani. Katika mji huo, kila siku kuna shughuli za mikutano na maonyesho mbalimbali ya kimataifa yanaendelea," alisema.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mikutano ya Kimataifa ya Utalii (MICE), kutoka TTB, Dorothea Massawe, alisema kuna haja ya kuwa na ukumbi mkubwa wa mikutano na maonyesho utakaotosheleza idadi kubwa ya watu kuanzia 5,000 hadi 10,000 kwa wakati mmoja.

Alisema TTB pamoja na kutangaza utalii wa vivutio mbalimbali vilivyopo nchini, imejipanga kuongeza nguvu katika mazao mengine ya utalii wa biashara unaohusiana na mikutano na maonyesho.

Alisema utalii wa mikuano una faida nyingi kwa kuwa washiriki baada ya kumaliza mikutano yao, wanapata fursa ya kutembelea maeneo ya vivutio au hata kupanga safari zingine peke yao kuja nchini.

ITV

JARIDA LA WANAWAKE:
SAA 1:00 USIKU

KATIKA KIPINDI CHA LEO MTANGAZAJI WAKO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA FATMA KANGE AKIELEZEA UMUHIMU WA WAJASIRIAMALI KUWA NA BARCODE AU KITAMBULISHO CHA BIDHAA KWA NJIA YA ALAMA ILI WAWEZE KUUZA KIMATAIFA.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

**PROJECTS CREATE EMPLOYMENT** AND GENERATE MONEY:Learn project proposal DESIGNING,Find project DONORS,Establish project NGO:0787 505108/ 0769 505108/0716 581562

### MAGARI/VIPURI

**GARI HONDA CRV YA MWAKA 2007 INAUZWA.** INATEMBEA NA IKO KATIKA HALI NZURI SANA. BEI MAELEWANO PIGA 0755834730 AU 0755260247

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA SELF CONTAINER INA FENCE MAJI NA UMEME INAPANGISHWA** ipo Segerea kwa bibi bei 3.6 milion kwa N0754467237/0754284708


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### CHETI KIMEPOTEA



**THERESIA C NTELYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita, chenye **index namba S0620-0665** ,cha shule ya sekondari TEGETA Mwaka 2010.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nae.
Taarifa ya Polisi : **KJN/B.1/21/VOL 251**

115016902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA MUUNGANO WA TANZANIA**

### HATI YA KIAPO


Mimi **HASSANI ALLY RUGA wa TANGA,** mtu mzima, mwenye akili zangu timamu bila kushawishiwa na mtu yeyote kwa hiari yangu mwenyewe ninaapa na kuthibitisha haya yafuatao:-

1. **KWAMBA mimi HASSANI ALLY RUGA** ni mmiliki wa kiwanja **Plot No.7 BLOCK "G" eneo la MABAWA** jijini Tanga.
2. KWAMBA kwa bahati mbaya hati ya kumiliki kiwanja hicho imepotea nimefanya juhudi ya kuitafuta lakini sikufanikiwa kuipata nimefika kituo cha polisi Mabawa na kupewa loss report yenye namba **NG/RB/218/2018** ya tarehe **16/02/2018.**
3. **KWAMBA** naiomba ofisi yako itambue nilikuwa na hati ya kiwanja lakini imepotea, kwa hiyo ninaomba kupatiwa hati nyingine kwa jina hili hili **HASSANI ALLY RUGA.**

**UTHIBITISHO.**

Nathibitisha kuwa yote niliyotamka ni ya kweli kweli tupu kwa kadri nijuavyo na kuamini kuwa ni kweli na kwa kutia nguvu tamko hili nimefika mbele ya Hakimu Mahakamani na kutia sahihi yangu kuwa ni kweli.

**MBELE YA: K.S KITOGO**
**CHEO: HAKIMU**



215016502

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ERNEST ELIAS MYENDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 649 CDD TOYOTA CHASER GX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **KMR/RB/48/2019.**

115017102

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ISACK CHUGU DANFORD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 721 DGZ TOYOTA RAV 4. CHASSIS** NAMBA **ACA365009976**. ENGINE NAMBA **ZAZ2429398.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KJN/RB/455/2019.**

115017002

### KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**GS GROUP LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi pikipiki yenye namba za usajili **MC 703 BQN** Aina yake **HAOJUE**. Yenye chasis namba : **LC6PCJK28HOO12897** na Injini namba **:156FMISAD2F20892** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi, Taarifa ya Polisi: **MOR/TR/RB/2417/2018.**

215016702


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223 311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## OVERMARS kuula Arsenal

**LONDON,** England

ARSENAL wana matumaini ya kumteua winga wao wa zamani, Marc Overmars (pichani chini), kuwa mkurugenzi wa ufundi.

Huku uvumi ukienea kwamba Mkurugenzi wa sasa, Sven Mislintat, anapanga kuondoka, Arsenal sasa wamekuwa wakisaka mtu sahihi wa kuchukua nafasi hiyo.

Habari kutoka ndani ya Arsenal zinasema kwamba jina la Overmans ndilo linalopewa nafasi baada ya kuonekana kuwa na mafanikio makubwa kule Ajax ambako alikuwa akifanya kazi ya ukurugenzi wa soka.

Akiwa na klabu hiyo, Overmars ndiye aliyehusika na kuwalea na kuwapaisha nyota kama Frenkie de Jong na Matthijs de Ligt, ambao wote wamekuwa wakiwaniwa kwa udi na umba na klabu kubwa barani Ulaya zikiwamo Barcelona na Paris Saint-Germain.

Overmars pia ndiye aliyewaruhusu wachezaji kama Christian Eriksen, Toby Alderweireld na Davinson Sanchez, ambao wote walitua pale Tottenham Hotspur.

Mholanzi huyo alitumia misimu mitatu akiwa na Arsenal kati ya mwaka 1997 na 2000, na alikuwa sehemu ya kikosi kilichotwaa ubingwa wa Ligi Kuu na FA mwaka 1998.

Alihamia Barcelona, lakini bado amekuwa na mahusiano mazuri na Arsenal.

Mislintat ambaye ni raia wa Ujerumani anatajwa kama anaamua kurudi kwa miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich baada ya kushindwa kuelewana na Mkurugenzi wa Soka wa Arsenal, Raul Sanllehi.





# MOURINHO: Nimekataa ofa tatu

**LONDON,** England

KOCHA Jose Mourinho amesema amekataa ofa tatu za kuwa kocha tangu alipofutwa kazi na Manchester United, huku akipinga madai kwamba anapendelea mtindo wa 'kupaki basi'.

Raia huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 55, alisema hakuna hatua aliyopiga kutokana na matokeo duni ya mechi, huku akijitetea kwamba sio muumini wa kupaki basi.

"Falsafa yangu inategemea. Ningependa kuwa katika klabu ambayo itanipatia mazingira sawa na yale ambayo kocha wa Liverpool anapata na mwenzake wa Manchester City.

"Tayari nimekataa ofa tatu za kazi kwa sababu nahisi sio ninazozitaka," alisema Mourinho katika mahojiana yake ya kwanza hadharani baada ya kufukuzwa Man United.

Mourinho ambaye aliiongoza Man United kushinda Kombe la Ligi pamoja na lile la Europa, anaeleweka kuwa na mkataba katika klabu hiyo ambayo inamzuia kuzungumzia kuhusu kuondoka kwake.

Lakini alizungumzia kuhusu masuala kadhaa akiwa mgeni maalumu katika televisheni ya habari za michezo ya Bein Sports:

Katika visa tofauti, Mourinho alikuwa akimkosoa winga Anthony Martial, beki wa kushoto Luke Shaw na mshambuliaji Marcus Rashford, ambaye mchezo wake umeimarika chini ya ukufunzi wa Ole Gunner Solskjier.

Lakini alisisitiza kuhusu mchezaji mmoja ambaye alimtaka kutomkosoa, huku Mourinho akihisi kwamba ni ishara ya wachezaji wa kisasa kuwa na hisia nyingi.

"Hivi majuzi nilipokuwa nikiwafundisha, mchezaji mmoja aliniambia tafadhali unaponikosoa nikosoe katika faragha sio mbele ya wachezaji wengine," alisema.

"Nilimuuliza kwa nini? Alinijibu, kwa sababu kwa hadhi yangu mbele ya wachezaji wengine unaponikosoa sihisi vema.

"Siku hizi lazima uwe mwerevu katika kuwasoma wachezaji wako, na kujaribu kuunda mazingira bora."

Alilinganisha hali hiyo na ile ya mshambuliaji wa zamani wa Chelsea, Didier Drogba, ambaye alishirikiana naye katika Uwanja wa Stamford Bridge aliposhinda ligi mara mbili 2005 na 2006.

"Drogba ni mchezaji ambaye unapozidisha shinikizo kwake ndipo anavyozidi kuimarika katika mchezo wake," alisema Mourinho.

"Kuna wachezaji ambao unapowapatia shinikizo ndipo sasa wanapozidi kuimarika.

"Kuna wengine ambao fikra yao na tabia zao sio nzuri. Walilelewa katika mazingira tofauti, kwa wao kufikia kilele cha soka kila kitu walipata kwa urahisi. Kuna wengine hawatoi hisia sawa, hutoa maneno machafu na mara nyingine wengine ni hatari."

Mourinho alisema kuwa falsafa yake ilitegemea timu aliyokuwa akiifundisha, lakini akapinga shutuma kwamba kikosi chake kilipendelea kucheza mchezo wa kulinda lango ama 'kupaki basi.

Alizungumza kuhusu mtindo wa soka aliocheza akiwa Chelsea na kusema: Je, unajua sifa hiyo ya 'kupaki basi 'ilianza wapi?

# Man City wafikisha mabao 100 msimu huu

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City ni timu ya kwanza katika ligi kubwa tano barani Ulaya kufunga mabao 100 kwenye mechi za mashindano yote msimu huu.

Vijana hao wa Pep Guardiola walifikisha mabao hayo baada ya dakika 18 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England juzi, Jumapili dhidi ya Huddersfield Town, wakati shuti la Danilo lilipochepushwa na beki Christopher Schindler na kuzama wavuni.

Miamba wa Ufaransa klabu ya Paris Saint-Germain, ambao walishinda mabao 9-0 dhidi ya Guingamp Jumamosi kwenye Ligue 1, ndio wanaowakaribia Man City, lakini wamepitwa kwa mabao 10, kwa kuwa kwa sasa wana 90.

Barcelona imefunga mabao 78 msimu huu, saba zaidi ya wanaowafuata kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Sevilla.

Tottenham wao wamefunga mabao 70 na Arsenal wakitikisa nyavu mara 68, wote wakiwa wamewazidi vinara wa Ligi Kuu ya England, Liverpool wenye mabao 65.





# LUIZ:

## Bado tunaimani kubwa na Sarri Chelsea

**LONDON,** England

DAVID Luiz amesisitiza kwamba kocha wa Chelsea, Maurizio Sarri, anapata sapoti yote kutoka kwa wachezaji, licha ya kocha huyo raia wa Italia kuwashutumu baada ya kufungwa 2-0 na Arsenal.

Blues hao sasa nafasi yao ya nne kwenye msimamo inaonekana kunyemelewa baada ya kupokea kipigo cha nne msimu huu, na Sarri alidai kwamba wachezji hawaonyeshi kucheza kwa hamasa.

Baadhi ya wachambuzi wa soka wamebainisha kwamba, Sarri anafanya kosa kubwa kuwashtumu wachezaji wake hadharani.

Hata hivyo, Luiz amedai kwamba wachezaji wote bado wana imani kubwa na Sarri na kwamba alikuwa sahihi kuwa na hasira."Hakuwa na furaha, lakini hakuna mtu aliyekuwa na furaha," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil akinukuliwa na Jarida la FourFourTwo.

"Ni staili yetu, ni falsafa yetu, nafikiri kama ungeuliza tangu mwanzo wa msimu kama Chelsea wanaweza kutawala mchezo, ningesema hapana.

"Na tuna uwezo wa kufanya hivyo, kama timu bora duniani. Hii ndio falsafa yetu, naamini katika hilo, hivyo najua kwamba tunahitaji kuimarika zaidi, kama timu yoyote duniani.

"Kitu alichofanya Sarri hadi sasa ni cha kupongezwa, kama ilivyo kwa Man City na Liverpool, ambao wanacheza soka la kuvutia.

"Kilichofanywa hadi sasa ni cha kupongezwa, hivyo tunahitaji kuimarika zaidi kwa sasa. Sidhani kama wachezaji hawachezi kwa kujituma, kwa kuwa kila mmoja anafanya kazi yake vizuri tu."

Chelsea inatakiwa kujiimarisha zaidi wakati itakapokutana na Tottenham Alhamisi kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali ya Kombe la Carabao, mwanzo walifungwa 1-0.

## Man Utd yamwania kinda wa Benfica

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa ipo kwenye mipango ya kutaka kutoa ofa ya kumsajili, Joao Felix (pichani chini), kutoka Benfica.

'Dogo' huyo mwenye umri wa miaka 19, tayari amekuwa akihusishwa na kutakiwa na klabu za Barcelona, Manchester City na Liverpool, na ripoti zinasema ofa ya paundi milioni 60 zilizotolewa na 'Vijigoo wa Anfiled' ilikataliwa mwezi uliopita.

Gazeti la Mirror limedai kwamba Liverpool bado wana nia ya kutaka kumsajili Felix na pengine wanaweza kutoa ofa nyingine, lakini sasa watakabiliwa na upinzani kutoka kwa Manchester United, ambao wamekuwa wakimwinda nyota huyo.

Aidha, imeripoti kuwa bei ya Felix ni pauni milioni 105 na alisaini mkataba mpya miezi miwili iliyopita. Mkataba wake unamalizika 2013 na Benfica.

Kama klabu yoyote itafika bei ya kumnunua Felix, anaweza kuwa mchezaji chipukizi wa pili kuwa ghali zaidi baada ya Kylian Mbappe.

Felix kwa sasa yupo katika kikosi cha kwanza cha Benfica na anaonekana kuimarika siku hadi siku na amefunga mabao manne katika mechi 10 alizocheza hadi sasa.

Ingawa Felix anatumia zaidi mguu wa kulia, lakini ana uwezo wa kucheza winga ya kushoto, kiungo na mshambuliaji.

Ameichezea timu ya taifa ya Ureno chini ya umri wa miaka 21 mara kumi na kama ataendelea na kiwango chake cha sasa kuna uwezekano mkubwa wa kuitwa timu ya wakubwa.



# Barcelona wamchunia Carlos Vela



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA haitamshawishi kumsajili Carlos Vela wakati huu wakiendelea kutafuta mchezaji wa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Kuondoka kwa Munir El Haddadi kwenda Sevilla kumewaacha miamba hao wa La Liga wakiwa kwenye wakati mgumu wa kutafuta mshambuliaji mpya, huku Luis Suarez akibakia kuwa ndiye straika pekee wa kati hapo Camp Nou.

Kikosi hicho cha kocha, Ernesto Valverde mara kadhaa kimehusishwa na kutaka kumsajili mchezaji wa kumsaidia Muuruguay huyo.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal, Vela amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kujiunga na Barca, lakini kwa mujibu wa Gazeti la Mundo Deportivo, mchezaji huyo raia wa Mexico hatashawishiwa tena.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, kwa sasa anaichezea klabu ya Los Angeles FC na amefunga mabao 14 katika mechi 28 za Ligi Kuu ya Marekani, MLS, akiwa amehamia huko Marekani mwaka jana.

Vela ana uzoefu na maisha ya nchini Hispania, kwa kuwa alicheza huko La Liga kwa miaka sita akiwa na klabu ya Real Sociedad baada ya kutua huko kwa mkopo wa mwaka mmoja akitokea kwa 'Washika Bunduki' wa London.

Vela alifunga mabao 69 katika mechi 252 alizocheza La Liga wakati akiwa na pale Sociedad.

## HABARI MICHEZO

### KWA UFUPI

**BELLERIN AZUA HOFU ARSENAL**
ARSENAL ina hofu beki wake wa kulia, Mhispania Hector Bellerin, 23, anaweza kuwa nje ya uwanja kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki kutokana na majeraha ya goti aliyoyapata wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Chelsea Jumamosi. **(Mirror)**

**CARROLL ATAKIWA SPURS**
MSHAMBULIAJI wa West Ham, Andy Carroll, 30, ameibuka ghafla kuwa straika anayewindwa na Tottenham kuziba tatizo la majeruhi linalowaandama. **(Sun)**

**HAZARD AISUBIRISHA REAL**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard, 28, hatajiunga na Real Madrid mwezi huu, ila nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anataka kukataa ofa yoyote itakayokuja ili kujiunga na miamba hiyo ya Hispania mwishoni mwa msimu. **(Marca, via Mirror)**

**MILAN YAMFUATA PIATEK**
AC Milan imekubali kumsajili straika Mpoland Krzysztof Piatek, 23, kutoka Genoa kwa pauni milioni 30.9 - kufuatia Gonzalo Higuain kuelekea kujiunga na Chelsea. **(Guardian)**

**DE JONG AITESA BARCA**
RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amekwea pipa kuelekea Amsterdam, Uholanzi kujaribu kumshawishi kiungo wa Ajax, Frenkie de Jong, 21, kujiunga na klabu hiyo badala ya Paris St-Germain ya Ufaransa. **(Mail)**

**DARMIAN AKARIBIA JUVE**
JUVENTUS inakaribia kukamilisha uhamisho wa mkopo wa beki wa Manchester United, Mtaliano Matteo Darmian, 29. **(Guardian)**

**RODRIGUEZ KUIKATALIA ARSENAL**
MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Colombia, James Rodriguez, 27, anajiandaa kukataa kujiunga na Arsenal na kubaki kwa mkopo Bayern Munich anayoichezea akitokea Real Madrid, hadi angalau mwishoni mwa msimu. **(ESPN)**

**UNITED, LIVER MBIO MOJA**
MANCHESTER United inaweza kujiunga na Liverpool katika mbio moja za kumsajili kiungo wa Benfica na Ureno U-21, Joao Felix, 19. **(Star)**

**SARRI HATABADILI MFUMO**
KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, amesema hana lengo la kubadili mfumo wake wa uchezaji kufuatia kipigo dhidi ya Arsenal na kudai ni jukumu la wachezaji kuweza kuzoea mbinu zake. **(Times)**

**CITY, CHELSEA ZATUA BARCA**
Chelsea imetoa ofa dakika za mwisho kwa kiungo wa Barcelona, Mhispania Ilaix Moriba, 16, ambaye pia anatakiwa na Manchester City. **(Sport)**

**EMERY, OZIL HOFU TUPU**
KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, pengine yupo tayari kumrejesha kiungo Mjerumani Mesut Ozil, 30, katika kikosi cha kwanza. **(Times)**

**KLOPP HATAENDA SOKONI**
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema hatafanya usajili wowote mwezi huu, licha ya kuandamwa na majeraha katika safu yake ya ulinzi. **(Liverpool Echo)**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HIGUAIN KUTUA CHELSEA LEO

**LONDON,** England

STRAIKA Gonzalo Higuain, anajiandaa kutua jijini London leo kukamilisha taratibu zake za kujiunga na Chelsea.

Straika huyo wa Juventus anajiandaa kujiunga kwa mkopo na miamba hiyo ya Stamford Bridge hadi mwishoni mwa msimu, huku kukiwa na uwezekano wa kuongeza mkataba huo kwa mwaka mmoja zaidi.

Higuain aliachwa katika kikosi cha AC Milan kilichokuwa kikijiandaa kwa mechi dhidi ya Genoa jana, na kocha Gennaro Gattuso alimkosoa kwa uamuzi wake wa kuondoka kipindi hiki akitumikia klabu hiyo kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Juventus.

Na inaeleweka Chelsea inatarajia kumpokea straika huyo leo, Jumanne kukamilisha taratibu za uhamisho wake.

Gattuso alisema: "Ninakubaliana na uamuzi wake hakika angeweza kufanya zaidi na pengine tungeweza kumsaidia yeye kuwa fiti vizuri.

"Ninataka kuwa mwaminifu na ninyi nyote. Tumekuwa na mazoezi mabovu leo kutokana na tetesi zote hizi. Tumezungumza baada ya mazoezi na sikumjumuisha yeye kwa utayari wa mechi hii."

Lakini pande zote zimekubali kumruhusu Higuain kuvunja mkataba wake wa mkopo Milan na kwenda kuanza mwingine Chelsea.

Maurizio Sarri anahitaji kuongeza nguvu katika kikosi chake baada ya kuwalaumu wachezaji kutokana na namna walivyoshuka dimbani kukabiliana na Arsenal na kuchezea kichapo cha mabao 2-0.

Lakini Higuain anaweza kuleta suluhisho katika safu yake ya ushambuliaji ambayo Alvaro Morata ameshindwa kuiongoza vema. Maoni ya Sarri yanafanana na ya Antonio Conte msimu uliopita wakati alipoanza kuzungukazunguka kuelekea kutimuliwa.

Sarri sasa ameamua kugeukia kukosoa wachezaji jambo ambalo linaonekana ni kama mtangulizi wake, Conte, Jose Mourinho, Andre Villas-Boas wote walitimuliwa na Chelsea vipindi vilivyopita.

Na mshambuliaji wa zamani wa Chelsea, Tony Cascarino, anadhani sasa kibarua cha Sarri kipo mashakani na amesema anaweza kutimuliwa kama kutua kwa Higuain hakutaleta mabadiliko chanya.

HABARI MICHEZO

# STEVEN PIENAAR KUTUA DAR KUWAFUNDA U-17

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZAJI wa zamani wa timu ya Everton FC ambaye kwa sasa ni Balozi wa klabu hiyo, Steven Pienaar, anatarajiwa kutua jijini Dar es Salaam wiki hii kwa lengo la kuwahamasisha wachezaji chipukizi hapa nchini.

Wakati wa ziara yake, mchezaji huyo atafanya mazoezi ya pamoja na timu ya taifa ya vijana chini ya miaka 17 (U-17) ambayo inajiandaa kwa ajili ya michuano ya AFCON ambayo inatarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam Aprili mwaka huu.

Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema ziara ya Pienaar hapa nchini ni moja ya mikakati ya muda mrefu ya SportPesa ya kukuza mpira wa miguu hapa nchini.

"Kwa muda mrefu SportPesa imekuwa na mikakati dhabiti ya kukuza mpira wa soka hapa nchini na kwa sababu ndio imeifanya timu ya Everton FC kwa kushirikiana na SportPesa imeamua mchezaji huyo kufanya ziara hapa nchini. "Huyu ni Mwafrika mwenzetu ambaye alikuwa na wakati mzuri wakati alipokuwa akiichezea timu ya Everton FC na kwa sasa ni mmoja wa mabalozi wa timu hiyo. "Ziara yake pamoja na kufanya mazoezi na timu ya U-17 itakuwa na hamasa kubwa na hasa kwa wakati huu, ambapo timu hiyo inajiandaa na michuano ya AFCON ambayo itafanyika nchini," alisema Abbas.




Meneja wa Game Supermakert ya Mlimani City, Josephat Okumu (kushoto), akimkabidhi mshindi wa droo ya pili, Grace Mboka, mkazi wa Goba jijini Dar es Salaam, Sh. 500,000 aliyoshinda katika Promosheni ya "Tusua Ada na Omo" inayoendelea. Droo hiyo ilichezeshwa mwishoni mwa wiki katika Supermarket hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

## 'Tusua Ada na Omo' yawatoa wakazi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa jijini Dar es Salaam, wameendelea kupata ahueni ya ada katika kipindi hiki kigumu cha Januari kwa kunufaika na Promosheni ya "Tusua Ada na Omo".

Katika droo ya pili iliyochezeshwa mwishoni mwa wiki ilitoa washindi watatu na kufanya jumla washindi sita, ambao wamejishindia Sh. milioni tatu kwa kila mmoja kuibuka na Sh. 500,000 baada ya kufanya manunuzi katika Supermarket za Game, Choppies Mlimani City na Shoppers Mikocheni, Masaki na Mbezi.

Washindi hao walipatikana baada ya kununua Omo na kuingia rasmi kwenye droo kubwa inayochezeshwa kila Jumamosi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja wa Omo, Upendo Mkusa, kwanza aliwapongeza washindi wote haswa watatu waliopatikana katika droo ya pili kukamilisha idadi ya washindi sita ambao ni Grace Mboka mkazi wa Goba aliyeshinda katika Supermaket ya Game Mlimani City, Shidu Abubakari, alishinda katika Supermaket ya Choppies Mlimani City na Lilian Patrick, aliyeshinda katika Supermakert ya Shoppers, ambapo aliwaomba pesa walizoshinda wakazielekeze kwenye elimu kwa watoto wao kama kauli mbiu ya kampeni inavyosema "Tusua Ada na Omo".

"Kampuni ya Unilever kupitia bidhaa yake ya sabuni ya Omo wanatambua kama jamii ya Watanzania imetoka katika kipindi cha Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, hivyo wakaona ni jambo jema kuungana na wanafamilia katika kipindi hiki cha watoto kwenda shule kuchangia kwa namna moja ama nyingine kupitia promosheni hii," Upendo alisema.

"Katika promosheni hii ya Tusua Ada na Omo jumla ya Sh. milioni sita zitatolewa kwa washindi 12 kwa kila mmoja kujishindia Sh. 500,000.

"Ushiriki uko wazi kwa kila mtu, lakini lazima uwe na umri zaidi ya miaka 18, ni lazima ununue Omo 1kg moja ziwe pakiti mbili au 500gm pakiti ziwe nne au 3.5kg pakiti moja, ambapo mshiriki atapewa kuponi itakayoingizwa kwenye droo ambayo huchezeshwa kila Jumamosi."

## Simba SC watakiwa wakajifue ughaibuni

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Simba, Abdulghan Msoma, amekitaka kikosi cha timu hiyo kikaweke kambi ya muda nje ya nchi kwa ajili ya kujiandaa na mechi yake ijayo ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayochezwa Februari 2, mwaka huu.

Hata hivyo, Simba ambayo imerejea nchini juzi usiku ikitokea Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ilikofungwa mabao 5-0 na wenyeji AS Vita, imebanwa na ratiba ya mashindano ya Kombe la SportPesa ambayo yanaanza kutimua vumbi jijini Dar es Salaam kuanzia leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msoma ambaye sasa anawaongoza vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, KVZ alisema endapo Simba wataenda kuweka kambi ya muda nje ya nchi, ndio watapata nafasi ya kurekebisha upungufu walionao na si jambo lingine.

Msoma alisema kikosi cha Simba bado kina nafasi ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa wanayoshiriki, lakini wanahitaji muda tulivu wa kumaliza makosa waliyonayo ambayo yameonekana katika mechi zao mbili walizocheza.

"Hii si mara ya kwanza, narudia tena, ushauri wangu kwa Simba waipeleke timu nje ya nchi kwa ajili ya mazoezi, wakajifungie mahali hata kama ni siku nne kabla ya kucheza na Al Ahly, hapo wataweza, la sivyo mambo yanaweza kuwa mabaya zaidi," alisema kocha huyo.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi tatu sawa na AS Vita iliyopo nafasi ya pili, huku Al Ahly ikiongoza Kundi hilo la D ikiwa na pointi nne, wakati JS Saoura ya Algeria yenye alama moja ikiburuza mkia.

Simba inatarajia kushuka uwanjani kesho kuwania ubingwa wa Kombe la SportPesa Super kwa kuwakaribisha AFC Leopards kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

## Jang'ombe Boys yarudi sokoni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WACHEZAJI wanne wa timu ya Jang'ombe Boys inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar wameachana na klabu hiyo na kuelekea kwingineko katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili jambo linaloilazimu kwenda sokoni kusaka mbadala, imeelezwa.

Nyota hao walioondoka ni pamoja na Kassim Suleiman ambaye amesajiliwa na timu ya Kagera Sugar inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara wakati wengine watatu wamejiunga na Mlandege pamoja na KVZ za visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Jang'ombe Boys, Ali Othman Kibichwa, alisema licha ya kupoteza wachezaji hao muhimu katika timu yake, anatarajia kusajili wachezaji wengine watano ili kukiimarisha upya kikosi chake.

Kibichwa alisema anatarajia kusajili washambuliaji, beki wa kati na beki wa pembeni ili kuziba mapengo yaliyopo katika timu hiyo na ili waweze kumaliza msimu huu wakiwa katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.


"Tumepoteza wachezaji muhimu ambao wamesajiliwa na timu nyingine, hivyo basi tunataka kusajili wachezaji muhimu ili waweze kuweka timu katika nafasi nzuri ya ligi itakayotuepusha kushuka daraja," alisema.

Aliweka wazi kwamba wanalenga kusajili wachezaji chipukizi kwa sababu wanaamini hao wataisaidia timu yao ili ifanye vizuri kutokana na kuwa na hamu zaidi ya kujituma.

Timu ya Jang'ombe Boys yenye pointi 26 iko katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Michezo
Jumanne Januari 22, 2019
Nipashe

## Higuain kutua Chelsea leo



HABARI UK. 30

CHUMA HICHO...



Leroy Sane akimzidi ujanja kipa wa Huddersfield, Jonas Lossl na kuifungia Manchester City bao la tatu wakati ikishinda 0-3 ugenini juzi. **PICHA: DAILY MAIL**

# AUSSEMS AREJEA NA MOTO MPYA SIMBA

Asema subirini mechi ijayo kwa Waarabu baada ya SportPesa Cup huku...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha Simba kikirejea salama nchini kutoka Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Aussems, amesema nafasi ya timu yake kusonga mbele itajulikana kabla ya mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, Aussems alisema kwa sasa nguvu za timu yake zinaelekezwa katika mashindano ya SportPesa Cup ambayo yanaanza leo jijini Dar es Salaam kwa kushirikisha timu nane kutoka Tanzania na Kenya.

Kwenye michuano hiyo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tayari kila timu katika Kundi D linalojumuisha Al Ahly ya Misri, AS Vita (DR Congo), Simba (Tanzania) na JS Saoura ya Algeria imeshacheza mechi mbili na zimebakia na mechezo minne.

Na Simba itamalizia hatua hiyo nyumbani dhidi ya AS Vita ambayo Jumamosi iliyopita iliwapa kichapo cha mabao 5-0.

Akizungumza na gazeti hili jana mchana, Aussems alisema matokeo waliyoyapata huko Kinshasa yanasikitisha, lakini bado hakuna timu yenye uhakika wa kusonga mbele kutoka katika kundi lao.

Aussems alisema anatarajia kuendelea kukiimarisha kikosi chake na anaamini mambo yatakwenda vizuri kabla ya kushuka uwanjani kuwakabili Waarabu wa Misri, Al Ahly mapema mwezi ujao.

Mbelgiji huyo alisema mechi zote za hatua hiyo ni ngumu na zenye ushindani kwa sababu wachezaji wanaendelea kujifunza na kuimarika kadri wanavyosonga mbele.

"Nasema kuwa bado nafasi iko wazi kwa kila timu, tumepoteza mchezo, lakini tumejifunza vitu kadhaa, tunavifanyia kazi na natarajia tutakuwa na matokeo tofauti katika mechi inayofuata," alisema Aussems.

Mshambuliaji Mnyarwanda wa timu hiyo, Meddie Kagere, alisema mechi dhidi ya AS Vita imemalizika na sasa wanajipanga kukabiliana na michezo inayofuata ikiwamo Kombe la SportPesa Cup.

"Kila siku tunajipanga kusaka ushindi, tunajua tunakabiliwa na mashindano mengi, kwangu binafsi sipendi kuongea sana, nitaongea uwanjani," alisema Kagere ambaye ametua Simba akitokea Gor Mahia ya Kenya.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao mwaka jana walifungwa katika mechi ya fainali na Gor Mahia, wataanza kampeni ya kuwania kombe la michuano hiyo inayoandaliwa na wadhamini wao wakuu kesho dhidi ya AFC Leopards ya Kenya.

## Yanga yaitafuta tiketi ya Everton

**Na Mwandishi Wetu**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, watashuka dimbani leo kuanza kusaka tiketi ya kucheza na Everton ya England kwa kuvaana na Kariobangi Sharks ya Kenya kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Yanga itashuka dimbani leo kwenye mechi hiyo ya ufunguzi ya michuano ya SportPesa Cup, ikitoka kuchezea kipigo cha kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu dhidi ya Stand United Jumamosi.

Aidha, kabla ya mechi hiyo ya Yanga dhidi ya Kariobangi Sharks itakayopigwa kuanzia majira ya saa 10:15 alasiri, itatanguliwa na mchezo kati Singida United dhidi ya Bandari FC ya Kenya katika uwanja huo majira saa nane mchana.

**Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema matayarisho ya michuano hiyo awamu ya tatu yamekamilika, huku timu zikiwa zimeanza kuingia Dar es Salaam tangu mwishoni mwa wiki.**

Akizungumzia kuhusu viingilio, Tarimba alisema SportPesa kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), wamekubaliana kutoza viingilio vya chini ili kuweza kuvutia mashabiki wengi. "Mashabiki wa mpira wa miguu kutoka Tanzania na Ukanda huu wa Afrika Mashariki kwa jumla watalipa Sh. 10,000 kwa VIP A, huku VIP B na VIP C wakilipa Sh. 5,000 na mzunguko Sh. 2,000 kwa mechi za robo fainali.

"Nia yetu ni kuweza kufanya mashabiki wa michuano ya SportPesa Cup kujisikia wamedhaniwa na hivyo nawaomba wajitokeze kwa wingi kushangilia timu zao kwa kuwa bingwa wa michuano hii atacheza mechi ya kirafiki na moja ya timu inayoshiriki Ligi Kuu nchini Uingereza ya Everton FC," alisema Tarimba.

Kesho Simba itashuka katika dimba hilo kuvaana na AFC Leopards kwenye michuano hiyo ambayo Gor Mahia ni bingwa mtetezi kufuatia kulitwaa taji hilo mara mbili mfululizo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002